Jamii Ya Zama Za Furaha

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

Istanbul - 2022

© Kimechapwa na Erkam 2022 / 1443 H

Jamii Ya Zama Za Furaha

Othman Nuri Topbash

Jina la Asili: Asr-ı Saadet Toplumu
Mwandishi: Othman Nuri Topbash
Msimamizi Mkuu: Abdi Mohamed Adam
Mfasiri: Shaaban Khambi
Mhariri: Ibrahimu H. Kabuga
Msanifu jalada: Altinoluk Graphics
Kupangiliwa vizuri na: Sarkhan Isgandarov
Nijat Garibov
ISBN: 978-9944-83-668-5
Mchapaji: Erkam Printhouse
Anuani: Ikitelli Organize Sanayi Bölgesi
Mah. Atatürk Bulvarı, Haseyad
1. Kısım No: 60/3-C Başakşehir,
Istanbul, Turkey
Simu: (+90-212) 671-0700 pbx
(+90-212) 671-0748
Barua pepe: info@islamicpublishing.org
Tovuti: www.islamicpublishing.org
Language: Swahili / Kiswahili

ERKAM PUBLICATIONS

Jamii Ya Zama Za Furaha

Othman Nuri TOPBASH

ERKAM PUBLICATIONS

DIBAJI

Sifa za Milele na shukrani kwa Mola wetu Mkarimu kwa kutujaalia kuwa katika *Ummah* wa Mtume Kipenzi wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na kumleta kwa wanadamu kama mnara wa maadili bora! ...

Salamu na amani ya miele iende kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), familia na Maswahaba zake, kwa kuwalea Maswahaba na kuwainua mithili ya nyota mbinguni, na kwa kuwapa wanadamu zawadi kubwa isiyokuwa na kifani ambayo ni *Asr-u Saadah*, yaani Zama Furaha!...

Zama za Furaha, ni kipindi kile cha wakati wa amani na furaha, ambapo binadamu walifurahia maisha mazuri na yenye neema nyingi mno.

Zama hizi za Furaha zilikuwa ni zama zilizopata heshima ya kuishi ndani yake Mtukufu Mtume (s.a.w); zama ambazo zilishuhudia kuteremshwa kwa Qur'an Tukufu ambayo ni chemchem ya mwongozo kwa wanadamu wote. Ni zama hizo za kipekee ambazo zilishuhudia kuibuka kwa kizazi adhimu cha Maswahaba, ambao walibeba Nuru ya Utume na kui-

peleka katika ardhi na maeneo ya mbali zaidi; Maswahaba ambao walijenga ustaarabu wa wema, hekma na haki kwa kufikia vilele vya juu kabisa vya upendo, huruma na ukomavu katika historia ya dunia hii.

Neno Asr-u Saadah pia limekuwa linatumika, mara kwa mara, kumaanisha kipindi na zama za Makhalifa Waongofu, mpaka kwa kizazi kilichofuata cha *Tabiun* na hata mpaka kilichofuata baada ya hicho, yaani *Tabiu Tabiin.*

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) anasema: "Zama zilizokuwa bora katika ummah wangu ni za wale walioishi katika zama zangu, kisha watakaofuata baada yao na kisha wale wataokufuata baada yao ..." (Bukhari, As-habu'n-Nabi, 1)

Kwa hivyo basi *Asr-u Saadah* ni zama zilizojaaliwa neema bora zaidi katika historia. Ni zama ambazo hazina mithili yake katika historia ya Uislamu na ni kipindi kilichopendwa na kitaendelea kukumbukwa.

Baadhi maoni ya wanazuoni wanasema kwamba kiapo kilichoapwa juu ya *Asr*, au 'zama', katika *Surat al-Asr*, ni kinakusudia zama hizi za *Asr-u Saadah*, kwa kuwa ni katika kipindi hiki ambapo haki (ukweli) ulitenganishwa bayana dhidi ya batili (uongo).

Kinyume na mtazamo wa kiulimwengu na wa kinafsi, Zama za Furaha, hakikuwa kipindi cha furaha na faraja za Kimaada. Bali ulikua ni wakati mgumu

wa mapambano na maisha ya taabu. Lakini pia ulikuwa ni wakati ulioshuhudia neema tele ambazo ni maisha ya Mtume Mtukufu (s.a.w) pamoja na ujio wa dini ya Uislamu.

Ulikua pia ni wakati ambapo ziliasisiwa kanuni bora ambazo zilihakikisha maisha ya amani na furaha ya binadamu wote katika dunia hii na Akhera

Ni zama zilizoshuhudia ukatili, kinyonyaji na genge la dhulma vikiondolewa kupitia haki, uadilifu na maadili mema.

Ni zama zilizoshuhudia mapinduzi makubwa kabisa kuwahi kutokea katika historia ya mwanadamu, ambapo kiza cha tamaa kiliondoshwa kwa nuru tukufu ya hali ya kiroho na nyoyo zikakombolewa kutoka kwenye kifungo cha mwili. Kwa kifupi, ni zama ambazo mwanadamu alianza kuuacha uovu na kuelekea kwenye furaha ya milele.

Hivyo basi, ili kuzielewa na kuzijua zaidi neema za kipeke za Uislamu ambao humuongoza mja kutoka kwenye giza na kwenda kwenye nuru, anatakiwa kuingia katika anga la Zama za Furaha.

WAPENDWA WASOMAJI!

Lengo letu katika kitabu hiki, ambacho ni mkusanyiko wa makala mbalimbali zilizoongezewa baadhi

ya mifano ya ziada, ni kuhakikisha watu wanakuwa na uelewa wa zama hizo adhimu, zama tukufu. Kuhakikisha hili linafanyika na kutoa mwanga mzuri zaidi juu ya tukio hili lenye kushangaza katika maendeleo ya shaksia ya mwanadamu, tumejitahidi kulibainisha na kulifanya lieleweke zaidi kwa kutoa mifano mingi zaidi ya kimaadili, wema na mambo yenye kuvutia ya zama hizo.

Katika hili, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Dr Murat Kaya na kumwomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kumlipa juhudi zake malipo yasiyo na mwisho.

Othman Nuri TOPBASH

Desemba 2009

بسم الله الرحمن الرحيم

وَالسَّابِقُونَ الْأَوَّلُونَ مِنَ الْمُهَاجِرِينَ وَالْأَنْصَارِ وَالَّذِينَ
اتَّبَعُوهُمْ بِإِحْسَانٍ رَضِيَ اللَّهُ عَنْهُمْ وَرَضُوا عَنْهُ

"Na wale walio tangulia, wa kwanza, katika Wahajiri na Ansari, na walio wafuata kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, na wao wameridhika naye; na amewaandalia Bustani zipitazo mito kati yake, wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa." (at-Tawbah, 9:100)

Jamii Ya Watu Wa Zama Za Furaha

Jamii Ya Watu Wa Zama Za Furaha

Wakati wa Zama za Ujahiliya, binadamu alizungukwa na wimbi kubwa la giza. Ujinga uliokithiri na kila aina ya dhambi na uhalifu uliovuka mipaka, vyote hivi vilikuwa ni sehemu ya maisha ya zama hizo. Mparaganyiko ulikuwa ukionesha sura yake mbaya bila kuchoka. Majangwa ya Arabia yaligeuka kuwa bahari za damu zinazotoka kwenye majeraha ya watu wasio na hatia.

Sheria na haki vilikuwa milki ya wale wenye nguvu tu. Wale waliokuwa na nguvu waligeuka madhalimu wakiwakandamiza wanyonge na wale wasioweza kujitetea. Marehemu Akif Mehmed anasimulia aina ya ukatili huo akisema: "Kwa yule asiyekuwa na meno, basi ndugu zake wangemtafuna." Hii ndio ilikuwa hali ya kila siku.

Wanyonge waliokuwa wamekanyagwa chini ya miguu katili ya madhalimu, walipambana kila siku ili wapate kuishi, huku mayowe yao ya uchungu yakipita bila kusikika.

Imani zenye kudhalilisha katika Zama za Ujahiliya

Imani ya kweli ilipotoshwa. Baadhi, wakidhani kwamba Mwenyezi Mungu yuko mbali sana, waliamini kwamba uwezo wa Mwenyezi Mungu ulinasibishwa katika vitu ya asili kama vile mawe, miamba, moto, miti au milima, ambavyo kwao waliviona vitu vitakatifu. Kulikuwa na baadhi ambao waliabudu vitu kama jua na mwezi na walivithamini na kuvitukuza wakidhani wangeweza kumfikia Mwenyezi Mungu Mtukufu Mtukufu.

Wengine walikuwa wakiabudu viumbe visivyoonekana kama malaika, majini au mashetani. Waliamini kwamba kwa kuabudu na kuheshimu vizuri viumbe hivi pengine vingeweza kuwatetea mbele za Mwenyezi Mungu.

Pia kulikuwa na washirikina ambao, kwa namna moja au nyingine, walidai kuwa wanamuamini Mwenyezi Mungu Mtukufu lakini kwa upande mwingine wakimshirikisha na washirika au vitu ambavyo walivitengeneza kwa mikono yao wenyewe.

Pamoja na kudai kuwa wao ni "watoto wa Ibrahim na Ismail-rehma na amani juu yao", walikuwa wameishaitelekeza tangu mapema kabisa imani ya *tawheed,* yaani imani ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mmoja, na walikuwa wamesimama mbali kabisa

na njia hii ya imani ya Mungu Mmmoja ambayo Mitume hao wawili walikuwa wameshikamana nayo na ambavyo walikuwa wamewausia kuifuata.

Washirikina walimshirikisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kila kitu unachokiona au kukifikiria.

Na kulikuwa na kundi lingine lililokataa kabisa kuwepo kwa Mwenyezi Mungu na siku ya akhera, wakidhani kwamba kila kitu ni sehemu ya ulimwengu huu unaoonekana kwa macho. Harith, (mume wa Halimah) baba wa kambo wa Mtume Mtukufu rehma na amani za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, alikuja Makkah katika miaka ya mwanzo ya Utume kwa ajili ya kumtembelea Mtukufu Mtume (s.a.w). Alipowasili, alikutana na washirikina, ambao walimwambia: "Ewe Harith, una habari ya anachokisema mwanao?" "Jambo gani analosema?" Aliuliza Harith. "Amekuwa akidai kuwa Mwenyezi Mungu atawafufua watu baada ya kifo. Pia amesema kwamba Mwenyezi Mungu ana makazi mawili yanayoitwa Pepo na Moto, ambapo atawalipa mema watiifu na kuwaadhibu waovu. Madai hayo yamepelekea kuvuruga utaratibu na kuigawa jamii yetu!"

Harith hatimaye akafika kwa bwana Mtume (s.a.w) na akamuuliza: "Mwanangu, huo mgogoro ni wa nini kati ya wewe na watu wa kabila lako? Wanalalamika kuhusu wewe, wakidai kwamba umewahakikishia watu kwamba watafufuliwa baada ya kifo,

ambapo watapelekwa aidha mbinguni au motoni?" "Ndiyo, baba yangu kipenzi", alijibu Mtume Mtukufu (s.a.w). "Hivyo ndivyo nilivyosema na ndivyo ninavyoamini. Na natamani nikushike mkono na nikuambie khabari hizi njema hivi sasa, na kukuelezea jinsi gani maneno hayo yalivyo na ukweli!" Harith (r.a) baadaye akasilimu, na kadri muda ulivyokuwa ukienda alianza kuona matunda ya misingi ya imani ya Uislamu. Baada ya kuukubali Uislamu alikuwa akisema:

"Natamani kama angenishika mkono siku ile na kunieleza ukweli wa maneno yake na asiniache, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, mpaka akaniingiza Peponi!" (Ibn Ishaq, Sirah, s 218;. Suhayli, Rawd'ul-Unuf, 284-285)

Wakati huo wa Zama za Ujahiliya, watu walikuwa wamezama katika imani nyingi za uongo. Walikuwa katika msiba mkubwa wa kibinaadamu, wakitamani kupata kitu kitakachowatambulisha kama wanadamu, kitu kitakachoitambulisha akili na uwezo wao wa kufikiri. Ilikuwa vigumu kupata fikra salama au mawazo sahihi. Mawazo na fikra potofu vilikuwa vikiyatawala maisha yao. Matokeo yake, wanawake walinyanyaswa katika jamii, akina mama walifukuzwa na huku mabinti wakionekana kama wanaleta aibu katika familia.

Siku moja, Swahaba mmoja alienda kwa Mtume (s.a.w) akasema:

"Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, hakika sisi tulikuwa watu wajinga. Tulikuwa tunaabudu masanamu, na kuwazika mabinti zetu hai. Mimi nilikuwa na binti yangu mdogo ambae alikuwa ananipenda. Nakumbuka…Nilikuwa nikimwita angeweza kuja mbio akifurahia. Siku moja nilimwita tena na yeye alikuja kwangu mbio. Nikamshika mkono na kuanza kutembea yeye akiwa kando yangu kuelekea karibu na kisima chetu. Kisha niliikamkamata mikono yake, nikamtupa katika kisima hicho, maneno ya mwisho kutoka kwake ni mayowe aliyokuwa akipiga, 'Baba, Baba!' akiwa anadidimia humo kisimani."

Baada ya kusikia habari hizi za kusikitisha machozi yalimlengalenga kwa huruma Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Swahaba mwingine aliyekuwapo jirani akamlaumu yule Swahaba aliyekuwa akieleza habari hizi za kusikitisha: "Wewe, huna haki ya kumhuzunisha Mtume wa Mwenyezi Mungu!"

"Muache", aliingilia kati Mtume (s.a.w) "Anataka kutoa yale yaliyo katika kifua chake, mpe nafasi aseme kile kilicho katika kifua chake". Kisha akamqcukia yule mtu, akasema: "Rudia kile ulichokua unaekielezea!"

Wakati yule Swahaba akirudia kisa chake hicho, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akaanza kutokwa na machozi, mpaka ndevu zake zikalowa na machozi. Akamgeukia yule bwana, kwa mara nyingine tena,

akamwambia: "Mwenyezi Mungu amesamehe dhambi zilizofanywa katika kipindi kile cha Ujahiliya kwa wale ambao wamekuwa Waislamuu. Sasa aanza upya maisha yako" (Darimi, Muqaddimah, 1)

Ubinadamu na utu ulikuwa umesimama kwenye ncha ya miale ya moto mkali. Jamii iliharibika kiroho, kwani watu walikuwa katika ncha ya kuangamia kabisa. Kisha Uislamu ukaja kuwaokoa kutokana na maangamizi hayo na kuwafanya kuwa watu wa jamii ya mfano wa kuigwa. Mwenyezi Mungu, Mtukufu, anasema katika Qur'an:

"Na shikamaneni kwa ahadi ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja na wala msifarakane, Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu mlipokuwa maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu kwa neema yake mkawa ndugu; na mlikuwa pembezoni kabisa mwa shimo la Moto, naye akawaokoa kutokana na hayo, Namna hii Mwenyezi Mungu anakubainishieni dalili zake ili mpate kufuata njia ya haki." (Al-i Imran, 103)

Kmtumikia Mwenyezi Mungu na Kuwahudumia Viumbe Wake Yaliyopuuzwa kwa Maslahi ya Kidunia

Mifumo halisi ya Ibada ilishasahaulika muda mrefu na ile iliyobaki ilipotoshwa. Walibadilisha

mifumo mingi ya kuabudu Kama hijja na sadaka ya kuchinja na kuifanya iwe kwa maslahi yao. Walidai kuzipa umuhimu ibada hizo, lakini kumbe walikuwa wakihamasisha uovu bila ya wao kujua. Kwa mfano, mahujaji waliizunguka *kaabah* wakiwa uchi, kisha baada ya hapo ndipo wangeweza kuvaa mavazi yao ya gharama ili kujionesha kwa kiburi na majivuno. Kanuni pekee ya uhusiano wa kijamii ilikuwa ni mabavu. Haki na utukufu vilikuwa kwa wale wenye nguvu tu; hapakuwa na hata chembe ya haki na uadilifu. Hapakuwa na athari hata kidogo ya amani na uthabiti katika jamii.

Mabaki ya Sifa za Kimaadaili Yalipotoshwa na Kugeuzwa

Ilifikia hatua ambapo maadili machache ambayo yalibaki yalikua kwa ajili maslahi binafsi. Yalifanywa ima kwa kupita kiasi au kwa nadra kabisa. Jambo jema lilifanywa kama nyenzo ya kuonesha nguvu na fakhari ya mtu. Mtu alikuwa akijifanya karimu na kufanya mauaji ya kutisha: Waliwazika binti zao hai kwa minajili ya kulinda hadhi zao na heshima yao katika jamii.

Kwa hakika, mwanadamu aliyeishi Zama za Ujahiliya alikuwa mbabe kupita kiasi, silaha ilikuwa karibu kila alipokuwepo. Ujasiri ndio ilikuwa alama yake ya utambulisho. Ujasiri huo ulipimwa kwa idadi ya

watu aliowaua kwa chuki za kikabila. Ujasiri wa mtu ulitokana na ujivuni na ubinafsi wake. Ili kuonesha mabavu na ukuu wa kabila lake na yeye mwenyewe binafsi, ilimpasa mtu kuonesha ana nguvu na ujasiri kiasi gani. Vita visivyoisha kati ya kabila moja na jingine viliwamaliza kiidadi na kiroho.

Kukomesha mila mbaya za kijahiliya, Uislamu ulibadilisha mfumo mzima wa maisha na kuleta kanuni nzuri na kamilifu za kuishi. Uliwaondolea hasira na ukaidi wao na badala yake ukawafundisha matumizi mazuri ya tabia nzuri kama subira, upole, huruma, uvumilivu na kutendeana haki.

Uislamu ulizitakasa nafsi zao na kuondoa ujivuni wao kutoka katika mioyo yao, ukaielekeza hali ya ujasiri wao kwenye malengo matukufu. Uliwafundisha kutumia ujasiri wao katika mambo mazuri zaidi, kama vile kurejesha haki na Ukweli.

Mtu wa zama za kijahiliya alikuwa mkarimu na mpole. Lakini sifa hizi zilitumika tu katika kutaka sifa yake mwenyewe nay a kabila lake. Tamaa yake kuu ilikuwa ni kutukuzwa, kupata umaarufu na kulinda sifa yake miongoni mwa watu, na kuamsha hisia za heshima na kuwatia hofu pia wapinzani wake. Hivyo Ilikuwa ni kawaida kwa mtu kuchinja kondoo sita au saba kwa wakati mmoja na kuchoma maini tu kwa ajili ya karamu na kisha kutupa masalia mengine ya minofu kwa madhumuni ya kujionesha tu.

Wakati Uislamu ukiendelea kustawisha ukarimu na upole, pia ukapandikiza maadili mema ndani ya nyoyo zao. Wakati wakifanya ukarimu, Waislamuu walikuwa wakijiweka mbali na hali ya kujionesha-*riyya*- wakitamani kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Walitambua kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Mmliki wa kweli na wa pekee wa viumbe vyote, na hilo ndilo lililokuwa ndani ya nyoyo zao.

Hivyo hivyo, utajiri wote ni wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na wanadamu wamepewa kama amana tu ambayo inatakiwa kurudi kwa mwenyewe pindi atakapoihitaji. Wana mamlaka yenye kikomo kwenye utajiri na mali hizi za Mwenyezi Mungu na kwa yule aliyepewa neema hii na MwenyeziMungu basi anapewa dhima na majukumu fulani juu ya utajiri huo. Hivyo kama mja ameaminiwa na Mwenyezi Mungu, akapewa dhima hii ni muhimu kwake kuitumia mali hiyo kutokana na jinsi alivyoelekeza Mwenyezi Mungu ili kupata radhi za Mwenyezi Mungu. Ni muhimu kwa mja kutafuta na kuitumia mali kwa njia halali aliyoelekeza Mwenyezi Mungu Mtukufu, na katika kumshukuru Mwenyezi Mungu kutokana na kutunukiwa mali hiyo ni lazima mja amtumikie Mwenyezi Mungu kwa kuwahudumia viumbe vyake.

Daima Mtukufu Mtume (s.a.w) alikuwa akisema:

"Mkono unaotoa ni bora zaidi kuliko mkono unaopokea".

Lakini wakati wa kutoa, mja anatakiwa kutoa kwa ajili ya Mwenyezi tu, bila kutarajia malipo ya kidunia na kujiepusha na kiburi. Qur'an imewausia na kuwafundisha binadamu wote kwa kusema:

"Sisi tunakulisheni kwa wajihi wa Mwenyezi Mungu Hatutaki kwenu malipo wala shukrani." Uislamu pia ulikataza *israf*. Hivyo kwenye Zama za Furaha kusingelitupwa hata kipande kimoja cha nyama ya kondoo aliyechinjwa kinyume na Zama za Ujahiliya.

Pia kwa kuonesha ukarimu na kutokuwa na ubinafsi, ilikuwa si kawaida kwa nyama kupita karibu familia saba tofauti na kurejea kwenye sehemu ile ile ilipotoka mara ya kwanza.

Maisha ya jangwa yalimdunisha kifikra mja wa Zama za Ujahiliya kuhusu dhana ya uhuru. Wasingetambua mamlaka na uasi wa aina yoyote dhidi ya mamlaka ambayo yalikuwapo kwa wakati huo. Matokeo yake, hapakuwapo na mamlaka ya Kuu. Mshikamano wa kijamii ulikua unategemea sana ukabila.

Kulikuwa hakuna mfumo wala taasisi ya sheria iliyokuwa inafuata na kutekeleza sheria zilizokuwapo. Inapotokea hali ya kutoelewana ilikuwa aidha kuitwa wasuluhishi wasiozingatia maadili au yataamuliwa kwa mujibu wa mabavu.

Uislamu ulipinga wazo la jumla la uhuru kuwa katika milki ya watu wachache tu. Tamko la Qur'an ya kwamba mtumwa mwenye imani ana thamani kuliko mtu huru asiyeamini kuwepo kwa Mwenyezi Mungu liliwakasirisha sana makafiri. Upinzani mkali dhidi ya Uislamu ulitoka katika kundi la watawala wa (maqureish). Walimwambia Mtume Mtukufu - amani na baraka juu yake - kuwa walikuwa tayari kusaini mkataba nae endapo tu wangewaondosha watumwa na wale wasiojiweza mbali na Mtume wa Mwenyezi Mungu. Wazo hili lilikataliwa kabisa na MwenyziMungu.

Maadili ya Uislamu yaliweka uhuru wa kimaanawi kwa kujenga msingi wa kimaadili. Ikaweka hatua za kinga ili kila mtu aweze kuweka kikomo cha uhuru wake mwenyewe ndani ya utambuzi wake. Qur'an inasema:

"Na hakika tumemuumba mtu, nasi tunayajua yanayo mpitikia katika nafsi yake. Na Sisi tuko karibu naye kuliko mshipa wa shingoni mwake." (Qaf:16)

"Je, hawajui kwamba Mwenyezi Mungu anayajua yale wanayofanya siri na yale wanayofanya wazi?" (Al-Baqara: 77; al-An'am, 3)

Hivyo Muislamu anatakiwa si tu aweze kudhibiti vitendo vyake, lakini hata tabia yake ya siri iliyo ndani ya moyo wake. Ari hii muhimu ilileta mabadilko na mapinduzi makubwa katika moyo, mtazamo na tunu za maisha ya mtu wa Zama za Ujahiliya. Matumizi ya

nguvu katika kupata suluhu hayakupata nafasi tena, badala yake upatanishi kwa hukumu ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume wake ndio ulichukua nafasi. Waislamuu wote walikuwa na moyo wa kumtii Allah na lile hitajio la "kumtii Mwenyezi Mungu, Mtume wake, na kiongozo kutoka miongoni mwenu."

Umoja na mshikamano baina ya wao kwa wao wakati wa Zama za Ujahiliya ulikua katika dhana ya ukabila (*asabiyya*). Mtu wa Zama za Ujahiliya alikuwa na moyo mgumu na katili dhidi ya watu wasio jamii yake. Thamani ya viumbe wengine ilipimwa kwa manufaa unayotoa kwao, hivyo kama huna unachokifanya kwao ajili yao maana yake kwamba huna faida kwao pia. Hapakuwapo na kizuizi wala mipaka kuzuia mtu mmoja kuharibu mali ya wengine, pia hakuona tabu mtu hata kidogo kutowalipa ujira wafanyakazi wake.

Uislamu uliondoa hisia za ubaguzi wa watu kushikamana kwa misingi ya kikabila, ukarudisha upendo na mahaba ambapo hapo mwanzo ulitoweka kutokna na mila zao mbaya. Uislamu ukafundisha jinsi ya kuwachukulia binadamu wote kama ndugu na kuwaweka kwenye jengo la imani ya Kiislamu mfano wa binadamu mwenye miguu mingi inayobeba mwili mmoja.

Mtume Mtukufu (s.a.w) siku moja alisema: "Msaidie ndugu yako, hata kama yeye ni myon-

yaji au myonywaji"! Maswahaba walishangaa kusikia kauli iliyoonekana kuwa ya ubaguzi wa rangi wa zamani ikitoka katika kinywa cha Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Mmoja wao aliuliza: "Kama ndugu yangu anadhulumiwa, Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, nitaweza kumsaidia. Lakini jinsi gani naweza kumsaidia ikiwa yeye ni mwenye kudhulumu? Mtume (s.a.w) akasema:

"Utamzuia na yeye kudhulumu na pia kuzuia pasitokee dhuluma." (Bukhari, Mazalim, 4;., Ikrah 6 Pia tazama, Tirmidhi, Fitan, 68).

Hapo Uislamu ukarekebisha ufahamu na uelewa wao wa kusaidiana kutoka kusaidiana wao kwa wao na kuheshimiana na kuufanya uwe kwa kila mtu. Kuanzia hapo, kusaidiana kukawa katika wema na uchamungu; kuwasaidia wengine katika maovu na uadui sasa kukapigwa marufuku.

Muujiza Mkuu wa Mtume (s.a.w): Mtu wa *Asr-u Saadah*

Mmoja wa wasomi wakubwa katika methodolojia ya sheria za Kiislamu aitwae Qarafi (aliyekufa mwaka 684), anasema:

"Kama Mtume wa Mwenyezi Mungu asingeleta muujiza wowote wa kuthibitisha Utume wake, Mas-

wahaba aliowalea wangetosha kuwa muujiza mkubwa wa kuthibitisha utume wake."

Hivyo, maadili ya kiroho yaliyoletwa na Mtume (s.a.w), mafundisho yake ya nje na taathira yake ya ndani yakuwa kiungo muhimu sana, kiasi kwamba aliiondoa jamii ya kijahiliya ambayo hapo awali ilikuwa imezama katika unyama, jamii yenye ujinga wa hali ya juu wa kutoweza hata kutambua misingi ya ubinaadamu, akaiinua juu kwenye daraja ya juu kabisa kama ya 'Maswahaba'. Jamii aliyoijenga bado inahusudiwa na kutamaniwa mpaka leo hiii.

Mtu mjinga na asiyekuwa na huruma alibadilika kuwa mwenye maendeleo, mtu katili akabadilika kuwa mstaarabu na watu wenye utovu wa maadili na waliojipaka tuhuma wakabadilika kuwa waja wema wa Mwenyezi Mungu Mtukufu walioishi kwa upendo na hofu ya kumuogopa Mwenyezi Mungu Mtukufu ikapandikizwa ndani ya nyoyo zao.

Fikiria mtu katili na mwenye chuki ambaye katika Zama za Ujahiliya aliweza kumtoa mtoto katika tumbo la mama yake na kisha kumzika hai…Mtu katili kiasi cha kutoa mateso makali kwa watumwa ambao aliwaona kama bidhaa rahisi tu kwake!

Ni watu hawa ambao baadaye walipata muongozo wa Uislamu ambao uliwapa fursa ya kujitambua. Ni watu hawa hawa ambao hapo mwanzo walikuwa

wajinga na walioshindikana lakini wakaweza kurekebika na kutengeneza ustaarabu wa wema.

Watu hawa ambao katika Zama za Ujahiliya walikuwa wagumu kama wawe katika viwango vya ubinaadamu, walipoanza kutekeleza kwa vitendo sheria na maadili ya Kiislamu katika maisha yao, waliweza kupaa kwenye vilele virefu vya ubinaadamu.

Zama za Furaha Ziliwaibua Watu wa Mfano

Kutoka katika jamii ya kijahiliya ambayo ilishindwa kuwa na mtu mwema hata mmoja kwa karne nyingi, ghafla waliibuka watu kadhaa waliokuwa mfano wa kuigwa waliojaliwa viwango bora vya maadili mazuri kwa mafundisho ya kiroho ya Mtume (s.a.w). Watu hawa waliibeba elimu walioipata kutoka katika Qur'an na Sunnah wakaiepeleka kwenye pembe zote nne za dunia, kama miale ya hekima na maarifa. Hawakuonesha dalili yoyote ya kuchoka au kukata tamaaa na badala yake mioyo yao ilikuwa makazi ya upendo wa Mwenyezi Mungu na kuwatazama viumbe kwa jicho la Muumba. Waliichukua nuru iliyokuwa imeshuka jangwani, wakailinda na kuutawanya Ukweli na uadilifu wake kwa wanadamu wote.

Waislamu wa *Asr-u Saddah* waliolelewa na malezi mazuri ya Mtume wakawa mfano wa hali ya juu kwa wanadamu wote, wakawa watu wa jamii ya yenye

maarifa, busara, hekima, upendo na haruma, ambao sio tu kwamba walimjua Mtume kwa nje bali pia kwa ndani, wakimjua kwa nyoyo zao. Hizo zilikuwa zama za tafakuri, zama za kumjua Mwenyezi Mungu na Mtume wake.

Maswahaba waliiweka *tawhid* katikati ya kitovu cha nyoyo na fikra zao. Walifanikiwa kuyavunja maslahi ya kidunia, tamaa za umimi na miungu ya matamanio ambayo kuzikumbua na kuzivamia nyoyo. Waliufanya uhai na mali kuwa nyenzo, hawakuvifanya kuwa lengo. Huruma ikastawi mioyoni mwao. Kuitumikia haki ikawa ndio njia ya maisha yao. Juhudi na kujitoa kwa moyo viliyapamba maisha yao. Walijitoa kwa moyo kiasi kwamba, Swahaba alikuwa akisafiri umbali wa mwezi mmoja kwenda tu kuthibitisha hadith fulani aliyokuwa akiijua, na licha ya kusafiri umbali wote huo, lakini alikuwa tayari kurudi nyumbani baada ya kuona kuwa mtu aliyekuwa akimtafuta muda wote huo alikuwa akimchezea shere farasi wake kwa kumpa mfuko mtupu usio na chakula; akiona kuwa uongo ni miongoni mwa mambo yasiyostahili kwa kazi adhimu ya kuthibitisha hadith ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w).

Abu'l-Aliya, mmoja wa maimamu nguli wa kipindi cha *Tabiun* anaelezea zaidi kuhusu umakini huu wa Kiislamu kama ifuatavyo

"Tunapokwenda kwa mtu kwa lengo la kuuulizia kuhusu *hadith* fulani, tulikuwa tukiangalia namna alivyokuwa akifanya ibada yake ya swala. Tukimuona anaitekeleza vizuri tulikuwa tukiwaza 'bila shaka mambo yake mengine anayafanya vizuri' na kisha huenda mbele yake na kumsikiliza. Lakini tukimuona anatekeleza ibada yake hiyo vibaya, tulikuwa tukiwaza 'bila shaka mambo yake mengine anayafanya vibaya' na hivyo tulikuwa tukiondoka bila kumsikiliza." (Darimi, Muqaddimah, 38/429)

Maswahaba walipata nini kutoka kwa Mtume Aliyebarikiwa (s.a.w) ?

- *In'iqas* au kupokea taathira kutoka kwenye hali ya kiroha ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, kuwa sehemu yake; chemchem kubwa ya nuru kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w) kwenda kwa Maswahaba.

- Kupata *aqrabbiyya*; ni mafunzo na mazoezi ya jinsi ya kupata ukaribu na Mwenyezi Mungu Mtukufu, na kumtambua ndani ya moyo.

Elimu mpya kabisa ya kumjua Mwenyezi Mungu Mtukufu, kuijua dunia na nafsi ilipandikizwa ndani ya Maswahaba mithili ya jua linaloakisi katika kioo. Kuandamana na hali ya kiroho ya Mtukufu Mtume (s.a.w) ndiyo iliyokuwa raghba yao kuu. Kwa namna hiyo, ukweli na wema wote vilidhihirika katika

maisha yao, kama ambavyo batili ilijidhirisha kwa ubaya wake wote. Kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu katika kila walilolifanya na katika kila pumzi waliyovuta ikawa ni sehemu ya maisha yao.

Walikuwa wakarimu, wenye huruma, wasio na inda na wenye kupendelea nafsi za wengine kwanza. Wakiwa wameshikamana mno na mapenzi ya kupenda ibana, maisha yao yalikuwa tu kwa ajili ya kumtumikia Mwenyezi Mungu.

Maswahaba pia walipitia mitihani na majaribu ya imani kipindi walipokuwa Makkah. Mwishowe wakaweza kuondosha vikwazo vyote vilivyokuwa vinakinza imani yao. Ulifika wakati walitakiwa kutoa mali zao na utajiri wao wote kuonesha imani yao na hakika walifanya hivyo. Kuna mahali walihitajika kutoa hata nafsi zao na bado walikuwa tayari kufanya hivyo bila kusita. Hamasa ya imani yao thabiti ndiyo iliyowahamisha kutoka Makka ilitoa msingi wa kimaanawi na kiroho kwa ajili ya ustaarabu wa aina yake ambao ungeasisiwa katika mji wa Madina.

Jamii ya Kiislamu iliyosambaza amani kwa kila kiumbe cha Mwenyezi Mungu iliundwa huko Madina. Majangwa yaliyokuwa yamechomwa kwa moto wa uovu, yakapata amani iliyokuwa inakosa kwa muda mrefu. Hata mimea nayo ilineemeka sana kwa mazingira ya amani; kukata miti na majani kiholela kulipigwa marufuku. Mafunzo ya uadilifu katika Uis-

lamu hayakuwaokoa wanadamu pekee bali hata kwa wanyama na mimea ambao walikosa neema hii kwa muda mrefu.

Uislamu Unasambaa Kwa Haraka kama Mwanga wa Alfajiri

Mipaka ya jamii ndogo ya dola ya Kiislamu huko Madina ilijumuisha jumla ya familia mia nne (400), miaka kumi baadaye ikasambaa mpaka nchi za Iraq na Palestina.

Mpaka muda Mtume (s.a.w) anaondoka katika ulimwengu Maswahaba walikuwa na uwezo na uimara wa kusimama na kukabiliana na uvamizi kutoka Warumi na Waajemi. Lakini viwango vyao vya maisha vilibadilika kidogo ukilinganisha na miaka kumi kabila. Waliendelea na maisha ya kujizuilia. Vitu kama kufanya israfu, uchoyo na kujifaharisha havikuwa na nafasi katika maisha yao. Waliamini siku zote kwamba kaburi lilikuwa linawasubiri kesho. Hivyo, daima walijizuia kujilimbikizia neema za dunia na kuzitumia kwa fujo. Badala yake, kutokana na imani ya hali ya juu waliyokuwa nayo, walizitumia neema hizo kama nyenzo za kuwaongoza wanadamu kuelekea kwenye wokovu. Waliyatengeneza maisha yao katika mfumo wa kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwa hakika, miongoni mwa sababu za kuchomoza na kusambaa kwa Uislamu, miongoni mwa watu wanyonge, waliodhulumiwa na kuonewa ni ule ukweli kwamba Maswahaba walionesha tabia na utambulisho adhimu wa Kiislamu kila walipokwenda. Kama wanafunzi wa Mtume (s.a.w), Maswahaba walijiepusha na choyo na waliwaangalia kwa jicho la huruma kila kilichoumbwa na Mwenyezi Mungu (s.w) na ari ya kusambaza ujumbe wa Uislamu kwa watu hao.

Marafiki wakubwa wa Maswahaba walikuwa Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Jamii ambayo hapo awali haikuwa ikijua kusoma sasa ikawa imefikia kilele cha ustaarabu; nyoyo zao zikajaa hamasa ya kuwa watu wenye thamani mbele ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

Hisia za kiroho ziliimarika na kustawi

Maswahaba walifikia hatua kubwa inayoweza kufikiwa kwa akili na moyo. Kwa kujiweka huru dhidi ya *nafsul-ammara* (nafsi yenye kuamrisha maovu), walipata moyo uliokamilika. Walijenga mazoea ya kujiuliza juu ya matendo yao mbalimbali.

Kwa kupambana na matamanio ya nafsi zao na kuimarisha vipawa vyao vya asili, walipiga hatua kubwa ya kuelekea kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Japokuwa hapo zamani walikuwa na sifa za unyama, lakini sasa walikuwa wamezivaa sifa na tabia za kimalaika.

Kutoka katika lindi la ujahili na kila aina ya uovu, waliokolewa mpaka kufika kwenye ufukwe wa huruma na moyo safi kupitia nuru ya kiroho iliyotoka kwenye ulimwengu wa ndani wa Mtume (s.a.w). Wakawa ni watu wa kupigiwa mfano, ambao waliutazama ulimwengu kwa macho ya huruma.

Kutoka kuwa mtu aliyeweza kumtoa mtoto mchanga toka tumboni kwa mama yake na kumzika hai, ghafla mtu huyo akageuka kuwa malaika wa huruma. Moyo wake ukawa kimbilio salama kwa wenye wasiwasi na wanyonge katika jamii, na kuwa hifadhi salama inayotoa miale ya matumaini na usalama kwa yatima na wajane.

Omar (r.a) ambaye hapo awali alikuwa na moyo mgumu, sasa akageuka kuwa mtu mwenye hisia na ulaini wa moyo usiokuwa wa kawaida alioupata kutokana na Uislamu, kiasi kwamba alikuwa akisema: "Naogopa kuitwa kwa Allah kama mbwa mwitu atakutwa akipora kondooo katika mto Tigris" (Ibn Abi Shaybah, Musannaf, VIII, 153)

Wakati wa usiku alikuwa akibeba kiroba cha unga mgomgoni mwake akienda kuwatafuta watu wenye kuhitaji na kusikiliza vilio na huzuni zao.

Alishughulishwa sana na dhima ya ustawi na furaha ya *ummah*.

Mfano mwingine ni ule wa Abdullah Ibn Masud (r.a) wakati wa vita vya Badr. Akiwa amekaa juu ya kifua cha Abu Jahl baada ya kumwangusha chini, mshirikina huyo alimtupia tusi lifuatalo: "Umepanda mlima wenye muiniko mkali mchunga kondoo mpumbavu wewe." (Ibn Hisham, II, 277)

Ibu Masud (r.a) akawa "mchunga kondoo wa kawaida" aliyekuwa akidharauliwa na wanajamii wengine. Baada ya kupokea muongozo na mafundisho mikononi mwa bwana Mtume (s.a.w) mwenyewe, moyo wake ukatakasika na kuwa na kina kirefu kama bahari, akawa kitovu cha ishara za Kimungu.

Shule ya Kufa ni moja ya vituo vikubwa vya sheria za Kiislamu vilivyonzishwa kutokana na kumbukumbu ya Swahaba huyu. Wanasheria wengi wa Kiislamu akiwemo Imamul-A'dham Abu Hazifa, mwanazuoni wa kwanza wa sheria za Kiislamu, alitoka katika kituo hiki. Kituo hiki cha mafunzo na elimu kiliibua watu kama hao wenye uelewa wa hali ya juu; watu kama vile Solon na Hammurabi, ambao wanatambulia duniani kama wanasheria nguli, wasingeweza kulinganishwa na Abu Hanifa hata kidogo.

Mchango wa Abdullah Ibn Masud (r.a) utakumbukwa katika historia ya Uislamu kila unapotaja taaluma yeyote ya Kiislamu.

Watu hao walikuwa mifano hai ya muujiza wa Qur'an, mhimili wa malezi bora, hekima na tunu zote za mwanadamu.

Akili na Moyo Vilikuwa Sawia katika Utendaji Kazi

Utendaji kazi wa akili na moyo, ambao uliwapeleka Waislamu wa zama hizo kwenye ukamilifu, ulikuwa ni utendaji kazi wa pamoja baina ya nyenzo hizo mbili. Kwa kuifanya shauku na upendo viendelee kuwa hai, waliweza kuimarisha uwezo wao wa kutafakari.

Waliishi kwa kuamini kwamba maisha ya duniani si lolote si chochote na ni majaribu tu ya kupita. Mioyo yao ikajengeka na imani kuwa uwezo wa Mwenyezi Mungu ni mkubwa na haushindi kitu chochote katika ulimwengu huu.

Katu hawakuonesha dalali yeyote ya kuchoka kulingania Uislamu kufika nchi za Asia ya kati mpaka mpaka China kwa ajili ya kusambaza ujumbe wa Mwenyezi Mungu na kukemea maovu.

Akiongozwa na amri ya Qur'an inayomkataza kujitupa katika maangamizi kwa mikono yake, Abbu Ayyub Al Ansari (r.a) alithubutu kujiunga katika safari ya kijeshi kwenda Istanbul licha ya kuwa na umri zaidi ya miaka 80. Mwisho, mwili wake ulipokelewa

na kuzikwa Istanbul kama kumbukumbu ya harakati zake. Kifo chake kiliwahamasisha wale waliobaki kiasi cha kuweza kuinyakua Andalus.

Uqbah Ibr Nafi (r.a) wa zama za *Tabiun* alitumwa Afrika wakati wa kipindi cha utawala wa bani Umayya. Aliikamata Quyrawan na akamteua Zuhayir Ibn Qys kama Kiongozi. "Nimeiiza roho yangu kwa Mwenyezi Mungu na nitapambana milele na wale wanaomkana", kisha akamwambia Zuhayr, akimwelekeza ndoto zake na matarajio yake endapo atatokewa na chochote.

Uqbah akiendelea na mapambano yake bila kuchoka. Kitu pekee kilichosimamisha na kumfanya asiendelee mbele ni bahari. Akiwa amesima kando ya bahari alisema maneno yafuatayo:

"Ewe Mola! Kama si kizuizi cha hii bahari ningeendelea kupambana katika njia yako na kuikamata miji mbalimbali." (Ibn'ul-Athir, al-Kamil fi't-Tarikh, Beirut, 1385, IV, 105-106)

Karne tatu za mwanzo za Waothamaniyya waliojitokeza baada yao na ambao msingi wao ulianzishwa na wapiganaji 400 tu ulikuwa ni muendelezo wa zama za Maswahaba.

Kutafakari Ndiyo iliyokuwa Nguzo

Jamii ya kijahiliya ambayo hapo mwanzo ilikuwa ikiishi gizani iligeuka kuwa "Jamii yenye Maarifa ya kweli" kupitia muongozo wa Mtume Aliyebarikiwa (s.a.w). Giza liliiondoka kuipisha nuru ya mchana, na msimu wa baridi ukaondoka kuupisha msimu maridhawa wa machipuo. Kiwango cha kufikiri kiliongezeka. Watu wakaanza kuangazia jinsi mwanadamu anavyostawi kutoka kwenye tone la maji, jinsi miti inavyokuwa kutokana na mbegu ndogo na mifano kama hiyo katika viumbe vingine. Maisha yao yaliendana na vile namna anavyotaka Mwenyezi Mungu (s.w). Hapakupata kuishi viumbe wenye upendo huruma na mapenzi baina yao kama wao.

Kulingania Uislamu ndio Kazi Waliyoipenda na Kuifurahia mno

Maswahaba walionesha tabia nzuri sana za Kiislamu. Wakiwa ni wenye kuvumilia shida za namna zote, walikuwa wakitaka radhi za Mwenyezi Mungu katika kila pumzi waliyovuta katika maisha yao. Kutokana na mkondo huo wa kiroho, waliamrisha mambo mema na mazuri kwa vitendo na kuwazuia wengine kufanya maovu na mambo yanayokiuka maadili. Kipindi kizuri na wanachokifurahia zaidi wao ni kile kipindi cha kuwafikishia wengine ujumbe wa *tawhid*.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) hakuwa akikutana na wanawake mara nyingi kama alivyofanya kwa wanaume katika kazi ya kulingania Uislamu. Guzayya (r.a), alikuwa ni mwanamke aliyeukubali Uislamu kule Makkah, alisaidia sana kuulingania Uislamu. Alikuwa akikutana na wanawake wenzie wa Kikureyshi kwa siri na kuwalingania Uislamu. Aliendelea na shughuli hii mpaka pale washiriki walipogundua. Walimtenza nguvu na kumpeleka uhamishoni pamoja na kundi la watu wa Daws, ambao walikuwa wakiondoka Makkah kwa wakati huo.

Walimpandisha farasi bila kipandio na kumnyima maji. Walimtesa mpaka akapoteza fahamu na kushindwa kuona wala kusikia kwa yale mateso. Watu hao wa Daws waliposhuhudia subira, ujasiri na imani ya dhati ya bibi Guzayya (r.a) walisilimu. (Ibn Saad, VIII, 155-157; Ibn Habbib, al-Muhabbar, p. 81-82, 92; Abu Nuaym, Hilya, II, 66-67; Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 447)

Baada ya kupona, mama Cuzayya (r.a) alihamia Madina baada tu ya Mtume (s.a.w) kuondoka. Baadhi ya ripoti zinasema kwamba alikwenda kwa bwana Mtume (s.a.w) kama balozi wa kabila la Abduqays.

Siku moja mwana mama mmoja alipokuwa akipeleka maji kwa watu wa kabila lake alikutana na Mtume (s.a.w) na kushuhudia miujiza yake. Mwana mama huyo aliporudi kwa watu wake aliwasimulia aliyoyaona, waliposikia hayo wote wakasilimu.

Watumwa wanawake pia hawakuwa nyuma katika kuweka juhudi zao za kutangaza Uislamu. Msichana mmoja kutoka Isfahan, Uajemi ambaye alikuwa amesilimu kabla ya Salman (r.a) ndiye aliyemuelekeza Salman alipo Mtukufu Mtume (s.a.w).

Swahaba mwingine, wakati anasubiri kuuawa akiwa kwenye mikono ya washirikina alipewa fursa ya dakika tatu tu za mwisho za kuomba. Aliwashukuru na kusema, "Hii ina maana mmenipa dakika tatu kuwalingania Uislamu!"

Katika kuangazia umuhimu wa *tabligh*, Abu Hurayrah (r.a) alikuwa kisema:

"Tulikuwa tukisikia maneno yafuatazo miongoni mwa Maswahaba: Siku ya Malipo mtu atashikwa kwa utepe wa kitambaa katika shingo yake na mtu mwingine ambaye kamwe hakupata kumjua. Huyo mtu atauliza: Unataka nini kutoka kwangu ili hali Mimi hata sikujui wewe?' huyo mtu mwingine atasema huku akimvuta 'Pamoja na kuniona mimi nikitenda maovu duniani, kamwe hukunionya mimi na kuniambia kama ni uovu!' Mtu huyo ataendelea kumshitaki mwezi wake katika mahakama ya sheria ya Mwenyezi Mungu Mtukufu."

Walishikamana na Qur'an

Hata mazingira na hali ngumu ya namna gani, havikuwazuia Maswahaba kumuenzi Mtukufu Mtume (s.a.w) na Qur'an.

Abu Talha (r.a) siku moja alimuona Mtume akifundisha Qur'an wanafunzi wa Suffa huku akiwa amesimama. Mtume (s.a.w) alikuwa amefunga jiwe katika tumbo ili kupata nguvu ya ya kustahmili njaa. (Abu Nuaym, Hilya, I, 342)

Hivyo azma kubwa ya Maswahaba ilikuwa kuelewa kitabu cha Mwenyezi Mungu, kupata mafundisho yake ya hekima na kuishi kama inavyotakikana. Waligundua ladha ya maisha katika kurudiarudia kuisoma Qur'an tena na tena, kuisikiliza na kuitekeleza katika maisha yao.

Kwa kifupi, Maswahaba waliishi na Qur'an wakiyafanyia kazi maudhui yake, wakijitoa maisha yao yote kwa ajili ya kitabu hicho cha Mwenyezi Mungu. Walionesha kiwango cha juu kabisa cha kujitoa dhabihu, ambacho hakikuwahi kushuhdiwa katika historia ya kabla yao.

Walikabiliwa na kila aina ya dhuluma na mateso, lakini kamwe hawakukitelekeza kile walichoamini. Katika kuitekeleza kwa vitendo Qur'an Tukufu, waliziteleleza mali zao zote, wakaihama hata miji yao,

wakahamia Madina, kwa maana walikuwa tayari hata kuyatoa maisha yao.

Daima Maswahaba walikuwa katika jitihada endelevu za kujifunza na kuifanyia kazi kwa vitendo kila ayah ya Qur'an Takatifu. Kamwe hawakupuuza Qur'an hata nyakati za hatari.

Abbad, (r.a), ambaye alikuwa ameteuliwa na Mtume (s.a.w) kuweka ulinzi kwa jeshi la Kiislamu, alikuwa ameanza kuswali. Adui aliyekuwa akisubiri kwa muda mrefu alianza kumtupia mishale. Ni baada tu ya kupigwa mishale miwili au mitatu ndipo Abbad (r.a) aliporukuu, akasujudu na kisha akakamilisha swala yake. Kisha alimtaarifu mlinzi mwenzake, Ammar (r.a) :

"Kwa nini usiniambie wakati alipokupiga mshale wa kwanza tu?" Ammar aliuliza kwa mshangao.

"Nilikuwa nasoma Surah ya Qur'an na mimi sikutaka kuikata sala yangu kabla ya kuikamilisha." alijibu Abbad. "Lakini wakati akiendelea kunishambulia kwa mishale nikasimamisha kusoma na nikainama kwa rukuu." Lakini kama si hofu ya kupoteza kazi ya ulinzi niliyopewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu, ningependa kifo kinikute kuliko kukatisha kisomo changu." (Abu Dawud, Taharat, 78/198;. Ahmad, III,344; Bayhaki, Dalail, III, 459; Ibn Hisham, III, 219; Waqidi, I, 397)

Maswahaba katika maisha yao waliongozwa na misingi na maudhui ya Qur'an. Kwao, kila nguzo ya Uislamu ilikuwa na ladha ya kipekee. Kila ayah kutoka kwa Allah (s.w) ilikuwa ni kama sikukuu kwao. Juhudi zote walizielekeza kwenye kuielewa vizuri na kuishi na Qur'an na kuwa mfano bora. Ni imani ya kiasi gani kwa Maswahaba wa kike ambao mahari yao walihitaji mume mtarajiwa amfundishe tu sehemu ya Qur'an anayoifahamu!

Maswahaba walikuwa na shauku na juhudi za dhati ya kuifahamu Qur'an wakiiga mfano wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na matokeo yake mji mdogo wa Madina ukajaa wasomi na *huffidhul-Qur'an.*

Mambo ya Yaliyowaelekeza Kwenye Qur'an Tukufu

- Walikuwa ni jamii isiyo na elimu, ambayo haikuwahi kuwa chini ya ushawishi na taathira ya utamaduni wowote wa kigeni. Hivyo, waliweza kuelekeza nguvu yao yote ya kiakili na kiroho kwenye Qur'an. Matokeo yake, walizalisha utamaduni adhimu; utamaduni ambao ulizuia dhuluma na kila aina ya ukandamizaji na kuitambua haki ya kuishi kwa kwa kila kiumbe hapa duniani.

Maisha ya kiroho ya umakini wa Kiislamu ni muhimu kwa binadamu yeyote. Msimamo mzuri wa

kiroho tu ndio unaweza kuleta silsila nzuri kiutamaduni na ustaarabu na ya maisha na kuipa tafakri uhai na pumzi ya kina. Ni hapo tu, ndipo jamii inapoweza kuwaibua watu kama Mawlana Rumi, Sinan Mhandizi, Fudhuli Mshairi na mfano wao.

- Kwa sababu aya za Qur'an zilikuwa zikishuka kidogo kidogo hatua kwa hatua na hivyo kufanya kazi ya kuikariri na kuyafanyia kazi yaliyomo kuwa rahisi. Kwa kiasi kikubwa ikafanya kazi ya mafundisho ya Qur'an kuwa yenye mazingatio kwao.

- Qur'an ilikuwa ikisomwa wakati wa sala, hivyo Maswahaba waliendelea kujifunza hata ndani ya swala na kuwafanya wazidi kufungamana nayo. Suratul Fatiha ambayo ilisomwa mara kwa mara katika kila rakah katika sala iliwaathiri sana kwa sababu hii.

- Ili kuhakikisha kwamba hukumu zao na matendo yao yalikuwa sahihi na yaweze kukubalika walikuwa wakichukua mifano na visa kutoka katika Qur'an Takatifu.

Binadamu Wote Waliwastaajabia

Hiyo ndiyo *Asr-u Saadah*, Zama za Neema zilizotengenezwa na Qur'an ndani ya muda mfupi. Tangu wakati huo, ulimwengu wote umekuwa ukikitazama kizazi hicho kwa macho ya kustaajabia.

Hivi kama wanasaikolojia, wanasosholojia, waalimu waliobobea na wanaanthropolojia, wanafalsafa na wahandisi wote wa karne ya 21 wangaliunganisha nguvu zao na akili zao je, wangeliweza kutengeneza na kuibua kizazi kidogo tu cha watu katika jamii mfano wa kile cha Maswahaba?

Qur'an na Sunnah, ambavyo kwa ufanisi vilizalisha jamii bora ya *Asr-u Saadah*, bado vinaendeleza taathira na uhai wake mpaka leo hii. Jamii ambazo ziliushika Uislamu daima zilistawi, wakati zile ambazo ziliachana na Uislamu ziliangamia. Baada ya kuichunguza misingi ya Uislamu yenye haki na usawa, La Fayette (d. 1834) alilazimika kutoa heshima kwa Mtume (s.a.w) na kumstaajabia akisema:

"Ewe Mwarabu mwenye ukuu! Hata ungelipewa sifa kubwa kiasi gani, bado sifa hizo zisingetosha; kwa maana umegundua maana sahihi ya uadilifu". (Kaamil Miras, Tecrîd-i Sarîh Tercemesi, IX, 289)

Maadili ya Kiislamu Yanatekelezeka, Sio Nadharia

Lengo la Uislamu si kuweka nadharia nyepesi ya kimaadili kuhusu masuala mbalimbali ya kimaadili au kujiingiza katika falsafa ya kimaadili inayonyumbuliwa kutoka katika maisha ya kila siku na kuingia katika mijadala kwa ajili ya kuridhisha matakwa ya nafsi. Bali lengo la Uislamu ni kukabiliana na

mahitaji ya maadili ya binadamu kwa kutoa suluhu na ufumbuzi na unaotekelezeka na kuwapatia fursa wanadamu ya kuwa na ufahamu pale wanapofanya makosa ili waweze kubainisha wenyewe ipi ni haki na ipi ni batili. Uislamu unakutaka kuzihawilisha kanuni zake za kimaadili na kuzipeleka kwenye maisha, kwa njia nzuri na iliyo bora kabisa.

Uislamu haulengi tu kuwa na maadili "yanayojulikana" bali pia kuweka maadili "yanayotekelezeka." Baada ya kutoka amri ya kuamrishwa "kusoma" katika aya za mwanzo mwanzo, aya zilizofuatia ni zile zinazomuamrisha kuwakataza watu kufanya maovu; na hilo pekee linatosha kupewa nafasi ya kuatafakariwa.

Kinyume chake, ukilinganisha mawazo ya kuleta amani na utulivu katika jamii yaliyotolewa na wanafalsafa ambao kamwe hawakupitia mafunzo ya Mwenyezi Mungu yalikuwa hayaendi mbali zaidi ya waliyoyaandika katika vitabu vyao vilivyo katika rafu ya maktaba vikipata tu vumbi. Wale ambao basi walithubutu kufaidika na baadhi ya mafundisho ya wanafalsafa hawa maisha yao yalikua ni mafupi mno hivyo hawakuweza kuishi muda mrefu. Mbali na hilo, wanafalsafa hawa walishindwa kuyatekeleza yale waliyokuwa wakiyahubiri kwenye vitabu vyao wenyewe, achilia mbali kuwa na ushawishi wa kudumu kwa wengine, hivyo mawazo yao yalibaki kama nadharia daima.

Kwa mfano, ingawa Aristotle anajulikana kama mtu aliyeweka aina fulani ya kanuni za falsafa ya

kimaadili, kwa kuwa alikuwa mbali na Ufunuo wa MweyeziMungu, kamwe hatujawahi kushuhudia hata mtu mmoja ambaye ameziamini falsafa zake, akazifanyia kazi, halafu akaneemeka na falsafa hizo. Pia hata kitabu mashuhuri cha bwana Farabi kijulikanacho kama *al-Madinatu'l-Fadheelah*, ambacho maudhui yake ni kuelezea mawazo ya mji na jamii bora, kamwe hakikukupata hata fursa ya kufanyiwa kazi. Mawazo ya watu hawa ni hayakuwa mawazo yenye kutekelezeka na kutoa manufaa yanayoonekana zaidi ya kuwa makaratasi tu yaliyoshibisha matumbo ya wadudu. Kwa kifupi, si mawazo yaliyohubiriwa kivitendo; wala si mawazo yaliyokuwa yamejengwa kwenye msingi wa Ufunuo kutoka kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu.

Kwenye maandiko yao huwa wakisema "Kulingana na maoni yangu" hivi ndivyo wanavyosema wanafalsafa, lakini manabii (mitume), wao husema "kutokana na amri ya Mwenyezi Mungu."

Kwa kifupi, kwa mara nyingine Mwenyezi Mungu alionesha uwezo wake wa milele kwa kumpa Mtume ambaye hakujua kusoma maarifa makubwa kabisa ya maadili yanayotosha kwa ustawi wa viumbe wote na yenye manufaa kwa binaadamu. Akamruhusu Mtume (s.a.w) kuiweka elimu hiyo katika matendo ili kwa wale wenye macho waweze kuona dhahiri jinsi muongozo huo wa maisha unavyotekelezeka.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَشْرِي نَفْسَهُ ابْتِغَاءَ
مَرْضَاتِ اللَّهِ ۗ وَاللَّهُ رَءُوفٌ بِالْعِبَادِ

"Na katika watu yupo ambaye huiuza nafsi yake kwa kutaka radhi za Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake."
(al-Baqarah, 2: 207)

Msisimko wa Imaan katika Jamii ya Asr-u Saadah

Msisimko wa *Imaan* katika Jamii ya *Asr-u Saadah*

Maswahaba walikuwa wakijitahidi kuishi maisha yao kulingana na vile anavyoelekeza Mwenyezi Mungu na vile vile mapenzi yao ya iman. Chini ya mlengo huu kulikuwa na msaada kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Hakika, wanadamu wa zama za jahiiliya ambao hadi wakati huo walikuwa wakiishi katika lindi la uovu na maadili mabaya wakapata rehma na nusra kutoka kwa Mwenyezi Mungu kupitia kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akawaletea nuru na kuwapa Maswahaba elimu iliyowafanya kuwa kiigizo kwa watu hao ambao walikuwa wakaidi, wajinga, madhalimu na wakatili wa kutosha kuwazika binti zao wenyewe hai, wakageuka kuwa waumini wazuri mpaka saa ya mwisho ya uhai wao.

Walikimbilia Kujiunga na Safu za Uislamu

Vijana kwa wazee wa jamii ya Asr-u Saadah waliingia katika misingi bora ya Uislamu kwa wingi sana. Abdullah ibn Zubayr (r.a), alikuwa ndiye mtoto wa kwanza kuzaliwa baada ya Hijra. Nao wazazi wake baada tu ya kumzaa wakampeleka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w). Baada ya kutafuna kipande kidogo cha tende akakiweka katika kinywa cha kichanga yule na kisha kukishitua kichwa chake na kumuombea kwa Mwenyezi Mungu na kumpa jina la Abdullah.

Abdullah ibn Zubayr, (r.a) baada ya kuwa amefikisha umri wa miaka nane alitumwa na baba yake kwenda kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kutoa kiapo cha utii na mbele ya Mtume, Mtume wa Mwenyezi Mungu baada ya kumuona Abdullah akatabasamu na kukubali kiapo chake. (Muslim, Adab, 25).

Abdullah ibn Hisham (r.a) wakati wa ushindi wa Makkah alikuwa na umri wa miaka sita. Mama yake Zaynab bint Humayd (r.a) alimpeleka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kumwambia "Kubali kiapo cha mwanangu, Mtume wa Mwenyezi Mungu, kwamba yeye ni Muislamu!" "Yeye bado ni kijana mdogo sana", alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), ambapo baada ya hapo alitikisa kichwa cha kijana yule na kuomba kwa ajili yake.

Katika miaka kadhaa baadaye, Abdullah ibn Hisham (r.a) alikwenda sokoni kununua vitu vya chakula na biashara, Ibn Omar na Ibn Zubayr baada ya kumwona Abdullah ibn Hisham (r.a) mara moja walikwenda karibu naye na kumuomba awafanye washirika katika vitu hivi kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, alifanya sala na ziada ya mali kwa ajili yenu" Abdullah bila kuzingatia maombi yao. Kulikuwa na nyakati wakati akiwa wapeleke nyumbani na shehena ya ngamia kama sehemu ya faida. (Bukhari, Shirkah, 13).

Abu Kursafah, (r.a) pia aliingia katika Uislamu akiwa mdogo sana anaeleza maisha yake na uzoefu wake hapa chini: "Niliwasikia mama yangu, shangazi yangu na mimi tulikuwa tunarudi nyumbani baada ya kuwa tumeshaapa kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, nikasikia wote wawili wakisema, 'Hatujamuona kamwe mtu kama yeye katika maisha yetu yote, hatujawahi kukutana na mtu mwingine mwenye uso mzuri, nguo safi na mawaidha yenye kusisimua. "Anapozungumza ni kama vile nuru kutoka katika kinywa chake" (Haythami, VIII, 279-280).

Hawakusita Kujitolea Maisha yao kwa Ajili ya Imaan

Sumayya na mume wake Yasir - Mwenyezi Mungu awaridhie - alikuwa ni maarufu na jasiri ambao wote wawili walitoa kafara maisha yao kwa

ajili ya kulinda imani yao. Sawa na ujasiri wa Ammar ibn Yasir, Bilal Habashi, Habbab ibn Arat, Suhayb ibn Sinan, Zinnira, Amir ibn Fuhayra, Abu Fukayha, Miqdad ibn Amr, Umm Ubays, Lubayna, na Nahdiya binti yake, wote hawa walipitia wakati mgumu sana wa mateso kwa ajili tu ya kulinda na kutetea iman zao. Licha ya mateso makali mno, Maswahaba hawakuchoka kuimarisha ngome ya imani zao kuhakikisha kwamba baraka hii ya Mwenyezi Mungu inaendelezwa salama mpaka kwa vizazi vijavyo, hata kama iliwalizimu kupoteza kila kitu walichokuwanacho katika safari yao ya maisha. Wakati wa kipindi cha ukhalifa wake, Omar (r.a) siku moja alimuuliza Habbab ibn Arat (r.a) ni mateso gani alifanyiwa na kuyavumilia. "Angalia mgongo wangu", Habbab (r.a) akamwambia. Baada ya kuukagua mgongo wa Habbab ibn Arat (r.a) Omar (r.a) akasema, "Sijawahi kuona viungo vya mwili vilivyosulubiwa kikatili kama hivi katika maisha yangu!" "Habbab (r.a), akasema Washirikina walikuwa wakiwasha moto mkali sana na kunilalisha juu ya moto huo bila nguo yoyote.

Moto huo ulikuwa ukizimika pale tu mafuta yanayotoka kwenye mgongo wangu yanapodondokea". Washirikina walikuwa wakimfunga Habbab, Mwenyezi Mungu makaa yeye moto mkali mgongoni mwake mpaka nyama zikawa zinadondoka kipande kimoja baada ya kingine hata hivyo haikutosha kumfanya aseme yale aliyoambiwa aseme na makafiri (Ibn Athir, Usd'ul Ghabah, II, 114-115).

Zayd ibn Dasina na Hubayb Mwenyezi Mungu awaridhie wote wawili walikuwa ni mateka waliotekwa na makafiri walikuwa tayari kuteswa mpaka kufa dakika za mwisho za pumzi zao wakaulizwa: "Je, unataka Mtume aje akae badala yako kwa malipo ya maisha yako?" Wote wawili wakawatazama washirikina na kutamani kuwauliza swali akasema: "Achilia mbali Mtume kuwa katika nafasi yangu sasa hivi mimi na familia yangu tusingelitaka hata mwiba usimchome mguu wake aliposimama yeye!" Abu Sufiyan, aliyesimama hapo alishtushwa na ujasiri huu wa kipekee japo hakuweza kusaidia chochote akajisemea mwenyewe "Katika maisha yangu sijawahi kuona kundi jingine la watu zaidi ya Maswahaba wa Muhammad wenye upendo kwa kiongozi wao kiasi hiki." (Waqidi,360-362; Ibn Saad, II, 56).

Baada ya vita vya Uhud, Saffiya (r.a), alitaka kuona maiti ya ndugu yake Hamza (r.a), alitembea kuelekea zilipo maiti za mashahidi zilizokuwa zinatisha sana kwa jinsi zilivyokuwa zimeharibiwa na makafiri. Mwanawe Zubayr akwambia "Mtume wa Mwenyezi Mungu ameshauri wewe urudi mama yangu mpendwa!" "Kwa nini?" Alijibu. "Hivyo nisione maiti ya ndugu yangu? Mimi najua amekufa kwa njia ya Mwenyezi Mungu... na Mwenyezi Mungu atatujaalia subira na hivyo tutarajie ujira kutoka kwake!" Zubayr, (r.a) akageuka nyuma na alielezea maneno ya mama kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu "Kama ndivyo

hivyo naruhusu kumwona kaka yake", lilikuwa ndilo jibu lake.

Safiyya, (r.a) alikuwa pembeni akimuombea dua kaka yake alipewa cheo cha mfalme wa mashaahid wa vita. (Angalia, Ibn Hisham, III, 48, Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 349).

Wanawake ambao kwenye zama za Ujinga kwa habari tu waliyopokea walikuwa wakiomboleza kwa siku nyingi na kuchana nguo zao na kuvuta na nywele zao wenyewe, ghafla wakawa mhimili wa utulivu, na wenye kushukuru kwa imani yao isiyotetereka katika njia ya Mwenyezi Mungu (s.w).

Moja ya mifano mizuri ya hii ni ile ya Kabsha bint Ubayd, (r.a), Saad ibn Muadh wa (r.a).

Baada ya kupata majeraha makubwa katika vita ya Uhud, Mtume wa Mwenyezi Mungu, baraka juu yake na amani, alikuwa anarudi Madina wakiwa na farasi, na Saad ibn Muadh (r.a) akimshikia uenyekiti wake, wakati Kabsha bint Ubayd, (r.a) akawakaribia. "Mtume wa Mwenyezi Mungu huyu ni mama yangu", alisema Saad, (r.a) Alijibu Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Akimuangalia kwa karibu Mtume wa Mwenyezi Mungu katika uso wake alisema, "Naomba wazazi wangu kuwa fidia kwa ajili yako mjumbe wa Mwenyezi Mungu, taabu hazina maana yoyote kwangu, mradi nakuona u mzima wa afya sina shaka kabisa

Amr ibn Muadh, Mwenyezi Mungu baada ya kutoa salamu za pole kwa kupoteza kijana wake aliyekufa shahidi katika vita vya Uhud, Mtume wa Mwenyezi Mungu aliongeza, "Nakupa habari njema wewe pamoja na watu wa nyumba yako kila aliyekufa shahidi katika watu wa kabila lako (zaidi ya kumi na mbili) wote wataenda peponi. Wana pia wamepewa ruhusa ya maombezi kwa niaba ya familia zao!" "Sisi tumeridhika, Mtume wa Mwenyezi Mungu. Ni nani atatoa machozi juu yao baada ya sasa?" alijibu kabla kumsihi Mtume wa Mwenyezi Mungu, "Tafadhali nakuomba uwaombee wale waliopotea pia!" Hivyo Mtume wa Mwenyezi Mungu aliomba: "Mwenyezi Mungu...ziondolee nafsi zao huzuni na uwape ujira wao juu ya matatizo yao! Na kuwalinda wale ambao wameachwa nyuma katika njia bora zaidi!"

Mtume wa Mwenyezi Mungu, (s.a.w) aliendelea na safari yake. Maswahaba walimfuata Mtume kila alipokwenda. Upendo wao kwa Mtume (s.a.w) uliwafanya wachukie kwenda majumbani mwao, walipenda sana kukaa jirani na alipo kufuatia hali hiyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu, (s.a.w) alimwambia: "Kuna watu kutoka kabila lako ambao watakuwa wamejeruhiwa Siku ya Malipo, hao wote watakuwa wakitokwa na damu kwenye majeraha yao. Rangi yake itakuwa ya damu lakini harufu yake itakua ya miski. Waambie warudi nyumbani na kutibu majer-

aha yao. Hivyo basi hakuna ruhusa ya kutufuata sisi. Waambie kwamba hii ni amri!"

"Ni amri hii ya Mtume wa Mwenyezi Mungu baraka na amani yake kwamba hakuna majeruhi kutoka kabila la Banu Ashal wataandamana na sisi kutoka hereon!" Saad, (r.a) alinukuu. Wapiganaji thelathini wote waliojeruhiwa, hawakuwa na la kufanya zaidi ya kutii amri bila kutaka waliutumia usiku mzima kufunga majeraha yao karibu na moto ambao uliwaka mpaka asubuhi. (Waqidi, I, 315 -316; Diyarbakri, I, 444).

Swahaba mwingine wa kike ambaye alionyesha ujasiri wa karibu zaidi ya uwezo wa binadamu alikuwa Sumayra, (r.a). Siku ya vita vya Uhud, Madina nzima zikasambaa habari kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu, (s.a.w) amekufa shahidi. Hofu na mayowe vikatawala miongoni mwa watu wa Madina. Sumayra (r.a) licha ya kuambiwa kwamba mume wake, na watoto wawili, baba yake na ndugu zake wamekufa shahidi katika uwanja wa vita, mwanamke huyu wa kiansari alionekana kutoshtushwa na habari hizo badala yake aliendelea kudadisi habari zilizogaa kwamba kwa Mtume (s.a.w) aliendelea kuuliza: "Je, yuko salama?" Hatimaye alipata jibu alilokuwa akilitumaini kutoka kwa Maswahaba "Ndiyo. Alhamdulillah yeye yungali hai na anaendelea vizuri!" Hapo Sumayra, radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kwake

kidogo aliridhika na jibu hilo kutoka kwa Swahaba huyo.

"Naomba nimuone tafadhali ili moyo wangu upate kutulia aliwaomba kwa hisia kali. Walipomuonesha alimkimbilia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na akasema: "Naomba wazazi wangu wawe wamekufa kwa ajili yako Mtume wa Mwenyezi Mungu...nami sina wasiwasi tena kama wewe u ngali hai." (Waqidi, I, 292; Haythami, VI, 115).

Walipambana na Kufanya Hijra kwa ajili ya Kulinda Imani yao

Kwa ajili ya kulinda imani zao kutokana na ukandamizaji wa makafiri wa Makkah, Maswahaba walihamia mbali na kuacha nyuma nyumba zao, familia zao na mali. Kama ushuhuda wa nguvu zao za imani, Mwenyezi Mungu, utukufu kwake, anasema katika Qur'an:

"Hakika wale walio amini na wakahama na kutoa malalamiko yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na wale ambao aliwachukua katika na kuwasaidia-hao ndio Waumini wa kweli. Kwa wao watapata msamaha na riziki ya ukarimu." (al-Anfal, 74).

Hotuba ya Jafar Tayyar, (r.a), aliyeteuliwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kama mkuu wa mjumbe wa kwanza wa wahamiaji wa Abyssinia,

aliyoitoa mbele ya Negus, inatoa picha halisi ya jinsi watu wa Zama za Ujahiliya walivyokuwa wamebadilishwa na mfumo wa Uislamu na athari ya imani waliyobaki nayo baada ya hapo:

"Ewe Mtukufu Mtume! Sisi tulikuwa wajinga wa kutupwa kabisa, tulikuwa tunaabudu masanamu tuliyoyatengeneza wenyewe kwa mbao zetu na kufikiri wao ni miungu. Tulikuwa tunakula nyamafu (kibudu) na kuwazika binti zetu wangali hai. Tulikuwa wacheza kamari, tulikuwa tunakula. Tulikuwa wazinifu na hatukuona madhara kuona mwanamke kushiriki katika mahusiano na watu mbalimbali. Hatukujua chochote kuhusu haki za ndugu zetu wala hatukutambua haki za majirani. Wenye nguvu waliwanyonya wale dhaifu, wakati wale matajiri waliishi mbali na maskini. Hatukujua chochote sisi kuhusu khabari ya haki! Kisha Mwenyezi Mungu muweza wa yote alituonea huruma na akatupa ahueni na akamteua Mtume kati yetu, kutoka kabila la kawaida na lenye kheri ambaye alikuwa tayari anajulikana aliyetuita kwenye njia ya Mwenyezi Mungu ni yeye alitufundisha jinsi ya kumwabudu Mwenyezi Mungu (s.w).

"Alituokoa na ibada za masanamu ya miungu ya mababu zetu. Ni yeye aliutupilia mbali uovu wote kutoka kwetu. Ni yeye alipiga marufuku umwagaji damu, kula riba, kusema uongo na matumizi mabaya

ya mali kwa yatima. Daima Mtume wa Mwenyezi Mungu alitufundisha mema. Alitushauri kupenda haki, kutimiza ahadi zetu, kuwatendea wema majirani na jamaa pamoja na na kulinda heshima zetu mbele ya wanawake na binti zetu. Alituokoa kutoka katika ushenzi na kutufundisha jinsi ya wema. Hivyo sisi tulimwamini na sasa tunaishi katika njia yake. Kwa sababu hiyo sana tumeingia uadui na watu wa kabila la Maquraysh, tuliteswa sana. Mateso yalipokuwa magumu sana, na hatukuwa tayari kuondoka, dini yetu tukaomba ruhusa kwa

Mtume wetu (s.a.w), kuhamia huku katika nchi yenu na si nchi za wafalme wengine. Tukajaalia hapa ni mahala salama na hatutaonewa na hapa tutapata ulinzi wa kutosha." (Ahmad, I, 202-203, V, 290-291;. Haythami,VI, 25-27; Ibn Hisham, I, 358-359)

Jeshi la mwisho la wahamiaji wa Abyssinia walirudi, na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), wakati wa ushindi wa Khaybar. Asma bint Umays, (r.a) alikuwa mmoja kati yao. Siku moja, alimtembelea Hafsa mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu heri, (s.a.w), baba wa Hafsa, Omar, (r.a) pia alikuwa pale ndani, Omar, (r.a) alishindwa kumtambua Asma, baada ya Hafsa (r.a) kujitambulisha, Omar, (r.a) aliuliza: "Ni yule Asma kutoka Abyssinia...mmoja wa watu walioshiriki katika safari ya baharini?" "Ndiyo", alijibu Asma, (r.a). "Sisi tuliwazidi nguvu kale Hijra", hivyo

basi alisema Omar, (r.a). "Sisi tuna haki zaidi ya kuwa karibu na Mtume ya Mwenyezi Mungu!" Asma Alifadhaishwa sana na maneno yale, alijibu, "kwa ajili Mwenyezi Mungu unafanya makosa kufikiri hivyo Omar! Muda wote huu, ulikuwa pamoja na Mtume wa Mwenyezi Mungu...akakutoa ujingani na kukufundisha kuwa mtu mwema.

Lakini sisi tulikuwa katika nchi ya mbali huko Abyssinia, kati ya watu wa nje, wanaoishi uhamishoni. Na yote haya ilikuwa ni kwa ajili ya jina la Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba mimi sitakula au kunywa chochote mpaka nitakapomwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu haya uliyoniambia. Tulikuwa tunavumilia mateso, shida na vitisho vingi sana huko. Lakini nina uhakika Mtume wa Mwenyezi Mungu akipata taarifa hii utapata kujifunza na kufahamu vizuri jambo hilo. Nami nitamwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu bila ya kuongopa au kuongeza kitu chochote cha kwangu mwenyewe!" Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alipofika, Asma, (r.a) alimpa taarifa ya Omar, (r.a).

Baada ya kupokea taarifa za Omar (r.a) na kuzithibitisha, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: "Yeye hana haki zaidi na mimi kuliko wewe. Yeye na rafiki zake wana safari moja tu ya Hijra wakati nyinyi mmevuka bahari mara mbili!"

Asma (r.a) akasema: “Mara baada ya hapo, Abu Musa al-Ashari na Maswahaba wengine ndani ya meli kutoka Abyssinia likanijia katika vikundi na alikuwa akinisihi kurudia kusema maneno ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, (s.a.w). Ilikuwa kama hapakuwa na kitu kingine katika ardhi ambacho kiliwapa furaha na kuwapa matumaini zaidi.

Abu Musa al-Ashari (r.a), alikuwa akinitaka kurudia kusimulia tukio hilo tena na tena na kila nilipokuwa nasimulia habari hizo njema niliyopewa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), wahamiaji wa Abyssinia walilipokea jambo hilo kwa furaha.” (Bukhari, Maghazi, 36; Muslim, Fadail’us-Masahaba, 169).

* * *

Msisimko wa Ibada Katika Zama Za Furaha

Msisimko wa Ibada Katika Zama Za Furaha

Kwa Maswahaba wakati wa kuabudu ni wakati wa kumkurubia Allah (s.w), utukufu juu yake. Nyakati hizi zilikuwa ni nafasi muhimu na pekee kupata amani ya nafsi. Walifanya kila tendo la kuabudu kwa shauku kubwa kutokana na upendeleo wa kushushiwa amri kuu, walichukulia hilo kama sifa na baraka kwa kuzawadiwa uwezo wa kukamilisha kila tendo la kuabudu.

Walikuwa Waangalifu Kutunza Udhu Wao Wakati Wote

Waislamuu wa zama za furaha walikuwa waangalifu kuwa na udhu wakati wote na walitawadha tena kabla ya swala. Mtume alobarikiwa, (s.a.w), siku moja alimuita Bilal Habash, Allah apendezwe naye, karibu yake na akamuuliza:

"Ni tendo gani ulifanya likakuwezesha kuingia peponi kabla yangu? Kila ninapoingia peponi

kwenye ndoto zangu, huwa ninasikia mlio wa viatu vyako mbele yangu. Jana usiku niliingia tena peponi nikasikia mlio wa viatu vyako mbele yangu tena…."

"Ninahakikisha ninaswali rakaa mbili kila nisikiapo adhana, Eh Mtume wa Allah! Kila udhu unaponitoka huwa ninatawadha upya na kufikiria kwamba napaswa kutoa rakaa mbili zingine kwa Allah." alielezea Bilal (r.a).

"Kwa sababu ya rakaa hizo mbili, itakuwa." Mtume wa Allah, (s.a.w), alisema (Tirmidhi, Manaqib, 17/3689; Ahmad, V, 354).

Abu Ghutayf al-Huzali anaelezea:

"Nilimsikiliza Abdullah bin Omar alipozungumza na sisi masjid tukiwa tumekaa sakafuni. Ulipofika wakati wa swala ya **zuhr**, alinyanyuka, akachukua udhu na akaswali. Hata wakati wa swala ya **asr** ilipofika alinyanyuka tena, akatia udhu tena achilia mbali ule aliotia mwanzo na akaswali. Ikifika wakati wa swala ya **maghrib** anatia udhu upya na kuendelea na swala hiyo. Baada ya hapo anarudi katika mahala pake.

"Allah akuongoze uwe kati ya waadilifu." Nikamwambia. "Je, ni faradhi ama sunnah kutia udhu upya kwa kila swala?"

"Ulikua ukinitazama wakati wote huu? Aliuliza.

"Ndiyo" Nikajibu.

"Hapana, si faradhi." Halafu akaelezea. "Nilivyotia udhu kwa ajili ya swala ya *alfajir*, ingeweza kuswali swala zote zilizofatia na udhu ule ule niliotia alfajir, ikiwa kwamba sijauvunja udhu ule, kama isingalikuwa kwa maneno haya niliyoyasikia kutoka kwa Mtume wa Allah (s.a.w):

"Yeyote yule mwenye kutia udhu juu ya udhu mwingine anapata thawabu kumi."

"Na hizo ndizo thawabu ninazozitaka." Alisema (Ibn Majah, Taharat, 73).

Maswahaba waliutendea haki udhu wao, walichukua udhu kwa umakini mkubwa. Abu Hazim wa zama za Tabiun mara moja alimuona Abu Hurayrah Allah apendezwe naye, akiosha mikono yake mpaka kwapani wakati wa kutia udhu.

"Ni aina gani ya udhu hiyo Abu Hurayrah?" Aaliuliza.

"Ulikua hapa? Nisingetia udhu hivyo kama ningalijua ulikuwa hapa. Nilimsikia Mtume wa Allah (s.a.w), siku moja akisema "Mwanga wa mwenye kuamini siku ya kiama utamulika mpaka sehemu ya juu kabisa iliyofikiwa na maji ya udhu." (Muslim, Taharah, 40).

Mtume wa Allah (s.a.w), siku moja alienda makaburini na akasema; "Salamu kwenu, wakazi wa ardhi ya walioamini, inshaallah siku moja tutaungana! Natamani ningaliwaona kaka zangu!"

"Sisi sio kaka zako?" Hapo hapo walistaajabu Maswahaba.

"Ninyi ni Maswahaba.", alijibu Mtume wa Allah (s.a.w). "Ndugu zetu, ni wale ambao hawajazaliwa katika dunia hii."

"Utawatambua vipi, Mtume wa Allah (s.a.w) ?" Wakauliza.

"Fikiria mtu ambaye ana farasi mwenye paji la uso jeupe na kwato. Je atashindwa kumtambua farasi wake kwenye kundi la farasi weusi tii?"

"Bila shaka ataweza."

Mtume Mtukufu (s.a.w), akasema, "pale...(siku ya kiama) ndugu zenu watakuja nyuso, mikono na miguu iking'aa mwanga wa udhu. Nitafika kwenye kilindi cha mto nitawasubiri hapo kuwapongeza. Kuweni waangalifu! Wapo baadhi ya watu watafukuzwa kwenye kilindi cha mto kama ambavyo ngamia mgeni anavofukuzwa kwenye kundi la ngamia. Nitawaita. Ila nitaambiwa, "walibadilisha nyendo zao baada ya wewe!"

Hapo nitasema, "Basi waache wakae mbali, mbali!" (Muslim, Taharah, 39; Fadail, 26; Nasai, Taharah, 110/150; Ibn Majah, Zuhd, 36; Muwattaa, Taharah, 28; Ahmad, II, 300, 408)

Swala Ilikuwa Nuru ya Macho yao

Waumini wa *Asr-u Saadah* walikuwa wakiswali kwa khushui na unyenyekevu kwa Allah, utukufu kwake. Walikuwa wakiswali kwa muda mrefu tena kwa umakini mkubwa kama vile ni swala yao ya mwisho katika maisha yao.

Saad ibn Abi Waqqas Allah apendezwe naye, anasimulia;

"Kulikuwa na ndugu wawili. Mmoja alikufa siku arobaini kabla ya mwenzake. Watu wakaanza kuzungumza maadili ya yule aliyokufa kabla ya mwenzake, mbele ya Mtume wa Allah (s.a.w).

"Huyo kaka mwingine hakuwa Muislamu, pia?" aliuliza Mtume wa allah (s.a.w)

"Ndiyo. Mtume wa Allah. Alikuwa Muislamu," wakajibu. Mtume wa Allah (s.a.w) akasema;

"Utajua vipi cheo alichopewa kwa swala zake? Swala ni kama mto mtamu na mzuri sana mbele ya mlango wa mtu, ambamo huoga mara tano kwa siku. Mnaonaje…hapo mtu huyo atabakiwa na uchafu wa

aina yoyote ile? Huwezi fikiria ni kiasi gani swala zinanyanyua cheo cha mtu! (Muwattaa, Qasr'us-Salat, 91)

Abu Talha Allah apendezwe naye, siku moja alikuwa anaswali chini ya kivuli bustanini mwake. Ndege anayejulikana kama *dubsi* akawa anapiga mabawa zake akitafuta njia ya kutokea pale bustanini. Abu Talha akachotwa na uzuri wa tukio lile na kwa muda akawa akimtazama yule ndege. Akaamua kurudi kwenye swala yake ila akashindwa kukumbuka alishia wapi kwenye kuswali. "Mali yangu imeniingiza matatani, nimepoteza umakini kwenye swala yangu" aliwaza, akimaanisha bustani, akielekea kwa Mtume wa Allah (s.a.w). Alipofika akamueleza yaliyotokea na akasema;

"Kwa hivyo, naitoa sadaka bustani kwa ajili ya Allah. Unaweza itumia vile vyovyote upendavyo, Mtume wa Allah, na umpatie yeyote yule anayestahiki." (Muwattaa, Salat, 69)

Kipindi akiwa khalifa, Omar (r.a), aliandika haya kwa magavana wake;

"Kwa ufahamu wangu, jukumu muhimu ni swala. Kwa yeyote atakayeswali vizuri, akachunga muda na kuifanya swala yake kwa umakini, atakuwa ameilinda dini yake ya islam. Kwa yeyote atakayepuuzia swala atapuuzia maamrisho mengine ya dini zaidi." (Muwattaa, Wuqut'us-Salat, 6).

Ifuatayo imetoka kwa Miswar ibn Mahramah Allah apendezwe naye-:

Nilimtembelea Omar ibn Khattab (r.a), baada ya kuchomwa kisu. Walikuwa wamemfunika blanketi akiwa hana fahamu.

"Anaendeleaje?" niliwauliza waliokuwa wakimuhudumia.

"Kama umuonavyo" wakasema.

"Muite akaswali", nikatoa wazo, "Hakuna kinachoweza kumuogopesha mpaka akaamka zaidi ya kumuita kwa ajili ya swala!"

Hivyo wakatangaza, "Khalifa…muda wa swala sasa!"

Omar (r.a), hapo hapo alinyanyuka kitandani pake, akisema: "Ni kweli...na kwa amri yake Allah yeyote atakayepuuzia swala si Muislamu" (Haythami, I, 295. Pia tazama, Muwattaa, Taharat, 51; Ibn Saad, III, 35).

Ali (r.a), naye pia alisema kwa makamanda wake, "Kila kitu kinategemea swala zako!"

Alaa ibn Abdurrahman anasimulia tukio hili:

"Ilikuwa mchana mmoja tukiwa tumeenda kumtembelea Anas ibn malik. Tulipofika Anas alinyanyuka kuswali swala ya asr. Tukamwambia mbona amewahi swala ya asr. Akiwa anaelezea sababu ya yeye kufanya hivyo alisema:

"Niliwahi kumsikia Mtume wa Allah (s.a.w), akisema hiyo ni swala ya wanafiki! Hiyo ni swala ya wanafiki! Hiyo ni swala ya wanafiki! (... Swala ya wale wanaobeba alama ya unafiki kwenye mioyo yao). Wanakaa wanakaa mpaka jua linapobadilika rangi ya njano na kuanza kuzama na kuchukua nafasi yake katikati ya pembe mbili za shetani, hapo huinama na kunyanyuka mara nne, kama vile ndege anaokota nafaka, na ni kidogo sana wakimkumbuka Allah kwenye swala zao." (Muwattaa, Qur'an, 46; Muslim, Masajid, 195)

Kwa matokeo ya maonyo yake Mtume wa Allah (s.a.w), Maswahaba walikuwa makini na walifanya kwa bidii kila tendo kwenye swala zao. Siku moja, Huzayfa (r.a), siku moja alimuona mtu akiswali bila kufata taratibu zilizo sawa za rukuu na sijida. Baada ya hapo Huzayfa (r.a), akamuuliza, "Ni kwa muda gani umekuwa ukiswali hivyo?"

"Miaka arobaini", yule mtu akajibu.

"Kwa hIvyo, inamaanisha kwamba hukuwa unaswali miaka yote hiyo arobaini. Ukifa na ilihali unaswali kama hivi unavyoswali, basi utakuwa kama umati uliomtangulia kabla ya Mtume wa Allah (s.a.w)." Akaendelea kwa kumuonyesha njia sahihi ya kuswali, akiongeza:

"Mtu anaweza kusamehewa kwa kuswali swala nyepesi kwa kufanya kwa usahihi rukuu zake na sijida zake!" (Ahmad, V, 384; Bukhari, Adhan, 119, 132; Salat, 26)

Hawakujitenga na Jamaa

Sifa bainifu muhimu ya jamii ya *Asr-u Saadah* ilikuwa ni kuondolewa kwa ukabila badala yake undugu wa dini na kutengeneza Jamii yenye nguvu na umoja. Na hali hii iliweza kuonekana kwenye swala za *jamaah*.

Akiwa Imam mwenye uzoefu katika swala za jamaah, Mtume wa Allah (s.a.w), aliweza kufahamu moja kwa moja kama kuna mtu hakuhudhuria kwenye jamaa. Angeuliza, "Fulani na fulani wamekuja kwenye swala leo?" "Rafiki yako yuwapi?" na ikiwa kama muhusika hakuja kwa kuwa ni mgonjwa. Alikwenda pamoja na Maswahaba kumtembelea. Kama huyo mtu angekuwa na matatizo basi angemtafuta kujua tatizo ama angemtumia mtu wa karibu wa muhusika.

Katika kuhamasisha Waislamuu kuswali jamaa, Mtume wa Allah (s.a.w) alikuwa akisema:

"Kama ukimuona mtu mwenye tabia ya kwenda masjid, basi shuhudia kwa imani yake, maana Allah amesema:

"Pekee atakayeingia msikitini ni yule mwenye kuamini uwepo wa Allah... (At-Tawba, 18)" (Ibn Majah, Masajid, 19).

Kwa hiyo mfululizo wa jamaah ni ishara ya imani, inaufanya msikiti uwe hai.

Abdullah ibn Masud (r.a), anasema:

"Allah shahidi, sijawahi kumuona mmoja kati yetu akitega jamaah, kasoro wale waliofahamika kuwa wanafiki. Ninaahidi Allah shahidi mgonjwa alikuwa akiletwa msikitini ilhali akiburuza miguu yake na wanaume wawili wakiwa wamemshika kila ubavu na alipangwa kwenye safu." (Muslim, Masajid, 256-257)

Kulikuwa na Waislamuu wawili kipindi cha Mtume wa Allah (s.a.w), mmoja kati yao alikuwa mfanya biashara na mwingine alikuwa mhunzi wa vyuma kazi yake kuu ilikuwa kutengeneza mapanga. Na alipokuwa akisikia adhana yule mfanaya biashara alikuwa akiweka mizani chini na kukimbilia msikitini kwa ajili ya swala.

Ndivyo ilivyokuwa kwa mhunzi vyuma pia aliacha nyundo zake hata kama ilikuwa azibonde panga zake muda ule, saa hiyo hiyo alienda msikitini. Katika kuwasifu wao na Waislamuu wengine pia, Allah alishusha haya:

"Wanaume ambao hawashughulishwi na biashara wala maslahi kuwatoa katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na kusimamisha swala na kutoa zakat wakiogopa siku ambayo zitabadilika (siku hiyo) nyoyo na macho." (an-Nur, 37) (Qurtubi, XII, 184).

Akiwa kwenye mnada Ibn Masud (r.a), siku moja aliona kundi la watu wakikimbilia msikitini waliposikia adhana. Akasema: Hawa ndiyo watu waliosifiwa na Allah kwenye *an-Nur* (aya iliyotajwa) (Haythami, VII, 83).

Walitoa Zaka na Sadaka Hali ya kuwa ni Wenye Furaha

Jamii ya Asr-u Saadah walikuwa wakiweka umuhimu sana kwenye sadaka na zaka, kama ambavyo Allah amekuwa akisisitiza sadaka pamoja na swala mara nyingi kwenye Qur'an. Walitoa sadaka na misaada kwa shauku kubwa kama vile wanatoa kwa Allah mwenyewe.

Akiwa na haraka ya kutenda jambo jema Abbas (r.a), Mtume wa Allah (s.a.w), mjomba wake, siku aliuliza kama anaweza kutoa sadaka kabala ya mwaka uliotakikana haujafika. Mtume wa Allah (s.a.w), alimruhusu. (Abu Dawud, Zakat, 22/1624; Tirmidhi, Zakat, 37/678; Ibn Majah, Zakat, 7; Ahmad, I, 104; Darimi, Zakat, 12).

Mwanamke, ambaye alikuwa ndugu yake na Mtume wa Allah (s.a.w), siku alimtembelea akiwa na mtoto wake wa kike pembeni yake. Yule mtoto wa kike alikuwa amevaa bangili nzito mikononi mwake.

"Huwa unazitolea sadaka?" Mtume wa Allah (s.a.w), akamuuliza yule mwanamke, akimaanisha zile bangili.

"Hapana", akajibu.

"Ungependa kama Allah angekufanya uvae bangili mbili za moto mbadala wake?" Mtume (s.a.w) akauliza.

Yule mwanamke akamvua mtoto wake akampatia Mtume zile bangili na kusema; "Hizi sasa ni mali ya Allah na Mtume wake. Fanya vile ikupendezavyo." (Abu Dawud, Zakat, 4/1563)

Ujumbe wa watu kumi na tatu wa kabila la Banu Tujib walifika karibu na Mtume wa Allah (s.a.w), wakiwa na sadaka kwa ajili ya kutoa. Mtume (s.a.w), alikuwa anapenda sana wanaopenda kutoa sadaka na baada ya kuwakaribisha kwa bashasha, akamwambia Bilal Habash (r.a), kuwakaribisha kwa ukarimu zaidi.

"Tumeleta kwako, Mtume wa Allah. Kile ambacho halali yake Allah katika utajiri wetu!" wakasema.

"Zichukueni mrudi nazo kwenye mji wenu mkazigawanye kwa maskini wa huko." Akasema Mtume wa Allah (s.a.w).

"Lakini tulichokileta ni kilichobaki baada ya kuwapatia maskini wa kule kwetu." Wakajieleza.

Abu Bakr (r.a), akawasifu na kusema, “Ama kwa hakika hakuna ujumbe wa waarabu kama hawa wanaume wa Tujib, ewe Mtume wa Allah!”

“Mwongozo upo mikononi mwa Allah” akasema Mtume wa Allah (s.a.w), “Allah anafungua imani kwa wenye mioyo inayotamani kuwa bora.”

Ujumbe wa Banu Tajib ulimuuliza Mtume wa Allah (s.a.w), baadhi ya maswali kuhusu Qur’an na Sunnah. Majibu yao waliandikiwa na wakapewa. Shauku yao iliongeza kutaka kuwasikiliza zaidi kwa Mtume rehma na amani ziwe juu yake. Baada ya kukaa muda mrefu, ule Ujumbe ukaelezea hisia zao za kutaka kwenda kwao. Na walipoulizwa kwa nini haraka hivyo, wakasema:

“Tunataka kurudi kwa watu wetu haraka iwezekanavyo ili tuweze kwenda kuwaeleza yale yote tumejifunza kutoka kwa Mtume wa allah!” Wakamuona Mtume wa Allah (s.a.w), kwa mara ya mwisho wakamuaga. Mtume (s.a.w), akamuagiza Bilal Habash (r.a), aende nao na akawapatia zawadi nyingi sana kuliko wajumbe wengine wowote waliowahi kufika. (Ibn Saad, I, 323; Ibn Qayyim, III, 650-651).

Ibn Abbas (r.a), anahadithia:

“Mtume wa Allah (s.a.w), aliongoza swala ya rakaa mbili siku ya eid. Baada ya kutoa hotuba kwa wanaume, alisogea kidogo upande wa wanawake kwa

kuwa hawakuwa wanamsikia vizuri. Pamoja naye alikuwepo Bilal (r.a), akawahubiria pia, akiwasisitizia wawe wanatoa misaada. Baada ya hapo, wanawake wakaanza kurusha bangili, dhahabu, silva na pete zao kwa Bilal aliyekuwa ametandaza shati." (Tazama, Bukhari, Zakat, 21, 33)

Akivuta umakini wa watu juu ya kupuuzia kutoa sadaka huwa inakuwa majuto baadae, Ibn Abbas (r.a), alikuwa anawaonya watu kwa maneno haya:

"Kwa yeyote asiyeenda hijja ama kutoa sadaka hali ya kuwa ana uwezo wa kifedha kufanya hivyo, atatamani kurudi duniani siku yake ya pumzi ya mwisho." Ataisoma aya ifuatayo;

"Enyi mlioamini! yasiwapumbaze mali zenu wala watoto wenu katika kumkumbuka Mwenyezi Mungu na atakayefanya hivyo basi hao ndio watakaopata hasara kwa (kwa kuuza kile kilichokuwa kikubwa na cha kubaki kwa kukimbilia chenye kudharaulika na kuisha), na toeni katika tulivokupeni kabla hayajamfikia mmoja wenu umauti akaja kusema ee h mola laiti kama ungenipumzisha kwanza mpaka muda wa karibu nikaweza kutoa zakat na nikawa miongoni mwa watu wema na Mwenyezi Mungu hatoichelewesha nafsi pale muda wake unapokuwa umefika, na Mwenyezi Mungu anayo taarifa ya yote mnayoyafanya." (al Munafiqun, 9-11) (Tirmidhi, Tafsir, 63/3316)

Watu wa zama za furaha walikuwa waangalifu na kiwango cha mali walizokuwa nazo na zingine kuwapatia walio masikini.

Ahnaf ibn Qays (r.a), siku moja alikwenda karibu na Khalifa Omar (r.a), akiwa kiongozi wa wajumbe toka Iraq. Ilikuwa ni siku ya joto sana. Akiwa amevaa kimori Omar (r.a), alikuwa anampaka mafuta ngamia aliyekuwa anaandaliwa kwa ajili ya sadaka. Alivyowaona alisema:

"Badilisha nguo zako Ahnaf…na uje kunisaidia, huyu ni ngamia wa zakat. Masikini, wajane na mayatima ni halali yao."

Mmoja wao akasema: "Allah akujaze rehma, khalifa! Umeshindwa kumpatia kazi hiyo mmoja wa watumwa wako?"

Kwa hilo, Omar (r.a), alitoa jibu zuri lifuatalo:

"Nani mtumwa bora zaidi ya Ahnaf na Omar? Tangu hapo mimi nimebeba majukumu ya Waislamuu wote mabegani mwangu, mimi ni mtumwa wa Waislamuu wote! Kama ilivyo muhimu kwa mtumwa kuwa mtiifu mbele ya bwana wake na kukamilisha majukumu yote, nami pia nitafanya hivyo kwa Waislamuu wote." (Ali al-Muttaqi, V, 761/14307).

Kuna taarifa pia omar Allh amrehemu, alimkimbiza ngamia wa zakat aliyetoroka mpaka akaishiwa

na pumzi na aliwajibu vivyo hivyo waliomshauri awaambie watumwa wake wakimbize badala ya yeye.

Ishara ya hisia walizoonyesha Waislamuu kuhusu sadaka ni kesi ya Khalifa Omar ibn Abdulaziz. Maofisa wa sadaka aliowaagiza kwenda Afrika, walirudi bila kutoa sadaka yoyote ile Afrika, kwa sababu nyepesi ya kwamba hakumkuta aliyekuwa na shida. Khalifa alitumia sadaka ile kuwakomboa watumwa wengi tu kutoka utumwani.

Kujitolea ilikuwa Kiini cha Maisha yao

Jamii ya Asr U Saadah ilijua kujitolea kwa ajili ya Allah, utukufu juu yake, utamlinda mwanadamu na majanga na matatizo, vile vile kujenga mapenzi ya Allah. Hata hivyo Qur'an imesema:

"Na toeni katika njia ya Mwenyezi Mungu na msijipileke wenyewe katika maangamizi na mfanye mazuri, hakika Mwenyezi Mungu anawependa wenye kufanya mema." (Al-Baqara, 195).

Umm Bujayd (r.a), Swahaba wa kike kuna siku alienda kwa Mtume (s.a.w), akilalama;

"Rehma za Allah ziwe juu yako, Mtume wa Allah. Mara kibao, wenye shida wamekuwa wakija mlangoni kwangu wakihitaji msaada nami sina cha kuwapa!"

"Hata kama ukikosa kila kitu iwe hata ukucha ulioungua wa kondoo" alisema Mtume wa Allah (s.a.w), "Mpatie masikini na usimuache aondoke bila chochote." (Abu Dawud, Zakat, 33/1667; Tirmidhi, Zakat, 29/665; Nasai, Zakat, 70/2566; Ahmad, VI, 383)

Hata kama Muislamu hana chochote cha kutoa, azungumze maneno walau machache ya kumfariji. Katika hali kama hiyo, Allah ameshauri tuseme maneno amabayo yataleta amani na faraja.

Katika kusisitizia wingi wa kutoa, Abu Masud Alllah amrehemu, anasema;

"Baada ya Mtume wa Allah (s.a.w) alipotuamrisha kutoa msaada, baadhi wakaanza kwenda gulioni kubeba mizigo ili walipwe *mudd* ambayo baadae wanatoa kama sadaka. Baadhi yao leo hii wana mamia-maelfu ya dinari." (Bukhari, Zakat, 10).

"Kila mtu atakingwa na sadaka aliyotoa mpaka siku ya kiama," anasema Mtume wa Allah (s.a.w).

Abu'l Khayr, mmoja kati ya waliosambaza *hadith*, alikuwa anahakikisha anachangia chochote kila siku, hata kama ikiwa ni mkate, kitunguu ama vitu vingine vidogo vidogo kama hivyo. (Ahmad, IV, 147-8; Haythami, III, 110)

Omar (r.a), anasimulia:

"Mtume wa Allah (s.a.w), ametuamrisha tuchangie. Nilimiliki mali nyingi tu kipindi hicho. Kama upo wakati wa kumpiku Abu Bakr', 'basi ni leo' nikajisemea. Kwa hiyo nikabeba nusu ya mali zangu zote nikampatia Mtume wa Allah (s.a.w)."

"Umeibakishia nini familia yako?" aliuliza Mtume (s.a.w).

"Kiasi hichi nilicholeta hapa ndicho nilichobakisha nyumbani," nikajibu.

Hapo hapo Abu Bakr' (r.a), akatokea akiwa ameleta utajiri wake wote.

"Umebakisha nini kwa ajili ya mke wako na watoto?" Aliuliza Mtume wa Allah (s.a.w).

"Nimembakisha Allah na Mtume wake," akajibu.

"Basi pale pale nikaamini ama kwa hakika siwezi kumshinda kwa lolote!" (Tirmidhi, Manaqib, 16/3675)

Kwa mujibu wa Abdurrahman ibn Abu Amra, usiku mmoja mama yake alisema atawaweka huru watumwa ifikapo asubuhi, na ikawa amekufa usiku ule ule. Kwa hiyo baadae akaenda kwa Qasim ibn Muhammad, akiuliza kama ni sawa yeye akiwaachia huru wale watumwa kwa niaba ya mama yake.

Qasim alisema, "Saad ibn Ubadah Allah akurehemu, kuna siku aliuliza Mtume wa Allah (s.a.w), kama mama yake aliyekufa anaweza kunufaika Kama aki-

wapa uhuru wao watumwa kwa niaba yake. "Ndiyo," lilikuwa jibu lake (Tirmidhi, Manaqib, 16/3675)

Aisha (r.a), anataarifu kwamba kuna siku mwanamume alikuja kwa Mtume (s.a.w), akasema, "mama yangu amekufa ghafla. Nina uhakika kama angezungumza ama kwa hakika angetoa sadaka. Ninaweza kutoa sadaka kwa niaba yake?"

"Ndiyo" alihakikisha Mtume (s.a.w). "Toa sadaka kwa niaba yake." (Bukhari, Wasaya, 19; Abu Dawud, Wasaya, 15/2881)

Harithah ibn Numan (r.a), Swahaba, alipatwa na upofu. Alikuwa na kamba mkononi mwake iliyofungwa kwenye mlango wake na pembeni alikaa na kapu la tende na vitu vingine. Wakati wowote ambao mwenye shida angepita na kumsalimia basi alibeba kilichokuwepo kwenye kapu na kuishikilia ile kamba mpaka alipofika mlangoni na kumpatia mwenye shida. Mara kwa mara familia yake ilikuwa ikimwambia; "Hakuna haja ya wewe kufanya hivyo… Tunaweza kutoa kwa niaba yako" lakini aliwajibu hivi kila mara:

"Nilimsikia Mtume wa Allah (s.a.w), akisema, kuwapatia wenye shida kwa mikono yako mwenyewe itakulinda na kifo kibaya!" (Ibn Saad, III, 488; Tabarani, Kabir, III, 229, 231; Haythami, III, 112)

Aisha (r.a), anaeleza Mtume wa Allah (s.a.w), siku moja aliwaambia wake zake, "Atakayewahi kuungana na mimi ni yule mwenye mikono mirefu." Tukaanza sasa kujipimisha mikono yetu kuona nani mwenye mikono mirefu. Lakini kumbe maana ya "Mikono mirefu" ni mikono inayotoa zaidi sadaka... naye alikuwa Zaynab (r.a), ambaye alifanya kazi na kusaidia kwa mikono yake." (Muslim, Fadailu's- Sahabah, 101).

Tajiri au masikini, mwenye afya ama mgonjwa wote walikuwa wakishindana katika kutoa sadaka.

Siku moja mtu maskini alikwenda kwa Omar (r.a), akilalamika, "Ninyi matajiri ndio wenye thawabu nyingi kwa kuwa mnatumia utajiri wenu kuwaweka huru watumwa, kwenda hijja na kutoa sadaka!"

"Ni kweli unatuonea wivu?" aliuliza Othman (r.a).

'Ndiyo." alijibu mtu yule masikini. "Allah shahidi ni kweli."

"Ninaahidi shahidi Allah." Othman (r.a), akaanza kuelezea: "Dhirham moja inayotolewa kwa shida ni zaidi ya dhirham elfu kumi inayotolewa na tajiri!" (Bayhaki, Shuab, III, 251; Ali al-Muttaqi, VI, 612/17098)

Waligundua kuwa Hakuna Zaidi ya Funga

"Nishauri tendo." Abu Umamah (r.a), siku moja alimuuliza Mtume wa Allah (s.a.w), "Ambalo Allah atanipa thawabu kwa ajili ya tendo hilo."

"Ninakushauri funga, kwa kuwa hakuna zaidi yake." Mjumbe wa Allah (s.a.w) akajibu. (Nasai, Siyam, 43).

Umm Ayman (r.a), alianza hijira yake kwa ajili ya Allah na Mtume wake. Alifunga. Akawa hana chakula wala maji, wala mnyama wa kupanda kama usafiri. Taratibu akitembea kwenye joto kali la jangwa la Tihama, ilikuwa bado kidogo afe kutokana na kiu na njaa. Karibu na muda wa kufuturu akiwa amejilaza ilihali amechoka, alisikia sauti juu ya kichwa chake. Aliponyanyua kichwa chake, aliona ndoo ya maji ikining'inia kwenye kamba.

Anasema: "Alichukua ile ndoo na kuanza kuyanywa yale maji mpaka moyo wake ukasuuzika. Sijawahi kusikia kiu kamwe baada ya hapo."

Kulikuwa na kipindi baada ya tukio lile Umm Ayman (r.a), alikuwa akifunga makusudi kwenye joto kali na kuizunguka kaaba, ili aone tu kama angeshikwa na kiu. Lakini hajawahi kamwe mpaka siku alipokufa. (Abdurrazzaq, Musannaf, IV, 309; Abu Nuaym, Hilya, II, 67; Ibn Hajar, Isabah, VIII, 170; Ibn Saad, VIII, 224)

Kabla ya kwenda kwenye vita ya Uhud, Hamza (r.a), aliweka nia ya kufunga. "Kama nikifa kifo cha kishahidi," akawaza, "Nitakutana na mola wangu nikiwa nimefunga."

Anas ibn Malik (r.a), anaelezea;

"Wakati Mtume wa Allah rehma na amani zimshukie yeye, akiwa hai, baba yangu wa kufikia AbuTalha (r.a), hakuwa mfungaji sana, ukiachana na funga ya lazima ya mwezi wa Ramadhan, ili aweze kupigana vizuri vitani. Lakini baada ya Mtume wa Allah rehma na amani zimshukie yeye, kufa, sijawahi kumuona akiwa hajafunga labda siku za *eid* pekee." (Bukhari, Jihad, 29)

Abu Talha (r.a), alikuwa mmoja kati ya wapiganaji majasiri vitani. Hakuwa anafunga mara nyingi kwa kuwa alitaka kupigana akiwa na nguvu. Lakini baadae maishani mwake wakati vita vimepungua, alitumia muda wake mwingi kwenye funga. Inaripotiwa kwamba alikaa miaka ishirini na nne katika hali hii hata baada ya kufa kwa Mtume wa Allah rehma na amani zimshukie yeye.

Kama ilivyosimuliwa na Anas (r.a), katika siku za mwisho za uhai wa Abu Talha (r.a), alikuwa akisoma sana ayah hii;

"Nenda mbele mwepesi na mzito, shughulika sana kufata maamrisho ya Allah kwa kutumia mali

zako na watu uliokuwa nao; hili ni jambo jema kwako, kama unatambua." (at-Tawba, 41.)

Baada ya hapo alisema;

"Allah Mtukufu, tuamrishe twende vitani wakubwa kwa wadogo. Nileteeni silaha zangu."

"Tutapigana badala yako, baba" walimjibu watoto zake. Lakin Abu Talha (r.a), hakutaka kusikia. Kwa hiyo wakaandaa silaha zake na Abu Talha (r.a), akaenda kwenye kampeni. Na katika kampeni hii ndiko alikovuta pumzi yake ya mwisho. Hata walipokuja kumzika siku saba mbele mwili wake haukuwa umeaanza kuharibika wala haukutoa harufu." (Ibn Hajar, Fath'ul-Bari, [Jihad, 29]).

Abu Burdah (r.a) na Yazid ibn Abi Kabshah siku moja walienda kwenye safari pamoja. Akijichunga kufunga siku nyingi iwezekanavyo, Yazid (r.a), alikuwa amefunga wakati huu pia. *Abu Burdak akamwambia:*

"Niliwahi kumsikia baba yangu Abu Mussa akisema mara nyingi aliwahi kumsikia Mtume wa Allah (s.a.w), akisema "Kwa yeyote anayeumwa ama yuko safarini anapata thawabu ya maombi yake ya ziada aliyoyafanya kipindi akiwa na afya ama amepumzika." (Bukhari, Jihad, 134).

Zama za furaha, mwezi wa Ramadhani ulipokelewa kwa shauku na Waislamuu waliwahamasisha

mpaka watoto zao. Omar (r.a), siku moja alikutana na mlevi ndani ya mwezi huo wa Ramadhani na akaanza kumsema, "Unahuzunisha…maana hata watoto wetu wamefunga kipindi hichi." (Bukhari, Sawm, 47)

Abu'd-Darda (r.a), alielezea umuhimu wa funga, tofauti na matendo mengine, kwa maneno yafuatayo;

"Kama isingalikuwa kwa vitu vitatu, nisingependelea kuendelea kuishi duniani, nikimsujudia Muumba, mchana na usiku, kwa kuweka paji langu la uso sakafuni na kujiandaa na maisha yangu baada ya kifo, kwa kukivumilia kiu na kufunga mchana wa joto kali, kukaa na watu wenye kuchagua maneno mazuri ya kuzungumza, kama ambavyo mtu anachagua matunda mazuri kwa kula." (Munawi, Fayz'ul-adir, II, 11/1193).

Walizipokea Kwa Shauku Hijja Na Umrah

Maswahaba walikuwa wanaweka umuhimu sana kwenye hijja. Walikuwa wakiizunguka Ka'aba kwa moyo, bila kuacha matendo haya. Waliyajaza mapafu yao kwa hewa safi ya mahala pale, wakipata shibe toka Madina na Makkah. Wakifata njia iliyoachwa na Mitume yote toka Adam –amani iwe juu yake, na mioyo yao iliyojaa upendo, wakizijaza nafsi zao na kumbukumbu zao. Wakionyesha heshima kubwa juu ya alama za utakatifu wa Allah, walitumia kila nafasi wakiwa hijja katika kumkumbuka Allah.

Bara ibn Marur, (r.a), mmoja kati ya wawakilishi kumi na mbili waliochukua Kiapo cha Kwanza cha Aqabah, aliahidi kwa kipindi kile, kwenda kumtembelea Mtume rehma na amani zimshukie yeye, pamoja na al ka'aba, katika hijja inayofata. Lakini kabla hajatimiza ahadi yake, alijikuta katika kitanda cha umauti. Hivyo basi, akaiomba familia yake imuelekezee upande ambao ka'aba ipo, kwa kuwa nilimuahidi Mtume wa Allah kwamba nitakwenda!"

Hivyo ndivyo alivyopatikana kuwa mtu wa kwanza kabisa kuelekea mahali ambapo baadae panakuja kuwa Qibla, wakati wa uhai wake na kifo chake.

Alipofika Madina, akiwa na baadhi ya Maswahaba wake Mtume wa Allah (s.a.w), alitembelea kaburi la Bara (r.a) na kusoma dua ya maiti. Baada ya hapo akasema;

"Allah…msamehe, mrehemu na upendezwe naye!" (Ibn Abdilbar, I, 153; Ibn Saad, III, 619-620)

Aisha (r.a), anasimulia;

"Niliwahi kumuuliza Mtume wa Allah kama sisi wanawake tunaweza kujiunga kwenye vita na tukafanya jihad. Lakini akasema, "Jihad ya kupendeza kwenu ni hija iliyokubalika." Tangu niliposikia haya toka , sijawahi kupuuzia kamwe." (Bukhari, Jaza'us- Sayd, 26)

Omar (r.a) aliwahi kumuuliza Mtume wa allah –rehma na amani ziwe juu yako- ruhusa ya kufanya *umrah*. "kaka yangu mpendwa", akasema, "usitusahau kwenye dua zako!"

"Maneno hayo ya Mtume wa allah" Omar (r.a) alizungumzia maneno yale: "yana thamani kwangu zaidi ya dunia nzima. Nisingekuwa na furaha zaidi ya hapo hata kama ningepewa dunia nzima." (Taz, Abu Dawud, Witr, 23/1498; Tirmidhi, Daawat, 109/3562; Ibn Majah, Manasiq, 5)

Maswahaba hawakukatishwa tamaa na ugumu wa hija na umrah. Aisha (r.a), hakuweza kufanya umrah kutokana na hedhi, alilalamika kwa Mtume (s.a.w) akisema:

"Wengine, Mtume wa allah, wanarudi wakiwa wamefanya hijja na umrah wakati mimi nimefanya hija tu."

"Subiri kwanza," alijibu Mtume wa Allah (s.a.w). "Ukishamaliza hedhi, nenda Tanim (Na kaka yako Abdurrahman), ingia *ihram* na nia ya *umrah* na uanze kusema *talbiyah*. Ukishakamilisha *umrah* yako, utufate mahala fulani. Ila tambua kwamba thawabu zako za umrah ni sawa na mali utakazotumia na ugumu utakaoupata katika shuhuli hiyo." (Bukhari, *Umrah*, 8)

Maswahaba walikuwa wastaarabu na wenye tabia njema kipindi cha hija. Walishauriwa kuwa wastaara-

bu wakati wa kuizunguka kaaba, Mtume (s.a.w) aliwahi kutoa ushauri huu kwa Omar (r.a) :

"wewe ni mtu mwenye nguvu, Omar. Usiwaumize wanyonge na wenye afya dhoofu katika kuwaharakisha kwenye Jiwe Jeusi! Na wala usikerekwe, wala usimkere mwingine! Kama ukiona hakuna watu, iguse *Hajar'ul-Aswad* na uibusu. Ama vinginevyo onyesha ishara waqkati unaizunguka huku ukisema *La ilaha ill-Allah* and *Allah'u Akbar*!" (Ahmad, I, 28; Haythami, III, 241)

Wanawake hawaruhusiwi kuzunguka kabla pamoja na wanaume. Aisha (r.a) kwa mfano, alikuwa akizungumka umbali mrefu kidogo na wanaume. Mwanamke mmoja aliwahi kumwambia siku moja wakiwa wanazunguka wote kwaniiaba walishike jiwe Jeusi. Lakini Aisha (r.a) alikataa.

Aisha (r.a) alikuwa akijifunga gubigubi pamoja na wanawake wengine kiasi kwamba huwezi kuwatambua na kuizunguka kaaba wakati wa usiku. Wanaume walikuwa wakitolewa ndani ya nyumba hiyo takatifu wakati wanawake walipotaka kuingia kwa ajili ya kuabudu. (Bukhari, Hajj, 64)

Kuna tukio moja, Mtume wa allah (s.a.w) wakati akijiandaa kwenda makka, aligundua kwamba mke wake Ummu Salammah, aliyekuwa katika hedhi, hakuwa ameizunguka kaaba.

"Unapoisikia adhana kwa ajili ya swala ya "*fajr*" na watu wakaanza kuswali" alimwambia, akimaanisha kwamba anaweza kukamilisha kuizunguka kaaba, kwa kupanda ngamia nje kabisa." (Bukhari, Hajj, 71)

Umm Salammah (r.a) anasimulia:

"Nilimuelezea Mtume wa allah (s.a.w) kutokana na hali niliyokuwa nayo kwenye hija. Akanieleza niizunguke Kaaba nikiwe nimepanda ngamia pembeni ya wale waliokuwa wakiswali. Wakati huo huo, Mtume wa Allah (s.a.w) alikuwa akiwaongoza kwenye swala ya *fajr* akiwa anaisoma (*surah* at-Tur)." (Bukhari, Hajj, 64)

Kutokana na masimulizi hayo tunaweza sema kwamab wanawake wanaruhusiwa kuzunguka kaaba na wanaume, ila tu waifanye wakiwa kwa nje, kwa jinsi vile hali inaruhusu. Kuizunguka kaaba ni ibada kama ilivyo swala. Kama ilivyo kwenye swala wanawake wanajipanga nyuma ya wanaume, ni sawa kabisa wao wakijipanga nje ya kaaba wakati wa kuizunguka.

Walienzi Sana Kujifunza Qur'an na Sunnah

Allah, utukufu juu yake, anasema:

"Ni kitabu tulichokiteremsha kwako (Muhammad) chenye manufaa ili watu waweze kutafakari aya

zake na ili waweze kuaidhika walio na akili salama." (Saad, 29)

"Hakika wale wenye kukisoma kitabu cha Mwenyezi Mungu (Allah) Na wakasimamisha swala na wakatoa katika yale tuliwaruzuku kwa siri na wazi-wazi wakitaraji kupata faida isiyokuwa na hasara." (Fatir, 29)

Mtume wa Allah (s.a.w) alikuwa akiisoma Qur'an, kwanza kwa wanaume na baada ya hapo kwa wanawake. Baadhi ya Waislamuu walihifadhi na wengine waliiandika Qur'an ile.

Uandishi wa Qur'an ulifanywa na Maswahaba. Karibu kila mmoja wao aliifanya kazi hyo. Na kwa ambao hawakuwa wanajua kuandika walikua wakienda misikitini na kalamu na kutafuta wanaojua kuandika wawandikie kile walichohifadhi.

Kwa njia hiyo, Qur'an tukufu iliweza kurekodiwa na kuanza kutumika toka enzi hizo, hata katika kipindi ambacho waumini wa dini ya islam walikuwa wakionewa na walioabudu masanamu. Omar (r.a) alisilimu na kuwa Muislamu baada ya kusoma vipande vya Qur'an amabavyo vilikuwa vimeshaandikwa.

Mtume wa Allah (s.a.w) aliikabidhi nakala ya Qur'an tukufu iliyokamilika ambayo ilikuwa imebeba kila aya amabayo iliyoteremshwa, kwa Rafi ibn Malik (r.a) wakati wa kiapo Cha Aqabah. Baada ya kurudi

madina, Rafi (r.a) ataisoma Qur'ana hiyo kwa Waislamuu wapya, ambao watajikusanya kwenye msikiti mpya wakwanza wa Kiislamu, ambao Rafi aliujenga mwenyewe kwenye mji wao.

Abdullah ibn Masud (r.a) alisema;

"Wakati Maswahaba walipokuwa wakirudi majumbani kwa wake zao walikuwa wakiulizwa maswali haya mawili; "Ni aya ngapi zimshushwa Leo?" Na "hadithi ngapi za Mtume umehifadhi Leo?" (Abdulhamid Kashk, Fi Rihabi't-Tafsir, I, 26)

Maneno yafuatayo, ambayo pia yametoka kwa Abdullah ibn Masud (r.a) anaelezea zaidi jinsi amabavyo Maswahaba walikuwa wameishika Qur'an;

"Naahidi Allah shahidi yangu, tukiachana na mahala amabapo Mungu hayupo, hakuna aya iliyoshushwa na allah kwenye kitabu takatifu, ambapo mahala imeshushwa siifahamu. Tena, hakuna aya iliyoshushwa kwa mtu bila mimi kumjua mtu huyo ni nanai na ni kwa sababu gani. Kama nikisikia kuna mtu anaijua Qur'an zaidi yangu na mahali alipo ninaweza kwenda kwa kutumia ngamia, ama kwa hakika nilishafiri kwenda mahali huko, sikupoteza muda." (Bukhari, Fadail'ul-Qur'an, 8)

Baada ya muda, Abdullah ibn Masud (r.a) alihifadhi na kuifundisha aya moja ya Qur'an kwa wanafunzi wake muda mrefu huku akisema, "aya

hii ni zaidi ya vitu vyote ambavyo vimepata mwanga wa jua hapa duniani. Na atasema hivyo kwa kila aya. (Haythami, VII, 166)

Maneno yake yafuatayo yanaonyesha ni jinsi gani Maswahaba walikuwa wanajifunza sayansi ya Qur'an:

"Kwa yeyote anayependa uelewa, basi aisome kwa umakini Qur'an na apate kuielewa maana yake na kuihifadhi; ama kwa uhakika yenyewe ina elimu ya zamani na ya sasa." (Haythami, VII, 165; Bayhaki, Shuab, II, 331)

Maswahaba mara kwa mara walikuwa wakikutana kuijadili Qur- an na hadithi. Wanafunzi wa *Suffa*, siku zote huwa msikitini, wakiisoma Qur'an mchana na usiku waliijadili.

Omar (r.a) alikuwa akiitafakari sana Qur'an, akiisoma, kwa njia ambayo akaanza kuiweka katika matendo yake. Ushahidi wa haya ni katika maneno yake; "niliweza kuitekeleza sura Al-baqara ndani ya miaka kumi na mbili, na kama shukrani nilichinja ngamia." (Qurtubi, I, 40)

Imam Malik anaelezea, Abdulla ibn Omar (r.a) alisoma aya ya sura al-baqara kwa muda wa miaka nane, ili aweze kuielewa na kuitenda aya hiyo. Alikisom kitabu kwa umakini na kuhakikisha anayatenda yale aliyoamrishwa na kuyaacha yale yaliyokatazwa.

Abu Bakr' (r.a) aliwahi sema," Kuielezea aya moja kwangu ni jambo zuri zaidi ya kuisoma peke yangu." (Ibn'ul-Anbari, Kitab-u Izah'il-Waqf, I, 23)

Siku moja mwanamume mmoja - akamuuliza Zayd ibn Thabit (r.a) maoni yake kwenye kuimaliza kuisoma Qur'an ndani ya wiki moja. "Itakuwa vyema", akajibu Swahiba, akaongeza;

"Lakini huwa ninafurahia kuimaliza Qur'an ndani ya siku kumi na tano au siku ishirini. Ukiniuliza kwanini, nitakwambia ni kwa sababu naweza kuisoma kwa undani zaidi na kupata kuielewa maana yake." (Muwatta', Qur'an, 4)

Baada ya nakala ya Qur'an iliyozagaa kuwekwa katika majalada mawili, Omar (r.a) aliwashauri watu watafsiri baadhi ya makala hiyo ili waweze kuitumia wao binafsi. Sababu kuu ikiwa ni katika kuhakikisha Qur'an haipotei, iwapo watu watakuwa wamehifadhi baadhi ya surah ama aya pekee. Lakini kwa kuwa sasa Qur'an ilikuwa imekusanywa kwenye majalada mawili chini ya tume madhubuti, ikithibitishwa na maelfu ya *Huffaz*, Waislamuu sasa wanaweza kutafsiri Qur'ana wao binafsi.

Ubaydullah ibn Abdullah (r.a) anaelezea kwamba nakala ya madina, moja wapo kati ya nakala nne ambazo zilitolewa kipindi cha Othman –allah marehemu- iliwekwa katika msikiti wa Madina, na alikuwa

akiusoma kwa sauti kila siku asubuhi kwa Waislamuu waliokusanyika.

Mtume wa Allah (s.a.w) pamoja na maKhalifa wake waliwatuma Maswahaba katika Jamii zingine za Kiislamu ulimwenguni kuwafundisha Qur'an na Sunnah. Musab ibn Umayr (r.a) akiwa mmoja wao alitumwa kwenda madina mbele ya *Hijra* awe mwalimu akiwaelezea kuhusu Uislamu na kuwasomea Qur'ana kila alipopata wasaa.

Abu'd-Darda (r.a) alikwenda Damascus, alifurahia maisha yake huko na wanafunzi wake walifika 1600. Aliwagawanya kwenye makundi, akiwapatia walimu ambao ni wanafunzi wake wenye uelewe mkubwa zaidi ya wengine na mwenyewe alikuwa akiwapitia kujua maendeleo yao.Wanafunzi ambao walifaulu daraja la kwanza, walipewa heshima ya kuwa kwenye mzunguko wa Swahaba huyo. Kwa njia hayo wanafunzi waliotangulia walikuwa na bahati ya kuhudhuria Abu'd- Darda's (r.a) kwenye mzunguko wake na wakati huohuo wakiendelea kuwa walimu kwa walioanza. Njia hiyo hiyo ilitumika na Maswahaba wengine huko mahali walikwenda.

Omar (r.a) alimtuma Yazid ibn Abdullah –Allah amwie radhi kazi ya kuwafundisha mabedui Qur'an na baadae Abu Sufyan (r.a) kukagua daraja walizofikia. Vile vile aliwaagiza Maswahaba watatu kuwafundisha Qur'an watoto wa Madina, Alikuwa akiwalipa dhir-

ham 15 kila mwezi, pia aliwaeleza kuwasaidia watu wote, wakubwa kwa wadogo, kuhifadhi walau aya tano kwenye Qur'an.

Ibn Abbas (r.a) alikuwa akiwafundisha Qur'an wenye daraja la juu. Watu walikuwa wakimzunguka kila mahali alipokuwa akienda. Alipoenda Basra, Kwa mfano, jambo la kwanza alilofanya ni kutoa hotuba, akiwaelezea kuhusu sura al-Baqara.

Ali (r.a) aliwahi kusikia makelele yakitokea msikiti wa Kufa na kuulizia nini kilikuwa chanzo cha makelele hayo.

"Kuna watu wanasoma na kujifunza Qur'an," akaambiwa.

"Ama kweli wana raha," akasema, "Kwani hao ndio wa kumpendeza Mtume wa Allah." (Haythami, VII, 162)

Mujahid (aliyefariki 103 H), mtafasiri kiongozi wa zama za Tabiun, anahadithia kwamba Ibn Abi Layla (aliyefariki 83 H), alikuwa hakimu na msomi wa hadithi, alitengeneza maktaba iliyokuwa na Qur'an pekee, ambapo watu walikuwa wakijumuika kuisoma Maneno hayo Matakatifu.

Abu Abdurrahman as-Sulami akawa mwalimu wa kiraa wakati wa kipindi cha Khalifa Othman (r.a), shuhuli ambayo aliendelea kuifanya kwa miaka mingi. Kufuatia kuwa imam na mwalimu wa Qur'an,

alikuwa akipenda kusema," kitu pekee, kinachoendelea kuniweka hapa, ni kwamaba namimi nitapata kusifika katika hadithi, Wabora kati yenu ni wale wenye kujifunza Qur'an na kuifundisha." (Bukhari, Fadail'ul-Qur'an, 21; Tirmidhi, Fadail'ul-Qur'an, 15/2907)

Jamii ya *Asr-u Saadah* walionyesha shauku hiyo pia ya kutaka kujifunza hadithi. kwa mfano;

Urwah ibn Zubayr (r.a) anasimulia:

"Siku moja shangazi Aisha (r.a) aliniambia, "nimesikia kwamba Abdullah ibn Amr (r.a) anakuja kututembelea akiwa anaelekea hija. Kutana naye na umuulize maswali yote yanayokusumbua, kwa kuwa anaufahamu mkubwa sana alioupata kutoka kwa Mtume wa Allah (s.a.w). Hivyo basi nikakutana na Abdullah (r.a) na nikamuuliza maswali mengi tu kuhusu aliyojifunza toka kwa Mtume (s.a.w) (Muslim, Ilm, 14)

Abdullah ibn Amr (r.a) alikuwa akiweka kumbukumbu ya maneno aliyotamka Mtume –rehma Na amani zimshukie yeye-, haswa kipindi alichokuwepo hai. Na haikuchukua muda mrefu akawa amerekodi hadithi nyingi.

Maswahaba waliokuwa na umri mkubwa nao walipenda kujifunza mengi ingawa umri wao ulikua umekwenda.

Walitafuta Tiba na Ponyo Kutoka Katika Qur'an Tukufu

Kiini cha maisha ya Maswahaba ilikuwa Qur'an takatifu waliishi kwa kumfata allah, Utukufu juu yake. Katika hali zote hata walipohitaji tiba kwa ajili ya magonjwa yaliyowakabili, waliisoma Qur'an.

Abu Said (r.a) anaelezea:

"Tulikuwa sehemu ya jeshi lililotumwa na Mtume wa Allah -rehma na amani zimshukie yeye-. Tulipumzika mahala

Abu Said (r.a) anaelezea:

"Tulikuwa sehemu ya jeshi lililotumwa na Mtume wa Allah –rehma na amani zimshukie, Tulipumzika mahala. Muda si mrefu, alikuja mtumishi, akitokea kwenye makazi jirani na pale akasema:

"Mkuu wetu ameng'atwa na nyoka na hakuna mmoja kati yetu anayeweza kumtibu. Je kuna mmoja kati yenu anayeweza *Ruqya* (kusoma Qur'an na kuomba kutibu ugonjwa)?"

Hapo, mmoja kati yetu, ambaye haikuwa anajulikana kama anajua ruqya, akanyanyuka na kuondoka na yule mtu. Baada ya muda kidogo akarudi na mbuzi thelathini, alipewa kama shukrani kwa kumtibu mkuu wao na wote tukanywa maziwa ya mbuzi wale.

"Kwahiyo unajua jinsi ya kusoma *ruqya*?" tukamuuliza.

"Sio kweli," akajibu. "Nilimsomea *surat-l-fatiha* tu."

Tukamshauri asifanye jambo lingine lolote mpaka tutakapozungumza na mjumbe wa Allah –rehma na amani zimshukie yeye-. Tulipofika tu madina, tukamtaarifu kuhusu yaliyojiri.

"Nani kakufundisha *fatiha* ni njia ya *ruqya?*" akasema Mtume (s.a.w), akaongeza, gawanya hao mbuzi kati yenu na mimi pia nipate." (Muslim, Salam, 66, 65; Bukhari, Fadail'ul-Qur'an, 9; Ijarah, 16; Tibb, 33, 39)

Ilikuwa ni katika kuwaondoa mashaka Maswahaba katika kupokea malipo kwenye Ruqya ndo Mtume (s.a.w) akasema "na yeye pia apate". (Ayni, Umdat'ul-Qari, XXI, 271-272)

Mtume (s.a.w) anaeleza, kwenye hadith nyingine, "kuna tiba ya kila ugonjwa kwenye *surat-l-fatiha*." (Darimi, Fadail'ul- Qur'an, 12)

Ilaqa ibn Sahar (r.a) alisilimu baada ya kukutana na Mtume (s.a.w). Akiwa anarudi kwenye mji wake, akakutana na kabila, wakiwa na mgonjwa wa akili ambaye alikuwa amefungwa kwenye machuma. Familia ya mgonjwa yule ikamfata, wakasema, "Kwa tuliyoyasikia, rafiki yenu (mjumbe wa allah-rehma

na amani zimshukie yeye-) ameleta baraka. Je unajua tiba kwa ajili ya mgonjwa huyu?"

Ilaqa (r.a) anasimulia yaliyotokea baada ya hapo:

"Nikamsomea mtu yule *surat-l-fatiha*. Hapo-hapo, akapona. Kwa malipo wakanipa kondoo mia moja. Nikarudi kwa Mtume (s.a.w) kumtaarifu kwa yaliyotokea, kujua kama ni ruhusa kwangu kupokea malipo."

"Je ulisoma kitu kingine zaidi ya Qur'an?" akauliza Mtume (s.a.w).

"Hapana", nikajibu.

"Kama ni hivyo basi chukua," akasema. "Niliahidi kwa uhai wangu kama mtu atapokea malipo kwa kusoma maneno ya ushirikina basi atabeba dhambi. Lakini wewe umepokea malipo kwa haki. (Abu Dawud, Tibb, 19/3986; Buyu', 37/3420; Ahmad, V, 211)

Walikuwa Wakitubu Wakati wa Mapambazuko

Allah, utukufu juu yake, anasema:

"Walikuwa wakilala kidogo usiku. Na asubuhi walikuwa wakitubu." (ad-Dhariyat, 17-18)

Jamii ya *Asr-u Saadah* walipendelea kuamka usiku kwa ajili ya swala na kusoma Qur'an na kutaja

majina ya Allah, utukufu juu yake, mapambazukoni, juu ya vitanda vyao. Mapambazukoni na asubuhi kwao wao ilijulikana kama "nyakati za kutubu na swala" na zilifanywa kwa hisia. Watu walikuwa wakipita karibu na nyumba zao walikuwa wakisikia sauti za *dhikr* na kisomo cha Qur'an, kama vile sauti za nyuki.

Qadi Baydawi (r.a) anaelezea ifuatavyo:

Pale ambapo swala tano zilipotangazwa kuwa za ulazima kwa *ummah* na swala za usiku kuwa za hiyari (sunnah), Mtume (s.a.w) alitoka chumbani kwake, usiku, na kutembelea nyumba za Maswahaba, kujua ni yapi wanayafanya. Alizikuta nyumba zao zikiwa na milio kama ya nyuki, zikiwa na sauti za Qur'an na *Dhikr*. (Anwar'ut-Tanzil, IV, 111)

Mtume (s.a.w) anasema:

"Nazijua vizuri sauti ya Qur'an inayosomwa kwa moyo wa upendo na ukoo wa Ashari waingiapo majumbani mwao usiku. Hata nisipojua safari zao za mchana wamepumzika wapi, napata kujua kwa milio ya sauti zao wanaposoma Qur'an usiku." (Bukhari, Maghazi, 38)

Aisha (r.a) anaelezea:

"Nikiwa chumbani kwangu, mjumbe wa Allah (s.a.w) aliamka kwa ajili ya swala ya usiku (*tahajjud)* na akasikia sauti ya Abbad ibn Abdullah, akiswali msikitini wakati huohuo.

"Je hiyo ni sauti ya Abbad, Aisha?" aliuliza.

"Ndio," nilijibu.

"Allah muhurumie Abbad!" akaendelea kuomba. (Bukhari, Shahadat, 11)

Kati ya mara nane au tisa, Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- alikuwa akiisogeza swala ya *isha* mpaka kwenye theluthi ya mwisho wa usiku. Abu Bakr (r.a) akamuuliza Mtume (s.a.w) kama angekuwa akiiwhisha swala kidogo, ili iwe rahisi kwao kuamka usiku kwa ajili ya *tahajjud.*

Mtume (s.a.w) akakubaliana na maombi ya Abu Bakr -allaha amhurumie-. (Ahmad, V, 47)

Alipokuwa akiamka kwa ajili ya *tahajjud* Omar (r.a) alikuwa akiomba, "Mola wangu unaona nilipo; unajua ninachohitaji. Allah niondoshe kwako nikiwa mtumishi ambaye mahitaji yake yamekamilishwa, huru wa vitisho na uoga, ambaye papo hapo anafata maamrisho yako mtumishi ambaye dua zake unazipokea, dhambi zake unasamehe na ukamfanyia huruma!"

Na alipo maliza swala yake, aliomba:

"Allah sijaona kinachoendelea kuishi hapa duniani. Wala cha kunipa mwongozo nikafata. Allah nifanye mtu mwenye kuzungumza na uelewa na mwenye kukaa kimya kwa busara! Allah usinipe vya

duniani vingi ili nisije nikatenda dhambi na pia, usininyime kabisa, nikashindwa kukumbuka wajibu wangu kwako. Ama hakika, bora kuwa na mali kidogo iliyo toshelezi, kuliko kuwa na mali nyingi zilizopitiliza na kumfanya mtu asahau wajibu wake." (Ibn Abi Shaybah, Musannaf, VII, 82)

"Ni nani anayependwa zaidi na Mtume wa Allah (s.a.w) zaidi ya watu wote?" Aisha (r.a) siku moja aliulizwa.

"Fatimah," akajibu. "Vipi kati ya wanaume?" wakauliza tena. "Mume wake", akajibu, "ambaye ninafahamu anafunga na kuswali usiku mara nyingi". (Tirmidhi, Manaqib, 60/3874)

Amir ibn Rabia, amabaye alikuwa akiweka umuhimu kwenye swala za *tahajjud* katika maisha yake yote, iliyokea kwamaba alikufa wakati akiwa kwenye *tahajjud*. katika kipindi hicho, Waislamuu walikuwa katika adha kubwa sana, wachache waliendelea. Ilikuwa kipindi hicho ambapo Amir alimuona mtu ndotoni, akimwambia:

"Nyanyuka na umuombe Allah akulinde na adha anawalinda watumishi wake wa kweli."

Hapohapo aliamka na kuswali. Baada ya swala, muda huohuo akapatwa na ugonjwa, ambao ndo ulikuwa chanzo cha kifo chake. Watu wakaja kuubeba mwili wake kwa ajili ya mazishi, bila ya yeye kukany-

aga chini kujiunga na adha ile. (Haythami, IX, 301; Ibn Abi Shaybah, Musannaf, VI, 362/32044)

Karibu na kifo chake, Amr ibn Abdiqays, wa Tabiun, alianza kulia.

"Unalia nini?" aliulizwa.

"Ninalia wala si kwa kuogopa kifo na wala si kwa kuipenda dunia," akajibu. Ninalia kwa kuwa kuanzia sasa, sitoweza kufunga tena katika siku za joto sana na wala sitoweza kuamka usiku kufanya swala ya *tahajjud.* (Dhahabi, Siyar, IV, 19)

Yafuatayo ni taarifa iliyotolewa na watu wal-ioamini kuhusu wakati wa mapambazuko, ambapo tendo la kuabudu limepewa thamani, toba na dua zinakubaliwa, dhambi zinafutwa na mwili unakuwa wenye afya:

"Usiku zenye kujirudia ndio utawala sahihi wa kujitegemea Allah ameuzungumzia kwenye aya, 'Sema: Eeeh Mwenyezi Mungu, Mfalme wa Tawa-la! Unampatia yeyote tawala unapopenda wewe na unamnyima yeyote tawala unapopenda wewe; na umpandisha cheo unapopenda wewe na kumshusha unapopenda wewe. Mkononi mwako kuna jema; ama kwa hakika, Una uwezo juu ya kila kitu' (Al-i Imran, 26)" (Hadimi, Majmuat'ur-Rasail (Risalatu'l- Wasiyyah wa'n-Nasihah), uk. 194)

Walikuwa Wenye Bidii Kwenye Matendo ya Ibada

Jamii ya *Asr-u Saadah* walikuwa akifanya bidii sana kwenye jukumu lao la kuabudu, ingawa walikuwa wakiona ibada zao hazitoshelezi. Siku zote waliishi kati ya uoga na matumaini.

Aisha (r.a) anaelezea:

"Tutawarejeshea ule uaminifu ambao nimeubeba mabegani mwangu!" (Sarraj, Luma. p. 139)

Walikuwa Wakishindana Kutenda Mema

Jamii ya *Asr-u Saadah* walikuwa wakishindana maadili katika kutenda yaliyo ya haki. Abdurrahman ibn Abi Bakr (r.a) anaelezea:

"Baada ya kuongoza swala ya *fajr*, Mtume –rehma na amani zimshukie yeye- aliwageukia Maswahaba zake na kuwauliza, 'kuna yeyote aliyefunga leo?'

'Sikuwa nimeweka nia jana jioni, mjumbe wa allah, hivyo sijafunga leo', Omar (r.a) alisema.

'Niliweka nia ya kufunga jana jioni na leo nimeianza siku kwa kufunga, mjumbe wa allah', Akajibu Abu Bakr (r.a).

'Kuna yeyote aliyemtembelea mgonjwa leo?' akauliza tena mjumbe wa allah (s.a.w).

'Ndio kwanza tumeswali *fajr*, mjumbe wa allah, hata hatujatoka kwenye nafasi zetu', akajibu Omar (r.a). 'Tungeweza vipi kuwa tumeshamtembelea mgonjwa?'

'Nilisikia kaka Abdurrahman ibn Awf anaumwa, mjumbe wa allah. Kwahiyo nikamtembelea wakati nakuja msikitini, nikamtakia dua njema na ndipo nikaja msikitini', alikiri Abu Bakr (r.a).

'kuna yeyote kati yenu ambaye ametoa chakula kwa fukara leo?' akaendelea kudadisi mjumbe wa allah (s.a.w).

'Ndio kwanza tumeswali fajr, mjumbe wa allah, hata hatujatoka kwenye nafasi zetu', akarudia kujibu Omar (r.a).

'Lakini Abu Bakr (r.a) akasema; "nikiwa niko njiani kuja msikitini nilikutana na mtu akanieleza kuwa ana shida. Kulikuwa na kipande cha mkate wa shayiri mkononi mwa mwanangu Abdurrahman nikauchukua nikampa."

"nakupa habari njema ya pepo," mjumbe wa Allah (s.a.w) akasema.

Akishusha pumzi nzito, Omar (r.a) alisema, "oh…Pepo!"

Baada ya kumfanyia ushauri Omar (r.a) kwa maneno ya kuridhisha, Mtume (s.a.w) akasema, "Allah amhurumie Omar; Allah amhurumie Omar!

Wakati wowote anapotaka kufanya jambo jema, Abu Bakar siku zote anakuwa ameshamtangulia. (Haythami, III, 163-164; also see, Abu Dawud, Zakat, 36/1670; Hakim, I, 571/1501)

Hili linatufundisha umuhimu wa kuishi kila wakati kwa kufanya yale yenye kumpendezesha allah, utukufu juu yake, na siku zote matokeo ya matendo yetu yanakwenda sambamba na malengo yetu.

Qur'an inasema:

"Hata unapopata tulizo, endele kufanya kwa bidii. Fanya jitihadi kumpendezesha mola wako." (Al-Inshirah, 7-8)

Walifuata Sunnah Hatua kwa Hatua

Fudayl ibn Iyad (r.a) anasema:

"Tendo linalofanywa kwa utulivu *(ikhlas)* halitokubalika kama halijafata masharti (*shurut*). Na tendo litakalofanywa kwa kufata masharti halitokubalika pia kama halitofanywa kwa unyofu. Litabaki kuwa halijakubaliwa, kama masharti na utiifu vitafanywa tofauti. Utiifu ni kufanya tendo likampendezesha allah, utukufu juu yake, pekee na ilhali njia sahihi ya kukamilisha masharti ni kwa kufuata Sunnah."

Ama kwa hakika, Kumtumikia Mtume (s.a.w) ni kumtumikia Allah, kama ilivyoelezewa katika *ayah:*

"Yeyote atakayemtii Mtume, ama Kwa hakika amemtii allah, na kwa yeyote atakayeasi, basi hatujakutuma wewe kama mwangalizi juu yao." (an-Nisa, 80)

Baada ya kuukumbatia ukweli huu, mtu wa *Asr-Saadah* alifata kwa uangalifu wa hali ya juu Sunnah za Mtume (s.a.w) katika matendo yote na tabia.

Kwa kundi la vijana wa kiume waliokuja kufata ushauri, Jabir (r.a) alisema:

"Mjume wa Allah (s.a.w) alikuwa kati yetu. Qur'an ilishushwa kwake na alikuwa akijua maana yake kwa undani. Na njia yoyote alifanyia mazoezi Qur'an, na sisi tulimfatisha na kufanya vilevile." (Muslim, Hajj, 147)

Umayya ibn Abdullah aliwahi kumwambia Abdurrahman ibn Omar (r.a) waliweza "kuigundua njia ya kuswali swala ya uoga (*salat'ul-khawf*) hata hivyo haikuendana na swala ya wakati wa safari."

Allah mweza alitutumia mjumbe wake (s.a.w) wakati hatukuwa tunajua lolote. "Tulifanya vilevile ambavyo tulimuona yeye akifanya." Alijibu Abdurrahman ibn Omar (r.a) (Ibn Majah, Iqamah, 73; Ahmad , II, 65, 94; IV, 78)

Qur'an inasema:

"Ewe ulioamini! Jisalimishe kwa Allah na Mtume wake; lakini mwogope Allah: kwakuwa Allah ndo mwenye kusikia na kujua yote." (Al-Hujurat, 1)

Said ibn Musayyab, mwanazuoni mashuhuri wa Tabiun, alimuona mtu akioa rakaa mbili za swala ya ziada baada ya swala ya *asr* , mwanazuoni yule hakupendezwa nalo lile jambo. Yule mtu alipogundua mwanazuoni hakupendezewa naye alijitetea hivi, "Je Mwenyezi Mungu ataniadhibu kwa kumuabudu?"

"Hapana, ama kwa hakika hatoweza kukuadhibu kwa kumuabudu," akajibu Ibn Musayyab, "lakini atakuadhibu kwa kuacha kufata Sunnah!" (Darimi, Muqaddimah, 38/442)

Ali (r.a) alikuwa ni nguzo katika kufata Sunnah za Mtume (s.a.w).

Aliwahi kuulizwa kama mtu anaweza kumpanda ngamia anayempeleka kutoa kafara kwenye hijja.

"Anaweza," akajibu.Hata mjumbe wa allah (s.a.w) alipokutana na watu wenye hali hiyo aliwaamuru wapande ngamia zao, awe wa kafara ama la. Huwezi kukutana na njia nzuri na yenye maadili kama ya Sunnah za Mtume (s.a.w) ama kufata njia ya zaidi yake." (Ahmad, I, 121)

Maneno yafuatayo yenye maana nayo yalitoka kwa Ali (r.a):

"Tulimuona mjumbe wa Allah (s.a.w) akisimama na sisi tulisimama…..na tulipomuona anakaa na sisi tulikaa." (Ahmad, I, 83)

"Ukiachana na njia yenye kumfata Mtume – (s.a.w), njia zingine zote zimefungwa kwa binaadamu." (Bursawi, Ruh'ul-Bayan, [an-Nisa, 28])

Baada ya kuchukua udhu na kupangusa juu ya *mas'h* Ali (r.a) inasimuliwa alisema, "kama asingalimuona mjumbe wa allah (s.a.w) akifanya hivyo, angejua kupangusa chini ya *mas'h* ndio sahihi. (Ahmad, I, 148, 95m 124)

Abdullah ibn Awfa (r.a) alifanya *takbir* mara nne wakati wa swala ya maziko ya binti yake. Alipofika ya nne, alisimama na kumuombea msamaha binti yake. Mkusanyiko ule ulidhani angetoa tena *takbir* kwa mara ya tano, la hasha alitoa salam upande wa kulia na kushoto na akamaliza swala yake.

"Ni nini hicho ulichofanya?" baadae wakauliza.

"Sijaongeza lolote lile kwa kile ambacho nilimuona mjumbe wa Allah (s.a.w) akifanya," alijibu. "Hii ndio njia halisi aliyofanya." (Taz, Hakim, I, 360; Ibn Majah, Janaiz, 24)

Siku moja Abu Musa Al-Shari (r.a), alishikwa na ugonjwa wa ghafla - akapoteza fahamu, kichwa chake kikiwa katika mapaja ya mke wake. Mkewe alitoa ukelele mkubwa na akaanza kulia. Lakini Abu Musa Al-Shari (r.a) alikuwa amechoka sana akashindwa kumnyamazisha. Lakini muda aliporejewa na fahamu vizuri, alimuonya, na kumwambia, "Nachukia na kukaa mbali na vitu ambavyo Mtume (s.a.w)

alivichukia na kukaa mbali navyo. Alikaa mabali na wanawake waliopenda kulia, kuchana nguo zao na kunyonyoa nywele zao kwa majonzi." (Bukhari, Janaiz, 37, 38; Muslim, Iman, 167; Nasai, Janaiz, 17)

Kipimo cha imani ni kupigana katika kufata yale aliyoaamrisha Mtume (s.a.w) hata kama upo karibu na kufa.

Alipokuwa akitoka kwenye shughuli za kulingania ama safari, Mtume –rehma na amani ziwe juu yake- jambo la kwanza kufanya ilikuwa ni kwenda msikitini. Na baada ya kuswali rakaa mbili ndipo alipoweza kwenda nyumbani. Ibn Omar (r.a) na yeye alifanya hivyo maisha yake yote.

Baada ya kukamilisha *hajj* ama *umrah*, Ibn Omar (r.a) alikuwa akisimamisha ngamia wake na kupumzika kwa muda Batha karibu na Zulhulayfah, Kwa sababu tu Mtume (s.a.w) alikuwa akifanya hivyo. Vilevile, Ibn Omar (r.a) alikuwa akiongoza swala za *zuhr, asr* , *maghrib* na *isha* akiwa Muhassab kwa muda unaotakikana na baada ya hapo alilala kidogo. Baada ya kuamka alikuwa akiwataarifu watu kwamba Mtume –rehma na amani zimshukie yeye- alikuwa akifanya hivyo pia.

Mtume (s.a.w) siku moja alinunua ngamia wa sadaka katika eneo la Qudayd, ambayo ipo kwenye barabara itokayo madina kwenda makka. Hata Ibn Omar (r.a) na yeye alifanya hivyo pia.

Kwa watu waliokuwa wakimuuliza kwanini anafanya vitu katika hali fulani, jibu lake halikubadilika:

"Kwa kuwa nilimuona mjumbe wa Allah akifanya hivyo."

Abu Raffi anasimulia:

"Niliswali swala ya *isha* nikiongozwa na Abu Hurayrah (r.a). Alisoma surat-il-Inshiqaq na aliendа kusujudu. Na nilipomuuliza kwanini alifanya hivyo alinijibu, "Nina sujudu nyuma ya uongozi wa mjumbe wa Allah kupitia sura hii na nitaendelea kufanya hivyo mpaka siku ya kufa kwangu. (Muslim, Masajid, 110; Ahmad, II, 229)

Abu Harun al-Abdi anaelezea:

"Tukiwa vijana, tulikuwa tukienda sana kwa Abu Said kwa matumaini ya kujifunza mengi kutoka kwake. Alipokuwa akituona, alikuwa akisema, "Watu ambao mjumbe wa allah (s.a.w) ametuachia kama urithi na jukumu letu. Karibuni nyote! Ama kwa hakika Mtume (s.a.w) alituambia:

"Watu watawafata. Watatoka katika kila pembe ya dunia, wakitafua kujifunza dini na kupata kuielewa zaidi. Wapokeeni wakija wenye kutafuta uelewa muwapokee kwa uzuri na wema." (Tirmidhi, Ilm, 4/2650; Ibn Majah, Muqaddima, 17, 22; Darimi, Muqaddimah, 26; Hakim, I, 164/298)

Mwanamke wa kabila la Ghifar alimuuliza Mtume 0rehma na amani zimshukie yeye- jinsi ya kusafisha matone ya damu kwenye gauni lake.

"Chukua galoni la maji," alishauri "dondoshea chumvi na uondoshe doa hilo kwa kutumia maji hayo." Katika maisha yake yote, yule mwanamke alifata ushauri ule, hakuwahi kuosha nguo zake tena bila kunyunyizia chumvi kwenye maji. Aliandika pia usia kwamba atakapo kufa mwili wake uoshwe kwa maji yaliyowekwa chumvi. (Abu Dawud, Taharah, 122/313)

Hiyo ndio ilikuwa zama ya *Asr-u Saadah.* Wakikubaliana na Mtume (s.a.w) ushauri, maneno na kuiga kila tendo kwa uaminifu,bidii na unyenyekevu ikawa kwao ndio chazo kikubwa cha furaha.

* * *

Ukomavu wa Kimaadili Katika Zama Za Furaha

Ukomavu wa Kimaadili Katika Zama Za Furaha

Zama za neema, bila shaka ni kipindi katika historia ya mwanadamu chenye fadhila za kipekee zisizo na mfano kutokana na ubora wake wa maadili na rehma kedekede. Kilikuwa ni kipindi kilichojaaliwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na ndipo sababu ya uumbaji ikapatikna kwa kupitia kwake. Kilikuwa ni kipindi kilichoongozwa na tabia yake nzuri. Kipindi hicho pia kilikuwa ni kipindi cha kumjua Allah (s.w) na Mtume wake kwa mazingatio zaidi Hebu fikiria unapoutazama mlima mkubwa ... Kutoka mbali unaonekana kama kivuli kidogo sana Lakini kwa kadri unavyosogoe karibu anapata kuona miti,matunda, ndege na maji yatiririkayo katika mito ya mlima huo. Vile vile haiwezekani kupata kumjua Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kwa kumsoma tu kutoka katika vitabu.Kumjua Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ni kumuweka katika moyo na kwa kupitia moyo huo wa kumpenda Mtume ndipo mtu anaweza kuwa karibu na Mtume. Ilikuwa ni kwa

moyo huo wa upendo Maswahaba wakafanikiwa kuishi karibu na Mtume kwa kusikiliza matakwa yake! "Iwapo baba na mama yangu, na kila kitu changu na hata maisha yangu mwenyewe nimeyatoa sadaka katika njia yako, Mtume wa Mwenyezi Mungu! "dalili bora ya upendo wetu wa kweli kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ni upendo wetu wa Qur'an na Sunna, mambo haya mawili ndio tuliyobarikiwa katika imani yetu kama ilivyotarajiwa katika hadith. Ni lazima kutekeleza Qur'an na Sunna katika masuala yetu yote ya maisha na kujitahidi kupata radhi za Mwenyezi Mungu Mtukufu, na upendo wa Mtume wake, kwa kutuonesha njia iliyoonyoka na pia kuwalingania watu wengine.

Kwa kuishi maisha ya Qur'an na Sunna, lazima kujitahidi kuwa mfano bora kwa kuviweka katika matendo mazuri ya Uislamu na kufanya kila juhudi ili kuwalingania watu waishi kama hivyo.

Walikuwa Vilele vya Unyenyekevu

Kadri Maswahaba walivyoibuka na misingi na maadili ya Kiislamu, ndivyo walivyokuwa wanyenyekevu hata wakawa ajabu.

Chini ni mfano halisi:

Salman Farisi (r.a) alikuwa mkuu wa mkoa wa Madain wakati mtu mmoja kutoka ukoo wa Taym,

aliwasili kutoka Dameski na gunia ya tini. Mtu huyo alikuwa hawezi kumtambua alipomuona Salman-Mungu awe radhi naye ambaye, kutokana na koti la ngozi la kawaida alilokuwa amevaa wakati huo.

“Njoo, unisaidie kubeba mzigo huu”, akapaaza sauti kumwabia Salman (r.a), kwa kufikiri yeye alikuwa mtumwa.

Salman-Mwenyezi Mungu kuwa vizuri anahuuma-akaenda karibu naye, kuweka gunia juu ya mabega yake bila kubisha. Haikuchukua muda mrefu kabla ya kuambiwa huyo aliyembebesha mzigo ni nani. “Huyo mtu ni mkuu wa mkoa wa Madain”, walisema.

“Tafadhali, nisamehe, "basi akasema mtu yule kwa upole.

“Sikuweza kukutambua wewe”.

“Hakuna tabu yoyote”, alijibu Salman (r.a) “ningekubebea mzigo wako popote ulipotaka niupeleke”. (Ibn Saad, IV, 88)

Mwenyezi sifa ya (Mwaminifu) watumishi wa Rehma ni wale wanaotembea ulimwenguni kwa staha, na wajinga wanapowasemesha wao huwajibu Amani Qur’an (al-Furqan, 63)

Walikuwa Bahari ya Huruma

Huruma ilikuwa sifa moja ya tofauti ya jamii ya Asr-u Saadah. Tukio hili lifuatalo linaonyesha kiwango cha juu kabisa cha huruma na ukarimu walichokuwa nacho Maswahaba, vijana kwa wazee: Hasan, (r.a) alikuwa akitembea katika njia ya mizabibu ya Madina, alimuona mtumwa mweusi akiwa na kipande cha mkat mkononi akiwa anakula mwenyewe na kumlisha mbwa kipande kidogo cha mkate aliyekuwa mbele yake. "Wewe ni nani, kijana?" Hasan (r.a) alimuuliza.

"Mimi ni mtumishi wa Aban ibn Othman" alijibu kijana yule.

"Shamba hili ni mali ya nani?"

"Ni la Aban ..."

"Msiondoke", Hasan (r.a) alisema. "Nitarudi baada ya muda mfupi!"

Hasan (r.a) haraka akaenda kwa Aban, mmiliki wa shamba la mizabibu, na kununua shamba lake mzabibu pamoja na mtumwa wake. Akarudi kwa yule mtumwa kwa mara nyingine:

"Kijana nimekununua wewe na hili shamba", alisema. "Vizuri sana," alisema kijana yule kwa heshima. "Basi ni wajibu wangu kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wewe ... "

"Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kuanzia sasa wewe uko huru ... na shamba hili ni mali yako sasa! "akasema kijana yule "kama ndivyo hivyo", nitalitoa shamba hilo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ambaye kwake umeniacha huru." (Ibn Manzur, Muhtasaru Tarihi Dimashq, VII, 25)

Kijana yule japokuwa alikuwa mtumwa lakini alikua ana imani thabit hivyo kwa nguvu ya imani hiyo alirudisha fadhila, kwa ukarimu aliotendewa. Abdullah ibn Mubarak (d. 181 AH), kiongozi na msomi wa Hadith wa kizazi cha Tabiun, alikuwa mja mwenye matendo mema.Siku moja akifuatana na jamaa zake, alitoka kwa ajili ya kwenda Hijja. Njiani, aliona mabint wawili wadogo, wanaoishi katika kibanda kidogo kandokando ya barabara. Walikua wakiishi peke yao bila mtu wa kuwatunza, mabinti hawa walikua wanaokota ndege vibudu ili kukidhi njaa kali walizonazo. Abdullah ibn Mubarak baada ya kuona hali hii alishindwa kuendelea na safari yake alikuwa na dinaar elfu moja akabakiza dinaar ishirin za kutosha kwa ajili ya safari ya kurudi kwake Dameski na jamaa zake kisha akawapatia wale mabinti zilizobaki.

"Mbona unafanya hivyo?" Rafiki zake wakamwuliza, alijibu, "Kwa jambo hili tutapata thawabu nyingi sana kuliko Hija yetu ya mwaka huu "siku moja, Sayidina Rabi ibn Haytham mbele ya macho

yake aliibiwa farasi wake mwenye thamani ya dinar elfu ishirini, kuibiwa haki. Lakini badala ya kumfuata mwizi, aliendelea na salat yake. jamaa zake baada ya kusikia hasara kubwa aliyopata,wakaenda haraka kumfariji "nilimwona mwizi alipokuwa anamfungua farasi wangu pale nilipomfunga, "aliwaambia rafiki zake.

"Lakini mimi nilikuwa nime elekeza akili yangu katika kitu muhimu zaidi katika kwa muda huo, tendo ninalolipenda sana. Hiyo ndiyo sababu ili-yonifanya nisimkimbize yule mwizi. "Jamaa zake waakaanza kumlaani yule mwizi mpaka Rabi mwe-nyewe alipowatuliza.

"Tulieni ndugu zangu ... Hakuna aliyenidhulumu huyo mwizi amiedhulumu nafsi yake tu mwenyewe. Hebu na tusiongeze chumvi kwenye jeraha lake, kana kwamba dhambi alizopata maskini yule hazimtoshi". (Bkz. Babanzâde Ahmad Naim, Uislamu Ahlâkının Esasları, s. 85-86)

Mshairi mmoja anasema:

Kimbia, kwa rehema yako, wakati muumini yu katika hatari, Na toa sehemu bora ya huruma yako kwa ajili ya mtendaji wa mabaya watu wa Asr-u Saadah pia walikua mfano kwa kuonesha huruma yao hata wanyama na mimea. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) siku moja alikutana na mtu mmoja akimkamua maziwa kondoo wake,alimwambia:

"Bakiza maziwa kiasi kwa ajili ya watoto wake." (Haythami, VIII, 196)

Katika tukio moja, Abu'd-Darda (r.a) aliwaona watu wachache wakipakia mizigo yao mizito sana katika ngamia zao. ngamia mmoja hakuweza hata kusimama mpaka Baada ya kushusha mizigo ya ziada na kuipandisha baada ya kumsadia kusimama

Abu'd-Darda akawaambia:

"Kama Mwenyezi Mungu atakusameheni kwa maumivu mnayoyasababisha kwa ngamia wenu, hakika wameonyesha huruma kubwa sana ... kwani Nimesikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akisema,

'Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kutendea wema viumbe hawa wasiosema!Kama mtapita katika ardhi yenye rutuba, basi waacheni wale kidogo!Kama mtapita katika ardhi kame, harakisheni kupita sehemu hiyo na wala msipoteze muda ili msiwape taabu hao". (Ibn Hajar, al-Matalibu'l-Aliyah, II, 226/1978)

Walipenda Kuwasamehe Watu kwa Ajili ya Mwenyezi Mungu

Daima Mtu lazima usamehe wengine, ili Mwenyezi Mungu pia naye apate kukusamehe. Sisi sote ni wakosaji kwa Mwenyezi Mungu au kwa viumbe

wengine hivyo tunasubiri kusamehewa. Abu Bakr-Mwenyezi Mungu awe radhi naye alikuwa akimkopesha misaada ya mara kwa mara mtu moja maskini mwenye kuitwa Mistah, baada ya kugundua mistah alikuwa miongoni mwa wahanga wa tukio la Ifk, waliotoa kashifa dhidi ya Aisha Mwenyezi Mungu-awe radhi naye -mama huyo, Abu Bakr-Mwenyezi Mungu awe radhi naye akaweka nadhiri kutomsaidia kamwe yeye na familia yake. Lakini Mwenyezi akabainisha wazi: "Na wale katika nyinyi wenye fadhila na wingi kuapa dhidi ya kuwapa jamaa na masikini na walio hama kwa Njia ya Mwenyezi Mungu, na wao waachilie mbali. Je, upendo kwamba Mwenyezi Mungu akusameheni? Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye huruma." (Nur-, 22) kusikia ayah hii akasema Abu Bakr- Mwenyezi Mungu-awe radhi naye "Kwa kweli, nautaka msamaha wa Mwenyezi Mungu ", nitalipa fidia (kaffarah) kwa ajili kiapo changu, na pia akawa anaendelea kutoa msaada kama ilivyokuwa kabla. (Bukhari, Maghazi, 34; Muslim, Tawba, 56; Tabari, Tafsir, II, 546)

Kama Khalifa, Ali- Mwenyezi Mungu-awe radhi naye aliandika waraka wa amri kwa Malik ibn Harith, aliyekuwa kama gavana wa Misri, maneno haya hapa chini ni sehemu ya maneno yaliyo chukuliwa kutoka katika waraka wa amri hiyo unatupa picha na mafano mzuri wa jinsi watu wa Asr u sadaah walivyokuwa wakielewa maana ya msamaha "msichukulie mwa-

nadamu kama mbwa mwitu anayewatolea macho kundi la kondoo! Malezi katika hisia za moyo wako wa upendo, huruma na wema kuelekea yao, kwa maana kila binadamu viumbe ni ama ndugu yako dada au katika dini au sawa yako katika uumbaji. Wanaweza kufanya makosa au kustahimili. Kushikilia dhaifu kwa mkono na ...kama unataka Mwenyezi Mungu msamaha basi kusamehe na kuwa lenient kwa wengine! Si milele kumpinga Mwenyezi Mungu! Je, si majuto ni lazima wewe kusamehe, na msifurahi lazima wewe mkono nje adhabu!

Akinukuu mfano huo uliomucha bumbuwazi Isam ibn Mustaliq anasema:

"Nilikuja Madina. Hivi karibuni, kwa mbali nikamwona Hasan Mwenyezi Mungu-awe radhi naye mtoto wa Ali Mwenyezi Mungu-awe radhi naye. Nikavutiwa na sura yake nzuri na tabia yake nzuri. Lakini hayo yote hayakuweza kuficha hisia za chuki ndani yangu ya moyo wangu, Kutokana na siri kubwa na kinyongo niliyokua nayo kwa baba yake. Bila kutaja jina la baba yake, nikamuuliza: 'Je, wewe ni mjukuu wa Abu Talib? Haraka alisema 'Ndiyo', nikaanza kuwalaani wote yeye na baba yake, kwa kutumia maneno ambayo mtu mwenye akili zake angelifikiri mara mbili kabla ya kutamka. Wakati huo, Hasan-Mwenyezi Mungu-awe radhi radhi naye –akastaajabu sana huku akiniangalia kwa huruma.

Baada ya kusema Bismilah, akasoma aya ifuatayo: 'Chukua na kusamehe, na amrisha mema, na kugeuka kando na majaahili. Na lazima maoni ya uongo kutoka Shaytan wanaowatesa ninyi, jikinge kwa Mwenyezi Mungu;Hakika Yeye ni Mwenye kusikia, Mwenye kujua. Wakati kujiliwa kutoka Shaytan taabu wale walinzi dhidi ya uovu, wao kukumbuka na ghafla waone'! (al-Araf, 199-201)

Kisha alinipa ushauri ufuatao:

'Pendelea kuwa na busara! Kututakia msamaha kwa Mwenyezi Mungu kwetu sisi wote! Kwa maana kama ungelitaka msaada kutoka kwetu, tungelikusaidia bila kusita. Kama ungelitaka kuwa mgeni wetu tungekukaribisha vizuri kwa upendo kama mgeni wetu, na kama ungelitutaka tukufundishe na si tungelikufundisha vizuri na kuonesha njia sahihi!'

Alipojua kwamba nimejuta kusema yale maneno akasoma aya hii: '... Hapatakuwa na lawama juu yenu siku hii; Mwenyezi Mungu atakusameheni, naye ni Mbora wa kurehemu huruma!' (Yusuf, 92) 'Je, wewe umetoka Dameski?' aliniuliza, nilijibu 'Ndiyo' baada ya hapo,akathibitisha kwamba mimi namuunga mkono na ni msaidizi wa Muawiyah akanisomea shairi hili lililooneshwa kutoshutushwa kutendewa vibaya na watu wa Dameski.

Kisha akiwa ni mwenye furaha na bashasha, alisema, 'Karibu ... amani ya Mwenyezi Mungu iwe

juu yenu! Mwenyezi Mungu awape afya na nguvu, na Yeye awaongoze! Kama mmepatwa na shida msijisikie haya tuambieni tutawasaidia, tuombeni chochote kutoka kwetu mnachojisikia. Inshaallah utaona kwamba sisi ni watu wazuri kuliko vile unavyofikiria!

Nilijisikia aibu. Nilitamani Dunia ifunguke ipasuke na niingie inimeze. Kisha nikapotea maeneo hayo nisiwepo kwenye upeo wake.Lakini jambo moja lilikuwa kwa uhakika. Baada ya hatua hiyo, hakuna mtu aliyekuwa akinipenda zaidi ya Ali na Hasan-Mwenyezi Mungu-awe radhi radhi naye'." (Qurtubi, Tafsir, al-Araf, 201)

Daima mtu ni hushindwa na wema, kama ilivyoelezwa katika Qur'an:

"Na mema na mabaya ni si sawa. Kinga maovu kwa kutenda nini ni bora, na ghafla yeye ambaye alikuwa na uadui, atakuwa kama rafiki jamaa wa joto." (Fussilat, 34) Tukio hili linaonyesha athari ya maadili mema kwa wanaadamu. Kuushinda moyo kwa kusamehe na hivyo kuonesha maadili ya Kiislamu yalivyo na ushawishi mkubwa kwa wengine. Mamun ibn Mihran alikuwa mwanazuoni wa Tabiun,aliyejitoa sana kwa kufanya ibada. Jioni moja, alikuwa na wageni nyumbani kwake kwa ajili ya chakula cha jioni, mtumishi wake aliteleza na kudondosha chakula cha moto. Mamun kwa maumivu aliyoyapata akaonyesha hasira za wazi kwa mtumishi wake. Kuogopa matokeo

ya hali hii, mtumishi huyo akasema: “bwana unachoweza kufanya sasa, ni kutimiza amri ya Mwenyezi Mungu na *‘dhibiti hasira zako’* .”

“Nimeshafanya hivyo”, alijibu Mamun na mara moja akatulia Hamasa, yule mtumishi akaendela katika aya hiyo. “Ni lazima pia kuzingatia amri ya ‘kusamehe wengine". “Ni kweli”, alijibu Mamun. “Mimi nimekusamehe!” basi yule mtumishi aliendelea na aya ile, akimkumbusha jinsi Mwenyezi Mungu, utukufu kwake, anavyopenda ukarimu (Muhsin). “na hivyo nitakuwa mkarimu kwako kwa amri ya Mwenyezi Mungu”, alisema Mamun.

“Na kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kuanzia sasa, wewe uko huru” (Kurtubi, IV, 207, [Al-i Imran, 134])

Walijipamba kwa sifa Mbili Za Mtume: Mkweli (Al-Sadiq) na Mwaminifu (Al-Amiin)

Wakati Mtukufu Mtume-(s.a.w) alitoa kiasi kikubwa cha mateka (nyara) kutoka Hunayn kwa wakazi wa Makkah kwa matumaini ya kutoa somo juu ya Uislamu, baadhi ya Maswahaba wa kiansari wakasema, “Hii ni ajabu! Panga zetu bado zina matone ya damu za Maquraysh badala yake tunapokea nyara wetu!

“Mtukufu Mtume (s.a.w) akahisi uchungu wanaoupata, akawakusanya askari waansari na kuwuuliza:

"Je, ni kweli kwamba mmesema haya mambo? Maswahaba sasa walikuwa wakiona aibu na kujuta juu ya maneno yao. Hata hivyo, pamoja na hayo wakainamisha vichwa vyao, walijibu, "Ndiyo ... Tumesema hasa yale mliyoyasikia!" kwa sababu tu kwao kusema uongo ni mwiko (Muslim, Zakat, 134)

Hata maadui wa Uislamu wangelishangaa kuona uaminifu wa kiasi kile kwa Waislamuu na kuchukua maneno yao. Baada ya vita vya Uhud, Abu Sufiyan, Kamanda wa jeshi la makafiri (washirikina), akamwita Omar Mwenyezi Mungu- Mwenyezi Mungu-awe radhi radhi naye akamuuliza:

"Nijibu Omar, kwa jina la Mwenyezi Mungu ... Je, ni kweli tumemuua Muhammad?"

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu hamjamuua", alijibu Omar- Mwenyezi Mungu-awe radhi radhi naye. "na hapa ninavyoongea na wewe anawasikiliza"

"Abu Sufiyan akasema: "Nina imani zaidi na maneno yako, Omar, kuliko Ibn yetu wenyewe Kamia ambao walitupa taarifa ya kuuawa kwake" (Ibn Hisham, III, 45;! Waqidi, I, 296-297; Ahmad, I, 288; Haythami, VI, 111) Hii ni ajabu kwa mshirikina anayekiri ni kutoamini maneno ya mshirikina mwenzake aliyepigana vita pamoja naye, bega kwa bega,lakini akaamini maneno ya Waislamuu na ambaye walifungana mapanga vitani Ingawa kama ni ajabu lakini ni asili tu ya binadamu kupendezwa na kumuamini sana yule mwenye sifa

hiyo thabiti. Mjumbe mmoja kutoka Yemen alifika kwa Mtume kumuomba awapatie Swahaba mmoja wa kwenda kuwafundisha Uislamu na Sunnah huku akimshika Abu Ubaydah ibn Jarrah Mwenyezi Mungu-awe radhi naye -Mtume (s.a.w) akasema:

"Huyu ni Mtu mkweli kati ya watu wangu wengi", na kumtuma Swahaba yule huko mbali kwa wayemeni. (Muslim, Fadailu's-Swahaabah, 54, Ahmad, III, 146) Tukio hilo hapo juu linaonyesha jinsi namana ukweli na umanifu unavyoweza kumpa mtu daraja hata akasifiwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w).

Walikuwa Wingi wa Huruma Katika Ukarimu na Kutoka Wabinafsi

Kwa malezi ya Mtukufu Mtume (s.a.w) Maswahaba walikuwa walijifunza sehemu kubwa ya ukarimu wake na kutokuwa na ubinafsi. Alisema Jabir- Mwenyezi Mungu-awe radhi radhi naye "sikupata kumjua mtu yeyete kutoka aidha Ansar au Muhajirun ambaye hakuwa muaminifu." (Ibn Qudamah, al-Mughni, V, 598) Ibn Hazm anasema:

"Maswahaba wengi ikiwa ni pamoja na Abdullah ibn Omar na Fatimah-Mwenyezi Mungu awaridhie walichangia amana mbalimbali ndani na nje ya Madina. Haya ni maarifa ya kawaida kabisa hakuna hata

mtu mmoja ambaye halijui hili." (M. Abduh Yemani, Fatimatu'z-Zahra, Beirut, 1996, uk. 330)

Khalid ibn Walid kamanda wa Kiislamu -Mwenyezi Mungu-awe radhi naye -alitoa mapanga yake na ngao, na vifaa vyake vyote vya kijeshi kama uaminifu katika njia ya Mwenyezi Mungu, utukufu kwake. (Bukhari, Zakat, 49, 33, Jihad, 89; Waislamuu, Zaka, 11)

Ubaidullah ibn Abbas- Mwenyezi Mungu-awe radhi naye-alikuwa safari, akifuatana na mtumishi wake, ambaye zamani alikua Mtumwa akamuachia huru.wakiwa njiani, waliona nyumba ya Bedouin. "Je unaonaje tukienda nyumba ile pale ?" Ubaidullah alipendekeza kwa mtumishi wake. "Tunaweza kupumzika .. na pengine hata kutupitisha usiku pale. "Basi wakaenda. Ubaidullah alikuwa ni mtu wa madoido na mbwembwe sana, yule Bedouin alipowaona mbele ya mlango wake, alijisikia fahari kumkirimu kwake. "Tuna mgeni Mtukufu!" Alimuita nje mke wake. Baada ya kukaribisha wageni wake,yule bedouin akarudi kwa mkewe na kumuuliza kama wana chochote cha kuwapa wageni wao." Hakuna kitu isipokuwa kondoo... ambaye binti yetu mdogo anamtegemea kwa maziwa yake ya kila siku", alisema kwa masikitiko. "Hatuna budi kumchinja!" Alisema yule bedouin.

"Hivyo itakuwa kama mauaji ya mtoto wetu!" akajibu mkewe.

"Na iwe hivyo basi", alijibu Bedouin kwa ushujaa. Bedouin akamuweka kondoo juu ya ardhi, basi akachukua kisu, na kusoma shairi fupi:

Usiamke ewe binti yangu ... kwa maana ukiamka utanipora kisu changu na kulia. Akachinja koo la kondoo yule na kutayarisha kitoweo cha nyama ya kondoo yule, na kuwapa Ubaidullah na mtumishi wake.

Ubaidullah alikuwa amesikia mazungumzo nyeti kati ya Bedouin na mke wake. Asubuhi, Ubaidullah aliumuliza mtumishi wake kama wana fedha kiasi chochote.

"Ndiyo ... karibu dinar mia zilizobaki katika safari yetu", alisema yule mtumishi wa Ubaidullah. "Mpe Bedouin zote", Ubaidullah alisema.

"Dinar mia tano zote?" Aliuliza kwa mshanago yule mtumishi. "wakati yeye katuchimjia kondoo mwenye thamani ya dinari tano tu?!

"Ona haya japo kidogo!" Alijibu Ubaidullah. "Usifanye makosa kudhani kwamba yeye ni mkarimu kuliko sisi. Tulimpa kile ambacho sisi tunacho, hata hivyo, naye alitupa chote alichokuwa nacho ... alijali faraja na furaha yetu kuliko maisha ya binti yake. Hatuna Tunachoweza kufanya kufidia kile alichofanya kwetu,hatuwezi kulipa hilo milele!" Muawiyah alipopata habari kuhusu tukio hilo,alisema, "Ubaidullah

ni mja mwema sana ameonyesha yeye ni mwana wa nani na nyumba gani amekulia." (Ibnu'l-Athir, Usdu'l-Ghabah, Beirut, 1417, III, 543;! Ibn Asakir, Tarikhu Dimashq, XXXVII, 483-484)

Ubaidullah alikuwa mtoto wa Abbas (r.a), ambaye alikuwa mjomba wa Mtume wa mwenyezi Mungu (s.a.w). Siku moja alikuja bwana mmoja masikini akiwa kwenye saum, alifika mlangoni mwa Aisha (r.a) na kuomba kitu chochote apate kufuturu. Hakuwa na kitu chochote zaidi ya kipande cha mkate tu. "Mpe huo mkate yeye", alisema mtumishi wake.

"Lakini huna kitu kingine cha kufuturu", alijibu mtumishi.

"Hata hivyo mpe tu", alisisitiza Aisha- Mwenyezi Mungu awe radhi nae Yule mtumishi akaendelea kusimulia baada ya hapo "Nilimpatia mkate maskini yule. Jioni yake Aisha Mwenyezi Mungu awe radhi nae alileteWa nyama ya kondoo. Aliita na kuniambia: 'Chukua kadri ya uwezo wako... hii ni tamu kuliko ule mkate!" (Muwatta, Sadaqah, 5) Inaelezwa kwamba Ibn Omar Mwenyezi Mungu- awe radhi nae –alikua hakai chini kula pasi na kuwepo yatima mmoja kula naye. (Bukhari, al-Adabu'l-Mufrad, hakuna: 136; Abu Nuaym, Hilyah, I, 299) Hasan Basri, ambaye alikuwa na bahati ya kuwaona Maswahaba wengi,alisema: "Nilishuhudia mara mara nyingi baada ya kuamaka asubuhi, kila Muislamu alikuwa anaisihi familia yake kuwachunga maya-

tima na kuwatendea wale wenye shida karibu yao,! 'Na leo, watu wema wameondoka na hao waliobaki ni wadhaifu kiroho. (Bukhari, Adabu'l-Mufrad, hakuna: 139)

Waliepuka Israfu

Aqil ibn Abi Talib- Mwenyezi Mungu awe radhi nae - siku moja alikuwa akihadithia misemo ya Mtume (s.a.w), alisema: "maji ya bakuli yatosha kwa ajili ya kutia udhu na si 'kuosha mwili wako wote".

Alikuwapo mtu mmoja akasema, "Hayo maji si mengi kututosha sisi"! Kisha Aqil akichukua nafasi ya Mtume alisema: "Hayo maji yaliweza kuwatosha watu wakubwa na wenye nywele nyingi kupita nyinyi" (IbnMajah,Taharah,1)

Kathir ibn Ubayd, mtumwa huru wa Abu Bakr na ndugu wa hiari wa Aisha-Mwenyezi Mungu awe radhi nao-, anakumbuka maneno haya: "Nilipata kwenda kwa Aisha sikumoja akaniambia nisubiri nje ili aliweza kumaliza kushona vazi lake lilikowa limechanika. Mimi nikasema,ningependa kuwaambia wengine kile unachokifanya kama si kuhofia wao kukuita bahili.'Wewe jali mambo yako', alinijibu. 'Yule ambaye hawezi kuvaa nguo zamani, kamwe hapati furaha avaapo nguo mpya'" (Bukhari, Adabu'l-Mufrad, namba: 471; Ibn Saad, VIII, 50) !

* * *

Walitilia Umuhimu Mkubwa Juu ya Malezi ya Kiislamu

Walitilia Umuhimu Mkubwa Juu ya Malezi ya Kiislamu

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alijitahidi kuisambaza elimu kila alipopata fursa ya kufanya hivyo.Mathalan ilikuwa kwa wale mateka wa vita vya Badr wenye kujua kusoma na kuandika ili waweze kuachwa huru walipaswa kuwafundisha watoto kumi wa Kiislamu kusoma na kuandika.Shule ambazo elimu hii ilitolewa na walimu Waislamu na wale wasio Waislamu ziliitwa *Kuttab.*Mashule haya (*Kuttab)* yalifunguliwa kipindi hicho ili kwamba watoto wajue kusoma na kuandika pamoja na kujifunza misingi ya Uislamu.

Maswahaba walizigeuza nyumba zao kuwa mahala pa kujifunzia. Msikiti wa Madina haukuweza kukidhi mahitaji ya ziada ya mafunzo ya *Suffa* yaliyokuwa yanayotolewa katika shule zijulikanazo kama Daru'l Qura hivyo ikabidi kufunguliwa *Daru'l Qura* za ziada katika baadhi nyumba katika mji huo. Mathalan, nyumba nzima ya Mahrama ibn Nawfal ya Mwenyezi Mungu awe radhi nae - ikageuka Daru'l-Qura, amba-

po Abdullah ibn Ummi Maktum- Mwenyezi Mungu awe radhi naye -alikaa kuwa kama mlezi aliyekuwa akisimamia mafunzo hayo.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alimuweka mateka mmoja kutoka kabila la Hawazin chini ya ulinzi wa Ali- Mwenyezi Mungu awe radhi nae ili aweze kumfundisha mateka huyo baadhi ya sura za Qur'an zilizochaguliwa. (Ibnu'l-Asir, Usdu'l-Ghabah,VII, 105; Ibn Hajar, al-Isabah, IV, 292)

Maadili Yao ya Kibiashara yalikuwa ya Kipekee

Jarir bin Abdullah (r.a) alikuwa sokoni alitaka kununua farasi. Akamuona farasi aliyempenda, ambaye muuzaji alisema alikuwa akimuuza kwa dinar mia 5. Lakini Jarir Mwenyezi Mungu awe radhi nae -alimwambia mtu huyo kuwa angetoa Dinar mia 6 hata kumongeza inar mia 8 kwa kuwa farasi yule alikuwa na thamani kubwa sana pasi na muuzaji kujua."Kwanini unaongeza bei" aliuliza mmiliki kwa mshangao "wakati unaweza kununua farasi kwa bei nafuu? "alijibu" ... sisi tulimuahidi Mtume wa Mwenyezi Mungu kwamba kamwe hatutafanya udanganyifu katika biashara" alijibu Jabir.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na Makhalifa haki waliomfuata,walifuatilia kwa makini maen-

deleo ya masoko, walifunga mianya yote ya kodi sizizo halali na kufungua njia za mapato ya haki pamoja kuzuia kuibuka kwa wazandiki na walanguzi wakubwa wa fedha , Ili kudhibiti mabepari wa biashara,Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alipiga marufuku wafanyabiashara kumiliki masoko katika soko, na wale wafanyabiashara walioshindwa kuzingatia sheria walichaniwa mahema yao ya kufanyia biashara.

Udugu Wao Wa Kiislamu Ulikuwa wa aina Yake

Ilipotokea kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) asipomuona mmoja wa ndugu zake katika dini kwa muda wa siku tatu mfululizo, alikuwa akiulizia habari ya huyo muumin.

Kama alimbiwa yuko katika safari, basi alimuombea dua kwa Mwenyezi Mungu amfikishe salama katika safari yake na kama alikuwa nyumbani au mgonjwa, atahakikisha anakwenda kujulia hali. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) baadaye alianzisha 'mkataba wa udugu', kati ya waansar na wahamiaji wa Madina (*Muhajirun*), ambao walikubali kutelekeza mali na utajiri wao wote huko Makkah kwa ajili ya dini yao. Sadaka hii nzito ilibarikiwa na ilikuwa sawa. Kila familia ya *Muhajirun* ilipewa hifadhi katika nyumba moja wa weneji wa Madina.

Kwa hivyo masahaba ambao walitangazwa kuwa ndugu walikuwa wakifanya kazi pamoja na kugawana kila walichokichuma. Waansar hata walitoa sehemu ya ardhi yao ya ziada kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ili aigawanye miongoni mwa Muhajirun. Bado hawakuridhika,waansar walikwenda kumwambia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w):

"... Na pia ukayagawe mashamba yetu ya tende miongoni mwa ndugu zetu na wageni wetu wahamiaji! "Hilo haliwezekani", Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema, na badala yake al waambia Muhajirun mapendekezo yafuatayo: "Mtafanya kazi ya umwagiliaji na kupalilia hiyo na baadae mavuno yatagawanywa" Kwa idhini ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w), pande zote mbili walikubaliana na wazo hilo." (Bukhari, Harth, 5)

Jabir (r.a) akikumbuka tukio hili hapa anasema

"Baada ya kukusanya mavuno ya tende, Ansar walizigawanya ndani ya chungu mbili, huku wakijaza zaidi upande mmoja kuliko mwengine. Kisha baada ya kuweka majani ya tende juu ya chungu ndogo ili kujazia na kuyafanya yaonekane n ukubwa sawa sawa na mengine,waliwaambia Muhajirun kuchukua fungu lolote walipendalo. Na wao (*Ansar*), waliwataka ndugu zao *muhajirin* kuchukua fungu kubwa zaidi, na wao muhajjirin walitaka ndugu zao (*Ansar*) kuchukua mafungu yale makubwa ya tende na wao

wabaki na yale madogo ili yale makubwa wawaachie wenyewe. Tendo Hili la ukarimu wa Ansar liliendelea mpaka kutekwa kwa Khaybar." (Haythami, X, 40)

Katika tukio jingine Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alitangulia kuwaita Ansar kabla ya Muhajirun katika kuigawa ardhi ya Bahrain. Hata hivyo, kama kawaida yao ya kutokuwa wabinafsi walisema: "Tafadhali, usitupe chochote Mjumbe wa Mwenyezi Mungu, mpaka utakapo wapa Muhajirun mara mbili ya ile sehemu uliyofikiria kutupa sisi! Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: "Nyie Ansar, kama hamtaki kuchukua chochote (Kwa ajili ya kuwapendelea ndugu zenu), basi kuweni wastahamilivu (pamoja na mateso ya dunia) mpaka mtakapokuja kuungana na mimi katika Kawthar na katika kipindi hicho watakakuwepo watu baadala yangu, wakaotazipendelea nafsi zenu kuliko zao". (Bukhari, Manaqibu'l-Ansar, 8)

Mwenendo huu wa kimaadili wa kipekee ulioonyeshwa na Ansar kwa kweli ilikuwa hatua kubwa zaidi ya ukarimu, ilikuwa. Pamoja na kuwa na mahitaji yao wenyewe,lakini bila ya kuchoka waliwajali kwanza ndugu zao kuliko wenyewe. Kwa sifa ya mawazo yao, Mwenyezi anasema: "Na walio na maskani zao na Imani yao kabla yao, wanawapenda walio walikimbilia yao, na si kutafuta katika mioyo yao haja ya kile wanapewa, na wanapendelea (yao) kabla ya

weny we ingawa umaskini inaweza msiba, na aliye ulinzi kutoka ubakhili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufanikiwa. Na walio kuja baada yao wanasema: Mola wetu Mlezi! Tughufirie sisi na yetu ya ndugu tutangulia katika imani, na kufanya si usijaalie ndani ya nyoyo zetu undani kwa wale walio amini, Bwana wetu! Hakika Wewe ni Mpole,Mwenye huruma". (Al-Hashr, 9-10)

Wakati wa zama za neema haikuwa tu kwa Ansar lakini pia waumini wa dini nzima walikuwa ni wenye maadili ya ubora wa kipekee waliopongezwa na Mwenyezi Mungu, utukufu kwake.

Sheria ya udugu imara uliyowekwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) ulikuwa hivyo hivyo hata wakati wa vita. Wakiwa kwenye harakati za kampeni, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) wakati wa kuondoka alimteua ndugu mmoja kwenda katika jeshi la Waislamu, na mwingine kumbakisha ili kulinda familia na mahitaji yao mengine kila inapobidi. Maneno haya ya Ali Mwenyezi Mungu awe radhi nae yanaleta mazingatio juu ya roho ya udugu walikuwa nayo watu wa Zama za neema: "Nafikiria baraka mbili na sijui ipi ambayo hukamilisha furaha yangu,ya kwanza ni wakati mtu anapokuja kwangu kwa matumaini kwamba mimi nina uwezo wa kumsaidia kwa dhati. Ya pili ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu anapomtimizia shida zake kwa kupitia mimi

au hata kumfanyia wepesi kwa kupitia mimi.Ningelitamani kuwa na mali nyingi za kutosha kutatua shida Waislamu duniani kote". (Ali al-Muttaqi, VI, 598/17049) Katika kuimarisha udugu wa kiroho, Anas ibn Malik-Mwenyezi Mungu awe radhi nae-alikuwa akiwashauri watoto wake "... kupeana zawadi kila mmoja, kwa maana kwamba ni mojawapo ya kuongeza upendo baina yao" (Bukhari, al-Adabu'l-Mufrad, hakuna: 595).

Siku moja Ibn Abbas- Mwenyezi Mungu awe radhi nae siku moja aliingia Masjid kwa ajili ya itiqaf, akamkuta bwana mmoja akamsalimu na kuketi chini karibu naye. "Unaonekana umechoka na kufedheshwa, ndugu yangu", alisema Ibn Abbas. "Kwa hakika ndio hivyo, ewe binamu wa Mtume 'alijibu. 'Kuna bwana alikuwa ameniacha huru na ilitakiwa kumlipa kiasi fulani cha malipo... lakini kwa haki ya Mtume ameshaingia katika kaburi hivyo, siwezi kumlipa tena." "Je, unataka nimuhabarishe kwa niaba yako?" aliuliza Ibn Abbas- Mwenyezi Mungu awe radhi nae "Hilo ni juu yako", alijibu yule bwana. Ibn Abbas-Mwenyezi Mungu awe radhi nae –alipochukua viatu vyake kutoka nje Masjid, yule mtu alimwita: "Je, umesahau kuwa uko katika itiqaf?" "hakika sijasahau. Lakini napenda kukuambia jambo moja alisema Ibn Abbas Mwenyezi Mungu awe radhi nae huku machozi yakimtiririka machoni mwake Nimeyasikia kutoka kwa huyo mtu aliyelala kaburini kwamba": "Kumsaidia na Kuhangaikia shida ya ndugu yako ni bora kuli-

ko itiqaf ya miaka kumi ... na kama mja ataingia itiqaf siku moja tu kwa ajili ya radhi ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu hutengeneza mifereji mitatu ya moto na upana wake ni sawa na umbali wa mashariki na magharibi ...” (Bayhaki,Shuab’ul-Iman, III, 424-425)

Akikumbuka uzito wa udugu ulivyokuwa Ibn Omar- Mwenyezi Mungu awe radhi nae, - nasema: “Tuliona hakuna mtu miongoni mwetu anayestahili kujifikiria mwenyewe kwanza kabla ya mwenzake na vitu kama fedha hata dhahabu havikua na thamani ya udugu tuliokuwa nao. Lakini kwa wakati huu ambao tunaishi sasa, dhahabu na fedha vina thamani kuliko udugu wetu. Niliwahi kumsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akisema, ‘ huko Akhera majirani watashikana mashati na kulalamika, ‘Ewe Mwenyezi Mungu huyu jirani yangu, alinifungia mlango wake nilipokwenda kuomba msaada kwake”. (Bukhari, Adabu’l-Mufrad, hakuna: 111; Haythami, X, 285).

Jamii Ilitawaliwa na Kuheshimiana na Kuwajali Wengine

Jamii za zama za neema, zilikuwa zikihurumiana wao kwa wao na kujaliana katika shida.Ukiacha binadamu wenzao, walikuwa wakarimu na wenye huruma hata kwa wanyama na mimea, katu hawakuweza kuvidhuru viumbe hivi kwa kwa kitu chochote. kiwango cha huruma na kujalina kilichoonyeshwa na

Maswahaba kilijidhirisha hasa wakati wa Hija. Huku wakivalia mavazi yao meupe yalifunika mwili mzima ihram,walikuwa wakionekana kama malaika. Wakati wa ibada ya Hijja,Waislamuu wote, wanaume na wanawake, walikuwa makini kujizuilia na kujionesha (Riyya) na tabia isiyompendeza Mwenyezi Mungu, kama Mwenyezi Mungu alivyoagiza, na kuinamisha macho yao chini kuangalia vidole yao,pamoja na kujizuilia kuleta ugomvi wa namna yeyote. Pia, kwa muda huo ambao waumin walikuwa katika ihram,] basi bila ya hata kuongoza wawindaji na mchezo wake, achilia mbali kuwinda wenyewe; hata maku-sudi kuondoa strand ya nywele, ilikuwa kitu wao bila kuacha. Ingawa kujihusisha katika shughuli hizi ilikuwa inaruhusiwa wakati wote mwingine, ukweli kwamba wao katazwa wakati wa kipindi fulani ya Hijja, alikuwa kurejesha katika mioyo yao mantiki kwa haja ya kuweka mbali na mambo yote imper-missible na hata mashaka. Kaimu na huruma kwa Muumba kwa ajili ya Muumba, na si kuumiza hisia yoyote au kuvunja mioyo yoyote, walikuwa mambo ambayo walikuwa milele ufahamu wa. Hii kazi hatua kwa hatua kuelekea kwenye kuzitakasa nyoyo zao kwa uhakika na kuwainua kwenye vilele vya wema na ubora.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa pia akishauri juu ya njia sahihi za kuwahudumia wan-yama, alitaka mabanda ya kondoo na mbuzi kusa-

fishwa vizuri na kufutwa mavumbi. Ibn Sawadah Rabi- Mwenyezi Mungu awe radhi nae anasimulia mfano mkubwa wa huruma wakati wa kazi: "Nimlitembelea Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kumuuliza mambo kadhaa. Kisha aliomba mimi nipewa ngamia wachache (3:10), na aliongeza: 'ukirudi nyumbani, waambie familia yako wawahudimie wanyama hawa na kuwalisha vizuri,wakumbushe pia kuwakata kucha zao ili wasiweze kuwaumiza wakamuaji maziwa wakati wanawakamua" (Ahmad bin Hanbal, III, 484; Haythami, V, 168, 259, VIII, 196).

Alipotangaza Madina na maeneo ya jirani haramu, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema: "Hapana ruhusa ya kukata miti ndani ya shamba la Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa vijiti au kwa namna yeyote ile. Lakini katika kesi ya haja, mtu anaweza kwa utaratibu kutikisa majani ya chini kwa ajili ya kulishia wanyama". (Abu Dawud, Hajj,95-96/2039)

Abu Dushum al-Juhani anakumbuka tukio alilosimuliwa na baba yake kutoka kwa babu yake; "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alimuona Bedouin akimpiga mfanyakazi wake na matawi ya mti anaotumia kuwalisha wanyama wake, 'Mwiteni aje kwangu msimtishe mwiteni kwa upole', alisema Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w)."

Yule Bedui alipofika kwa Mjumbe wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akamwambia, 'tikisa matawi polepole,

ewe Bedouin, ili majani yadondoke yasidondoke kwa nguvul ...'. Ni kama vile bado unaweza kuona majani juu ya kichwa cha Bedouin'. (Ibnu'l-Asir, Usdu'l-Ghabah, Beirut, 1417, VI, 378) kuwaelimisha Waislamu kuzingatia heshima, na kuyatunza miti na mimea Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema yafuatayo kuhusu mimea: "Hakuna miti ipandwayo dunia hii ikakoswa kulindwa na malaika wa wema. Malaika hawa wanaendelea kuilinda mimea hii mpaka pale inapopevuka, na kila anayekanyaga hupata laana ya malaika." (Ali al-Muttaqi, Kanz, III, 905/9122)

Walijizuia Na Zinaa

Usafi na wema akatawala kati ya wanaume na wanawake katika jamii ya zama za neema, kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, utukufu kwake, alivyowaambia; "na uwaambie waumin wa kike wainamishe macho yao na walinde tupu zao na wala wasidhirishe mapambo yao ila kile kitakachodhiri kwa bahati mbaya na wateremshe shungi zao kwenye vifua vyao na wala wasidhihirishe mapambo yao ila kwa waume zao au baba zao au baba wa waume zao au watoto wao wa kiume au watoto wa waume zao au watoto wa kaka zao au watoto wa dada zao au wanawake wenzio wao au wale wanaowamiliki katika mkono wao wa kuume au wale wanaowafuta katika majumba yao ambao hawana mtamanio au watoto wadogo ambao

hawajaanza kutazama uchi wa wanawake wala wasipige pige miguu yao ili kikafahamike kile walichokificha ktk mapambo yao na toeni toba kwa m/Mungu enyi waumini wa kweli ili mpate kufaulu! (Nur-, 30-31) Aisha (r.a), anaripoti:

Baada ya kushuka kwa aya hii mara moja masawhaba wa kike walianza kukata vitambaa ziada katika nguo zao kwa ajili ya kufunika vichwa vyao na mabega kama walivyoagizwa katika aya hiyo. (Bukhari, Tafsir, 24/12; Abu Dawud, Libas,31-33/4102) Safiyya bint Shaybah (r.a) anasimulia baada ya Mwenyezi Mungu kuteremsha amri hiyo, wanaume walikwenda majumbani mwao na kuwasomea wake zao, dada zao na mabinti zao. Wanawake wakageuza hata nguo zao nzuri kuwa hijjab kujifunika toka kichwani mpaka miguuni. Kwa kufanya hivyo, walionyesha kwa kiwango gani wanaheshimu na kutii amri ya Mwenyezi Mungu.Inapowadia swala ya Fajr wanawake waliwahi nafasi zao katika safu za misikiti wakiwa wamejifunika kutoka juu hadi chini. Maswahaba walilinda sana mipaka ya maingiliano ya watu wa jinsia tofauti. Wanaume na wanawake, ambao walikuwa hawafahamiani kisheria walikuwa hawachangani pamoja na kila mmoja alikaa mbali na mwenzake kuepusha tu ile tu mtihani baina yao. Katika maisha ya kijamii ya kila siku ,siku zote maingiliano kati ya wanaume na wanawake yaliwekewa mipaka na pale ilipotokea maingiliano baina ya jinsia mbili tofauti basi sheria na nidhamu vilifuatwa.

Baada ya yote, si tu Uislamu ulizuia dhambi, bali pia ulizuia tabia na mazingira ambayo kuchochea mazoezi ya dhambi. Uislamu haukuzuia tu kufanya zinaa bali hata maeneo na mazingira yanayopelekea watu kufanya zinaa kwa kufunga mianya yote inayochochea watu kufanya hivyo. Pamoja na kuweka umuhimu mkubwa wa sala na sadaka nyingine siku ya Ijumaa, Uislamu ukawapa ruksa wanawake kuswalia majumbani mwao ili tu kuepusha maingiliano ya wanaume na wanawake, na kupendekeza ni vyema kwa wao kufanya swala na maombi yao majumbani badala ya misikitini. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alisema:

"Msikiti bora kwa wanawake ni kona za nyumba zao". (Ahmad, VI, 297)

Hata hivyo, Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) hakuwazuia wanawake kuhudhuria misikitini na alitoa idhini kwa wale ambao walitaka kufanya hivyo. lakini akaelekeza wanawake wanaohudhuria misikitini kutojipanga safu sawa na wanaume lakini badala yake wakae nyuma yao.

Baada ya kila sala wawapo msikitini Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) na Maswahaba waliwasubiri wakina mama watangulie kutoka msikitini kwanza kuelekea maju mbani mwao kisha wao ndio wangetoka. Tu kisha wasingeli kufanya njia yao nje. Hasa baada ya sala ya Fajr, ambayo iliswaliwa kabla ya jua

kachomoza, wanawake walijifunika na nguo zilivofunika juu ya nguo zao mpaka kichwani na kwenda majumbani mwao ili isiwe rahisi kwa wao kubainika. Kulikuwa na wakti hata wao kwa wao walishindwa kutambuana. Mtume wa Mwenyezi Mungu alipendekeza kutenga mlango mmoja wa msikiti kwa ajili ya matumizi ya wanawake pekee, ambapo Maswahaba wa kiume hawakutakiwa kuutumia mlango huo. (Abu Dawud, Salat, 53/571)

Pia wanawake hawakukatazwa kuhudhuria sala ya Eid, lakini kama ilivyo kawaida, sehemu yao ya kusalia ilikua na umbali fulani pale walipo wanaume. Mara baada ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) kumaliza hotuba yake kwa wanaume, atakwenda kwa kina mama na kuwahutubia pia. (Bukhari , Iydayn, 7-8)

Siku moja, wakati Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) akitoka msitini aliona wanaume na wanawake kwa bahati mbaya wamechanganyika akitembea, ambapo akapaza sauti kuwaambia wanawake "... tembeeni kando ya barabara na siyo kutoka katikati." Kwa kuyasikia hayo, toka hapo hiyo wanawake walianza kutembea pembezoni kabisa mwa kuta za barabara kiasi kwamba nguo zao zilikuwa zinagusa ukutani. (Abu Dawud, Adab, 167-168/5272)

Aisha (r.a) aliwaona wanaume na wanawake wamechanganya wakati wa kipindi cha Bani Umayya alisema, "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) angeli-

ona hili,angelipiga marufuku wanawake kuingia misikitini kama ilivyokuwa kwa wana wana wa Israeli." (Bukhari, adhan, 163)

Nyuso Zao Zilikuwa Na Tabasamu Daima

"Je, ucheshi ni mbaya?" Mtu mmoja alimuuliza Sufiyan Uyaynah ibn (r.a) (d. 198AH). "Kinyume chake ni sahihi", alijibu, "ni Sunna; kwani Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w)amesema, ninayoyatenda ni kama ucheshi lakini siku zote ni ya kweli."

"(Nuwayri, Nihayatu'l ya Kiarabu ya fi Fununi'l-Adab, Cairo, IV, 2) lakini usfanye kumuudhi mtu badala yake uwe kwa ajili ya kuleta umoja na kupatanisha watu. Ibn Qayyim al-Jawziyya (d. 751 AH) anasema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) wakati akitenda na akizungumza alionekana mcheshi siku zote, ingawa ailyoyasema yote yalikuwa ya kweli. Hotuba zake zilijaa *metonymy* ndani yake ambazo zilitumika kuelezaea ukweli". (Ibn Qayyim al-Jawziyya, Zadu'l-Maad, I, 58)

Maswahaba walikuwa pia ni wenye furaha na kujua jinsi ya kuishi na watu,walijua wapi pa kusema nini na kwa nini wamesema hivyo. Pale walipohitajika kuwa wachesi walifanya na pale walipohitajika kuwa na mazingatio pia walifanya hivyo,hivyo maisha yao yalikuwa kwa mlingano huo ulio sawa. Bakr ibn

Abdullah (r.a) anasema: "Maswahaba mara kwa mara walikuwa wakitaniana wao kwa wao kwa kutumia matikiti. Lakini napokuja suala la kuhitaji mazingatio walilifanya kwa umoja" (Bukhari, al-Adabu'l-Mufrad, no:266).

Abu Salamah bin Abdurrahman- Mwenyezi Mungu awe radhi nae –anawaelezea Maswahaba kama ifuatavyo:

"Maswahaba walikuwa si watu wa kubweteka na kukaa bila shughuli ya kufanya.Katika mikusanyiko yao walipokuwa na muda kidogo basi walisoma mashairi na kusimuliana hadithi za maisha yao ya zama za Ujinga. Lakini inapotokea mmoja kati yao alikuwa anakabiliwa na wajibu wowote kuhusu dini ya Mwenyezi Mungu, basi nafsi yake haikutukia mpaka oale atakapolifanikisha lile jambo" (Bukhari, al-Adabu'l-Mufrad, no: 555).

Thabit bin Ubayd anaelezea:

"Sijawahi kumuona mtu makini zaidi kuliko Zayd ibn Thabit, ingawa pia sijawahi kumuona mtu mchesi zaidi yake pale nyumbani" (Bukhari, al-Adabu'l-Mufrad, hakuna: 286). Siku moja Omar- Mwenyezi Mungu awe radhi nae alimuona Bedouin akiomba Baada ya swala ya,akisema kiutani , "ewe mwenyezi Mungu niozeshi kwa malaika wa peponi"!

Omar alimwambia:

"wewe ... unaomba malipo makubwa kwa kazi ndogo sana uliyofanya" Kwa mujibu wa taarifa ya Abu Bakr as-Saqafi, Maswahaba walikuwa wakisoma Qur'an na mashairi kwa kupishana siku. (Kattani, at-Taratib, II, 236)

Ibn Abbas- Mwenyezi Mungu awe radhi nae anapokuwa na wanafunzi wake huwasimulia hadithi chache, na kisha kusema:

"Matumbo yetu yanapokuwa na kiu yanywesheni utani au baadhi mistari michache ya mashairi, kwani nafsi pia huwa zinachoka kupata dawa na hivyo huchoka kama mwili vile unavyochoka."

Alikuwa akifanya hivi huku akileta ucheshi wa hapa na pale huku akinukuu baadhi mifano mashuhuri ya Waarabu, ambapo baadaye angeweza kuendelea somo, na alikua akirudia utaratibu huu wakati wote pale inapohitajka. (Kattani, at-Taratib, II, 237) Abu'd-Darda Mwenyezi Mungu awe radhi nae alihakikisha anatabasamu pale anapokuwa anazungumza chochote, Siku moja, mke wake akamwambia, "nahofia watu wanaweza kupata hisia mbaya." "alijibu na kusema daima kulikuwa na tabasamu katika hotuba za Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w)." (Ahmad, V, 198, 199)

Abdullah ibn Muhammad, mwanazuoni wa kizazi cha Tabiun, alikuwa mtu wa bashasha na mcheshi. Hata pale alipokwenda kumangalia shangazi yake

Aisha- Mwenyezi Mungu awe radhi nae wakati anaumwa amelala kwenye kitanda alichofia, Abdullah ibn Muhammad hakusita kumfanyia mzaha shangazi yake. Inasemekana kwamba alimtembelea shangazi yake wakati yupo katika sakrat maaut, alimuuliza: "Unajisikiaje shangazi yangu kipenzi?" akaendelea kumwambia "kwa jinsi nnavyokuona nakuhakikishia hii ni hatua ya mwisho kabisa ya kufa kwako". Aisha- Mwenyezi Mungu awe radhi nae alishangazwa kumwona mpwa wake akiendelea na utani wake hata katika mazingira hayo, Aisha Mwenyezi Mungu-amrehemu-alisema: "Wallahi, inaonekana utakujua kuacha tabia yako!" (Ibn Saad, VIII, 76)

Kwa Mukhtasari

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w) alikuwa na huruma si tu kwa ajili kwa wanadamu lakini pia kwa vyote vilivyoko ulimwenguni. Muonekano wake na nuru yake ya ajabu viliangaza na kumulika mpaka katika anga zenye kiza kinene zikimaanisha kuja kwa zama mpya amabazo wanaadamu walikua wakizisubiri. Nuru yake iliangaza duniani na kumulika mpaka katika anga zenye kiza kinene zikiashiria kuchomoza kwa siku mpya ya nusra ambayo mwanadamu alikua akisubiri,

Mioyo ya wanadamu ilifunguka, macho pia yakapata kuona neema za Mwenyezi Mungu. Kwa

Baraka za neema na ujio wake Mtume (s.a.w) Ulimwengu ukapata nusra ya kweli kabisa .

Mwanadamu akapatanishwa na haki utu wake ambao alikosa kwa kipindi kirefu. Alikuwa ni Mtume (s.a.w) aliepatanisha mwanadamu na vitu hivi viwili .

Ni Mtume yuleyule aliyetokea kwenye jamii iliyojaaa uovu lakini Mwenyezi Mungu akamletea kitabu kiwe mwanga wa kuangaza kiza kilichokuwepo katika vitabu vingine vilivyokuwepo.

Hekima na busara vikaingia mioyo ya wanadamu wenye kiu ya utu, ilikua ni mwanzo wa elimu na maarifa ya kweli.

Alikua ni Mtume aliewafunulia wanadam kitabu kitakatifu cha Mwenyezi Mungu ambacho hakikuwepo kabla akawa ndiye mkalimani wa lugha zilizokua hazijulikani katika ulimwengu kwa kupigania haki zilizopotea mwenye nafsi wanyonge na kuwainua daraja kutoka watu dhahili kabisa mpaka kuwa viumbe bora katika ulimwengu huu.

Mwenyezi Mungu akamjalia Mtume (s.a.w) kuwa mfano bora kwa wanadamu na kumfanya kiigizo chema kwa watu. Tabia njema na mienendo bora ya maisha hayo ukawafikia wanadamu kwa kupitia matendo na mawaidha mazuri ya utume (s.a.w)

Aisha (r.a) alipozaliwa maadili na tabia za Mtume (s.a.w) alisema mienendo na tabia zake zilikua kama Qur'an.

Siri nzima ya maisha ya Mtume (s.a.w) ilikua ni tafsiri ya Qur'an tukufu aliyoshushiwa yeye bwana Mtume katika kutambua mchango mkubwa wa Mtume wa Mwenyezi Mungu.

Mtume (s.a.w) alikua ni mhimili wa maadili ambao haujawahi kushuhudiwa katika historia ya mwanadamu. Na wafuasi wake watiifu, Maswahaba wa Mtume (s.a.w) walijitahidi kufuata kile alichokisema wakaiga mienendo yake na kuishika imani. Kumfuata Mtume wa Mwenyezi Mungu rehma na amani juu yake kukawafanya Maswahaba wafuzu na hata Mwenyezi Mungu akawasifia katika Qur'an

Na wale walio tangulia, WA kwanza, katika Wahajiri Na Ansari, Na walio wafuata Kwa wema, Mwenyezi Mungu ameridhika nao, Na wao wameridhika naye; Na amewaandalia Bustani zipitazo Mito kati yake, na wadumu humo milele. Huko ndiko kufuzu kukubwa. (At-Tawbah, 100)

Ewe Mwenyezi Mungu ... tujaalie sisi kuwa na tabia na maadili mema ya kiislam, uturuzuku rizki za halalli na utufanye ni waja wenye kuyasikia maneno yako na ya Mtume wa Mwenyezi Mungu na kisha kuyafuata,utupeshe na njia ya wale uliowakasirikia na utufanye wenye tabia na mienendo kuwa kama ya Mtume wako Muhammad (s.a.w)! katika Qur'an.

Amin!

YALIYOMO

Dibaji **5**

Jamii Ya Watu Wa Zama Za Furaha **11**

Imani zenye kudhalilisha katika Zama za Ujahiliya 12

Kmtumikia Mwenyezi Mungu na Kuwahudumia Viumbe Wake Yaliyopuuzwa kwa Maslahi ya Kidunia 16

Mabaki ya Sifa za Kimaadaili Yalipotoshwa na Kugeuzwa 17

Muujiza Mkuu wa Mtume (s.a.w): Mtu wa Asr-u Saadah 23

Zama za Furaha Ziliwaibua Watu wa Mfano... 25

Maswahaba walipata nini kutoka kwa Mtume Aliyebarikiwa (s.a.w) ? 27

Uislamu Unasambaa Kwa Haraka kama Mwanga wa Alfajiri..... 29

Hisia za kiroho ziliimarika na kustawi..... 30

Akili na Moyo Vilikuwa Sawia katika Utendaji Kazi 33

Kutafakari Ndiyo iliyokuwa Nguzo..... 35

Kulingania Uislamu ndio Kazi Waliyoipenda na Kuifurahia mno 35

Walishikamana na Qur'an 38

Mambo ya Yaliyowaelekeza Kwenye Qur'an Tukufu..... 40

Binadamu Wote Waliwastaajabia..... 41

Maadili ya Kiislamu Yanatekelezeka, Sio Nadharia 42

Msisimko wa Imaan katika Jamii ya Asr-u Saadah . 47

Walikimbilia Kujiunga na Safu za Uislamu 48

Hawakusita Kujitolea Maisha yao kwa Ajili ya Imaan 49

Walipambana na Kufanya Hijra kwa ajili ya Kulinda Imani yao..... 55

Msisimko wa Ibada Katika Zama Za Furaha..... 63

Walikuwa Waangalifu Kutunza Udhu Wao Wakati Wote 63

Swala Ilikuwa Nuru ya Macho yao 67

Hawakujitenga na Jamaa..... 71

Walitoa Zaka na Sadaka Hali ya kuwa ni Wenye Furaha 73
Kujitolea ilikuwa Kiini cha Maisha yao 78
Waligundua kuwa Hakuna Zaidi ya Funga..... 83
Walizipokea Kwa Shauku Hijja Na Umrah..... 86
Walienzi Sana Kujifunza Qur'an na Sunnah ... 90
Walitafuta Tiba na Ponyo Kutoka Katika Qur'an Tukufu..... 98
Walikuwa Wakitubu Wakati wa Mapambazuko..... 100
Walikuwa Wenye Bidii Kwenye Matendo ya Ibada 105
Walikuwa Wakishindana Kutenda Mema 105
Walifuata Sunnah Hatua kwa Hatua..... 107

Ukomavu wa Kimaadili Katika Zama Za Furaha . 117
Walikuwa Vilele vya Unyenyekevu..... 118
Walikuwa Bahari ya Huruma..... 120
Walipenda Kuwasamehe Watu kwa Ajili ya Mwenyezi Mungu..... 123
Walijipamba kwa sifa Mbili Za Mtume: Mkweli na Mwaminifu 128
Walikuwa Wingi wa Huruma Katika Ukarimu na Kutoka Wabinafsi..... 130
Waliepuka Israfu..... 134

Walitilia Umuhimu Mkubwa Juu ya Malezi ya Kiislamu 137

Maadili Yao ya Kibiashara yalikuwa ya Kipekee 138

Udugu Wao Wa Kiislamu Ulikuwa wa aina Yake 139

Jamii Ilitawaliwa na Kuheshimiana na Kuwajali Wengine 144

Walijizuia Na Zinaa 147

Nyuso Zao Zilikuwa Na Tabasamu Daima 151

Kwa Mukhtasari 154